

SERA YA LUGHA KATIKA ELIMU NA UKUZAJI WA KISWAHILI NCHINI

UGANDA

NA

AGUME INNOCENT

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA
LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI
YA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

CHUO KIKUU CHA MOI

2022

IKIRARI**Mtahiniwa**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine ili kutimiza mahitaji ya shahada ya digrii. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa au kuchapishwa bila idhini ya mwandishi au /na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: _____

Tarehe: _____

AGUME INNOCENT**SASS/PGK/01/2019****Wasimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ridhaa yetu tukiwa wasimamizi wa Chuo Kikuu.

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Prof. Nathan O. Ogechi

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Prof. Mark Mosol Kandagor

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

TABARUKU

Kwa mke wangu Nabimanya Consolate na watoto wangu wapendwa Agume Leo Baraka na Agume Arnold Amani.

Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda na kuwahudumia daima dawamu.

SHUKURANI

Shukrani za dhata ni kwa Mwenyezi Mungu, anayenilinda na kunijalia amani na afya kila uchao.

Kwa heshima na taadhima pamoja na mapenzi ya dhata, ninawashukuru wazazi wangu pamoja na ndugu zangu wote kwa mchango na maelekezo waliyonipa tangu utotoni hadi leo. Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda na kuwabariki.

Nishukuru bila kikomo pia, mpango wa Ufadhili wa Malkia wa Uingereza kwa Wanafunzi kutoka Nchi za Jumuiya ya Madola Duniani kwa kunifadhili na kunipa fursa ya kujiendeleza kimasomo katika kiwango cha uzamili. Ninashukuru pia Chuo Kikuu cha Moi kwa kunipa nafasi ya kusomea shahada hii.

Kwa wasimamizi wangu Prof. Nathan O. Ogechi na Prof. Mark Mosol Kandagor pamoja na wahadhiri wangu wote idarani, ninasema asanteni sana kwa mafunzo na maelekezo mliyoniya ya kutimiza na kufaulisha malengo yangu ya kiakademia hapa Chuo Kikuu cha Moi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda na kuwaendeleza kwa kila hali na mali.

IKISIRI

Kiswahili ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa Afrika Mashariki. Hutafitiwa na hufundishwa katika nchi mbalimbali barani Afrika na nje. Itifaki ya Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inatambua Kiswahili kama lugha ya mawasiliano ya kikanda. Aidha, katiba ya nchi ya Uganda ya 1995 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005, hati maalumu za serikali kama vile “*The government white paper*” ya 1992, zinatoa matamko bayana kuhusu uendelezaji wa Kiswahili nchini Uganda. Licha ya matamko ya kikatiba na mapendekezo kutoka hati mbalimbali za serikali, maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda, hayajaenda sambamba na ya nchi nyingine za Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa sera ya lugha ya elimu katika uendelezaji wa Kiswahili nchini Uganda. Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo: kujadili nafasi ya sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda, kufafanua changamoto zinazokumba ukuzaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda na kufafanua suluhu za changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda. Data zisizo za kitakwimu zilikusanywa katika utafiti huu huku usampulishaji wa kimaksudi ukitumika kwa watafitiwa kumi na watatu kutoka taasisi za serikali na za binafsi jijini Kampala. Njia ya upekuzi wa nyaraka maktabani na uchambuzi wa data za kiyaliyomo zilitumika. Aidha, mahojiano na maafisa kutoka taasisi zilizohusika yalifanywa. Hali kadhalika, Nadharia ya Upangaji Lugha ya Einer Haugen ilitumika katika utafiti huu. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa kuna nyaraka nyingi za sera, maagizo na matamko ambayo yanakipa Kiswahili hadhi ya kukuzwa na kuendelezwa kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda. Hata hivyo, hali hii inakwamishwa na changamoto kama vile: ukosefu wa mikakati ya kutekeleza sera za lugha kuhusu Kiswahili, ukosefu wa utashi thabiti wa kisiasa, mvutano na mashindano kati ya lugha za kiasili na Kiswahili, mtazamo hasi kwa Kiswahili, serikali kutoajiri walimu wa kutosha wa Kiswahili na uhaba wa vifaa vya kufundishia shuleni. Suluhu za changamoto zinazokumba ukuzaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu zilizojadiliwa ni: serikali kuwekea mkazo utekelezaji wa sera kuhusu lugha ya Kiswahili, kuunda baraza la Kiswahili la kitaifa, kuhamasisha watu kwa wingi kuhusu manufaa ya Kiswahili, kuandaa warsha za kuboresha mbinu za ufundishaji kwa walimu wa Kiswahili, kuandaa na kutoa vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia, kuthamini mtaala mpya wa sekondari unaozingatia umilisi na kuandaa vituo vya kujifunzia Kiswahili katika jamii. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa; watunga sera na wapangaji lugha, wakuza mitalaa na wadau wengine katika sekta ya elimu kuhakikisha utekelezaji wa mikakati mwafaka ya ukuzaji wa Kiswahili kupitia elimu. Utafiti huu pia unachangia maarifa yaliyopo kuhusu sera na mipango ya lugha pamoja na maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda katika mipaka ya elimu. Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yatakuwa msingi wa tafiti za baadaye kuhusu masuala ya sera ya lugha pamoja na maendeleo ya Kiswahili kupitia mawanda mengine kama utamaduni, bungeni, biashara na kwingineko.

ABSTRACT

Kiswahili is a Bantu language majorly spoken in East Africa. It is also being taught and researched in some other African countries and across the globe. Besides Kiswahili being pronounced in the East African Community Treaty under article 137 as a *lingua franca* of the East African region, its development in Uganda is not at the same footing compared to the situation in other East African member states. The 1995 constitution of Uganda that was reviewed in 2005, the Government White Paper of 1992 on Education reform in Uganda, and other government language policy statements, clearly spells out how Kiswahili should be developed in Uganda. Besides all this, the fate of Kiswahili in Uganda is still unpredictable. Therefore, this study sought to investigate the language policy in education sector and its influence on development of Kiswahili language in Uganda. The objectives of this study were: To discuss the position of language policy on the development of Kiswahili in Uganda through education system, to explain the challenges affecting the growth of Kiswahili through education system and to explain the possible solutions to the challenges affecting the growth of Kiswahili through education system in Uganda. This qualitative research was guided by a case study research design that provided room for purposive sampling. Thirteen respondents from thirteen government and private entities concerned with language policy and language planning together with its implementation were interviewed from within Kampala city. Interview schedule, library research and content analysis were used as methods for data collection. Similarly, Einer Haugen's language planning fourfold model was used in this study. The findings of the study indicate that there are numerous policy documents, decrees and pronouncements that should be enhancing the development of Kiswahili through the education sector. However, this is hampered by challenges like lack of strategies to implement Kiswahili language policies, lack of strong political will, ethno linguistic competitions, negative attitude towards Kiswahili, inadequate deployment of Kiswahili teachers and shortage of teaching-learning Kiswahili materials. A number of solutions to mitigate such challenges were discussed and these include: government to mainstream Kiswahili language policy, mass sensitization about importance of Kiswahili to be done, retooling of Kiswahili language teachers, provision of enough teaching and learning materials, embracing the competency based curriculum, formation of National Kiswahili Council and to open Kiswahili learning centers in communities. The outcomes of this study will benefit; the language policy makers and language planners, curriculum developers and other education stake holders in ensuring smooth implementation of policies in education that support the growth of Kiswahili in Uganda. This research contributes to the existing knowledge about language policy and planning in relation to the development of Kiswahili in Uganda's education system. It also forms a basis for further research about language policy and planning in relation to its role towards the development of Kiswahili through other fields such as culture, parliament, business and beyond.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKURANI	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT	vi
YALIYOMO	vii
ORODHA YA MAJEDWALI	xi
MAELEZO YA ISTILAHI NA VIFUPISHO	xii
SURA YA KWANZA	1
MISINGI YA UTAFITI	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Utafiti.....	1
1.2 Suala la Utafiti	4
1.3 Malengo	5
1.4 Maswali ya Utafiti.....	5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	5
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	6
1.6.1 Upeo	6
1.6.2 Mipaka.....	7
1.7 Umuhimu wa Utafiti	7
1.8 Muhtasari wa Sura	8
SURA YA PILI.....	9
MAPITIO YA MAANDISHI NA MWIMO WA NADHARIA	9
2.0 Utangulizi.....	9
2.1 Mapitio ya Maandishi	9
2.1.1 Dhana ya upangaji lugha	9
2.1.2 Dhana ya sera ya lugha.....	11
2.1.3 Sera ya lugha katika elimu	15
2.2 Mwimo wa Nadharia.....	18
2.2.1 Nadharia ya Upangaji Lugha (UL) ya Einer Haugen (1966, 1983)	19
2.2.1.1 Uteuzi.....	20
2.2.1.2 Ukuzaji msimbo.....	20

2.2.1.3 Utekelezaji	21
2.2.1.4 Upanuzi.....	21
2.3 Muhtasari wa Sura	23
SURA YA TATU.....	24
MBINU ZA UTAFITI.....	24
3.0 Utangulizi.....	24
3.1 Mkabala wa Utafiti	24
3.2 Msuko wa Utafiti	24
3.3 Eneo la Utafiti	25
3.4 Utafiti Mwigo.....	26
3.5 Watafitiwa.....	27
3.6 Sampuli na Usampulishaji	29
3.7 Ukusanyaji wa Data	30
3.7.1 Mahojiano.....	30
3.7.2 Utafiti wa maktabani	33
3.7.3 Uchambuzi wa data za kiyaliyomo	34
3.8 Vifaa vya Kukusanya Data	35
3.9 Taratibu za Ukusanyaji Data.....	36
3.10 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data	37
3.11 Uhakikisho wa Uaminifu katika Utafiti.....	39
3.11.1 Ukweli	39
3.11.2 Uhawilishi	39
3.11.3 Utegemeaji.....	39
3.11.4 Uhakika	40
3.12 Maadili katika Utafiti.....	40
3.13 Muhtasari wa Sura	41
SURA YA NNE	42
NAFASI YA SERA YA LUGHA KATIKA UKUZAJI WA KISWAHILI	
NCHINI UGANDA KUPITIA MFUMO WA ELIMU.....	42
4.0 Utangulizi.....	42
4.1 Matamko ya Sera ya Lugha Kuhusu Ukuzaji wa Kiswahili	43
4.1.1 Tume za serikali tangu uhuru	43
4.1.2 Sheria ya Kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.....	45
4.1.3 Katiba ya Uganda	46

4.1.4 Mitaala ya elimu	47
4.2 Hadhi ya Sera ya Lugha katika Elimu Kuhusu Kiswahili	49
4.3 Muhtasari wa Sura	60
SURA YA TANO	61
CHANGAMOTO ZINAZOKABILI UKUAJI WA KISWAHILI KUPITIA	
MFUMO WA ELIMU NCHINI UGANDA.....	61
5.0 Utangulizi.....	61
5.1 Ukosefu wa Utashi wa Kisiasa	61
5.2 Ukosefu wa Mikakati ya Kutekeleza Sera ya Lugha kuhusu Kiswahili	66
5.3 Serikali Kutoajiri Walimu wa Kutosha wa Kiswahili.....	68
5.4 Uhaba wa Vifaa na Rasilimali za Kufundishia na kujifunzia Kiswahili	71
5.5 Mvutano Kati ya Lugha za Kiasili na Kiswahili.....	75
5.6 Mtazamo hasi kwa Kiswahili.....	78
5.7 Muhtasari wa Sura	82
SURA YA SITA.....	83
SULUHU ZA CHANGAMOTO ZINAZOKUMBA UKUAJI WA KISWAHILI	
KUPITIA SEKTA YA ELIMU NCHINI UGANDA	83
6.0 Utangulizi.....	83
6.1 Uhamasishaji wa Kijumla	83
6.2 Kozi za Uboreshaji wa Stadi za Ufundishaji kwa walimu wa Kiswahili	86
6.3 Uundaji wa Baraza la Kitaifa la Kiswahili	87
6.4 Kuweka Mkazo kwenye Utekelezaji wa Matamko ya Sera kuhusu Lugha ya Kiswahili	90
6.5 Utoaji wa Vifaa vya Kutosha vya Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili	92
6.6 Kukubali na Kuthamini Mtaala Mpya wa Sekondari Unaozingatia Umilisi	95
6.7 Kuandaa na Kufungua Vituo vya Kujifunzia Kiswahili katika jamii	96
6.8 Muhtasari wa Sura	99
SURA YA SABA	101
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	101
7.0 Utangulizi.....	101
7.1 Muhtasari wa Utafiti	101
7.2 Matokeo na Mahitimisho ya Utafiti	102
7.2.1 Nafasi ya sera ya lugha katika ukuzaji na ukuaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda	102

7.2.2 Changamoto zinazokabili maendeleo ya lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda	104
7.2.3 Suluhu za changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda	105
7.3 Mapendekezo	106
7.3.1 Tafiti za baadaye	108
MAREJELEO	110
VIAMBATISHO.....	119
Kiambatisho I: Kielekezi cha mahojiano kwa watungaji na waratibu wa sera ya lugha (DEO KCCA, NCDC, UNEB, NCHE, ESC, LIMUK).....	119
Kiambatisho II: Kielekezi cha mahojiano kwa watekelezaji wa sera ya lugha (Walimu, Wadarisi na Wahadhiri)	121
Kiambatisho III: Kielekezi cha mahojiano kwa watekelezaji na waratibu wa sera ya lugha (Wachapishaji).....	123
Kiambatisho IV: Kielekezi cha mahojiano kwa watetezi wa haki ya lugha ya Kiswahili (CHAKITAU).....	124
Kiambatisho V: Kielekezi cha tathmini ya nyaraka	125
Kiambatisho VI: Idhini ya Kitivo na Idara.....	126
Kiambatisho VII: Idhini ya Kurugenzi ya Elimu na Huduma za Kijamii ya Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji Kuu la Kampala (KCCA)	128

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Nadharia ya UL ya Einer Haugen (1966, 1983).....	20
Jedwali 3.1: Watafitiwa	29

MAELEZO YA ISTILAHU NA VIFUPISHO

CHAKITAU – Chama Cha Kiswahili cha Taifa - Uganda

CoK – Constitution of Kenya

CoU – Constitution of Uganda

EAC – East African Community

EACT – East African Community Treaty

EALA – East African Legislative Assembly

ESC – Education Service Commission

EPRC – Education Policy Review Commission

GoU – Government of Uganda

IMU – Instructional Materials Unit

Ip – Interviewed person

MT – Mtafitiwa

NCDC – National Curriculum Development Centre

NCHE – National Council for Higher Education

UBoS – Uganda Bureau of Statistics

UL – Upangaji lugha

UNCP – Uganda National Culture Policy

UNEB – Uganda National Examinations Board

UPDF – Uganda People's Defence forces

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea utangulizi wa jumla kuhusu misingi ya utafiti. Sura hii inabainisha usuli na suala la utafiti. Aidha, malengo, maswali, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka pamoja na umuhimu wa utafiti vimejadiliwa.

1.1 Usuli wa Utafiti

Utafiti huu ulitathmini jinsi sera ya lugha katika mfumo wa elimu ilivyoathiri ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Wataalamu wa upangaji na ukuzaji wa lugha kama vile, Fishman (1986), Wolff (2006), Albury (2015), na Groff (2018), wamedai kwamba siasa pamoja na lugha ya kufundishia shuleni, ni mihimili miwili mikuu kati ya mihimili mingineyo inayochangia ufanisi au kufeli kwa sera yoyote ya lugha hasa katika mazingira ya wingi lugha.

Mathalan, ufanisi wa Kiswahili kama lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Tanzania umetokana na siasa za aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Julius Kambarage Nyerere. Katika enzi za utawala wake, Nyerere alichangia pakubwa katika uidhinishaji na uendelezaji wa Kiswahili kama lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Tanzania (Mulokozi, 2001; Legere, 2006, 2009). Vivyo hivyo, kubadilika kwa hadhi ya Kiswahili nchini Kenya hasa baada ya mwaka 1983, kulitokana na siasa za aliyekuwa rais Hayati Daniel Arap Moi, aliyebadilisha mfumo wa elimu kutoka 7-4-2-3 hadi 8-4-4 ambapo Kiswahili kilifanywa somo la lazima kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne (Mazrui & Mazrui, 1998; Ogechi, 2001; Simala, 2003). Isitoshe, imedaiwa kwamba kuimarika kwa kiasi cha matumizi ya Kiswahili nchini Uganda katika miktadha rasmi kunahusishwa na siasa za aliyekuwa rais nchini humo, Iddi

Amin alipotangaza Kiswahili kama lugha ya taifa mnamo 1973 (Mukama, 1990; Mulanga, 2006; Kingei, 2010; Jjingo 2011; Masereka, 2018).

Waama, wanasiasa (hasa waliotajwa hapo juu) wamechangia pakubwa katika maendeleo ya Kiswahili kuanzia wakati walipofufua Jumuiya ya Afrika Mashariki na kusaini mkataba ambao umeeleza kwamba juhudi zafaa kuendeshwa ili kuhakikisha kwamba Kiswahili ni lugha ya kazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC, 2006). Licha ya siasa, matumizi ya lugha katika elimu kama somo na lugha ya kufundishia huchangia pakubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha (UNESCO, 1953; CIA, 2010; Groff, 2018). Mifano ya majaribio ya matumizi ya lugha asilia kama vile Yoruba nchini Nigeria (Bangbose, 2004) na Kiswahili nchini Tanzania hadi darasa la saba (Rugemalire, 2003, 2004, 2006) imeonyesha kwamba, lugha inapotumika katika kufundishia masomo mengine, kufundishwa kama somo na kutahiniwa, ufanisi wa ukuzaji na uendelezaji wa lugha hiyo hutokea (Groff, 2018). Isitoshe, katika utafiti wao juu ya sera ya lugha ya kufundishia na haki za lugha nchini Kenya, Kembo-Sure & Ogechi (2009), walibainisha kwamba uwekezaji katika lugha ya kufundishia huchangia ama kichanya au kihasi maendeleo ya lugha mbalimbali.

Uganda ni nchi yenye wingi lugha ikiwa na lugha takribani 45 za kiasili (Walusimbi, 1973; Tembe, 2008; King'ei, 2010; Jjingo, 2011). Fauka ya lugha hizi za kiasili, kunazo lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kichina, Kiitaliano, Kijerumani na nyingine pamoja na Kiswahili kama lugha ya Kiafrika. Kiingereza na Kiswahili zinatumiwa kwa mapana zaidi kuliko hizo nyingine za kigeni (Viser na Jjingo, 2017; Masereka, 2018). Lugha hizi vilevile hutumiwa katika mfumo wa elimu kama lugha ya kufundishia (Kiingereza) au kama somo (Kiswahili).

Itakumbukwa kwamba Kiswahili kilipendekezwa kuwa lugha rasmi ya pili baada ya Kiingereza kikatiba nchini Uganda (R.O.U, 1995). Pia Kiswahili ni lugha inayopangiwa kuwa lugha ya kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC, 2006). Kwa hivyo, kisiasa, uteuzi wa Kiswahili umekwishafanywa kama lugha ya Jumuiya. Kiswahili kimependekezwa kama lugha rasmi ya pili ya taifa na somo shuleni katika elimu kutoka shule ya msingi hadi Chuo Kikuu nchini Uganda (GoU, 1992; Albaugh, 2012).

Hata hivyo, ufanisi wa Kiswahili, kama somo katika elimu utategemea juhudi na utekelezaji katika lugha hiyo. Kutokana na hali hii, maswali kadhaa huibuka: Je, kuna juhudi gani zilizowekwa kurahisisha ufanisi wa kufundisha Kiswahili? Je, kuna mandalizi ya walimu wa kufundisha Kiswahili kupitia mafunzo ya vyuo vya walimu? Iwapo ndiyo, mafunzo hayo yanalenga walimu wa viwango vipi kati ya chekechea, msingi, sekondari, vyuo anuai na vyuo vikuu? Je, mafunzo hayo, yanasaidiwa vipi na vifaa vya kufundishia lugha kama vile maktaba na vitabu? Je, yapo mashirika ya uchapishaji yanayopokea miswada ya Kiswahili? Iwapo ndiyo, kuna changamoto zozote zinazohusiana na ukubalikaji wa haraka kwa miswada ya Kiswahili? Je, wapo watunzi Wanauganda wanaotunga kwa Kiswahili? Iwapo idadi yao si kubwa, wapo watunzi kutoka nje? Ni vipi nchi za Afrika Mashariki zinashirikiana katika kukuza Kiswahili nchini Uganda? Je, serikali ya Uganda inatoa motisha gani kwa wanaofundisha Kiswahili? Mathalan, waliohitimu kama walimu wa Kiswahili wanapata ajira? Iwapo ndiyo, ni baada ya kipindi gani kufuatia kufuzu kwao? Je, kuna shughuli au juhudi zozote za serikali zinazokagua ubora wa vifaa na ufundishaji wa Kiswahili? Je, mbali na ufundishaji rasmi darasani, kuna jitihada gani za ziada zinazosaidia ukuzaji wa Kiswahili katika elimu nchini Uganda?

Maswali haya yanaweka msingi kuhusu mambo muhimu yanayoshughulikiwa katika utafiti huu.

1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu uliazimia kuchunguza mchango wa sera ya lugha katika shughuli za kukuza na kuendeleza Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu. Kwa mujibu wa nyaraka za serikali na baadhi ya tafiti ambazo ziliwahi kufanywa zikijihusisha na suala la sera ya lugha nchini Uganda, Kiswahili kimekubalika kama lugha rasmi ya pili nchini Uganda (CoU, 2005). Kiswahili pia kinaruhusiwa kufundishwa Kama somo la lazima katika shule za msingi, vyuo vya walimu wa shule za msingi na vyuo vya kiufundi (GoU, 1992). Aidha, nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki ambako Uganda ni nchi mwanachama, zilisaini mkataba unaopendekeza Kiswahili kuwa lugha ya kazi ya kikanda (EAC, 2006). Licha ya mapendekezo na matamko ya sera ya lugha kuhusu uendelezaji wa Kiswahili, kufikia sasa, juhudi za maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda hasa kupitia sekta ya elimu bado hazijakita mizizi. Kuna baadhi ya vyuo, taasisi na shule hasa za sekondari ambazo hazina walimu wa Kiswahili wa kutosha walioajiriwa na serikali licha ya Kiswahili kuwa somo la lazima kwenye ngazi hizo za elimu. Isitoshe, katika baadhi ya shule ambazo ziliamua kufundisha Kiswahili kama somo la hiari, kuna wanafunzi wachache sana wanaoamua kuendelea kusoma Kiswahili hadi kidato cha nne na sita. Kwa hivyo, Kiswahili, nchini Uganda hakijakita mizizi kimatumizi ikilinganishwa na vile hali ilivyo katika nchi nyingine wanachama katika Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Suala hili linazua dukuduku iwapo kuna utekelezaji kikamilifu wa matamko na mapendekezo ya sera kuhusu ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Utafiti huu basi unafafanua msimamo wa sera ya lugha katika ukuzaji na ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kwa kujikita kwenye mfumo wa elimu.

1.3 Malengo

Kwa kujikita katika mfumo wa elimu nchini Uganda, utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

- i. Kujadili nafasi ya sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili.
- ii. Kufafanua changamoto zinazokumba ukuzaji wa Kiswahili.
- iii. Kufafanua suluhu za changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili.

1.4 Maswali ya Utafiti

- i. Sera ya lugha nchini Uganda ina nafasi gani katika uendelezaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu?
- ii. Ni changamoto zipi zinazokabili ukuzaji wa Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Uganda?
- iii. Ni masuluhisho yapi yanayoweza kutatua changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Kwa kiasi kikubwa, hali ya sera ya lugha nchini Uganda kwa sasa ni changamano. Uganda ni nchi ya wingi lugha na kuna zaidi ya lugha 45 zinazozungumzwa nchini humo. Kiswahili kama lugha mojawapo ya lugha za kibantu, huzungumzwa na baadhi ya Wanauganda na hutazamwa kama lugha ya umoja, inayoweza kufunzwa na kuzungumzwa na wengi kwa vile haihusishwi na kabila lolote maalumu nchini Uganda (Walusimbi,1973; King'ei, 2010). Kwa hivyo, uendelezaji wa Kiswahili nchini Uganda utaimarisha umoja miongoni mwa raia na kupunguza hali ya uwezekano wa changamoto zinazoweza kusababishwa na masuala ya ukabila.

Aidha, mkataba na protokali ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki vilipendekeza Kiswahili kama lugha ya mawasio katika Jumuiya. Kwa hivyo,

uendelezaji wa Kiswahili nchini Uganda, utakuwa juhudi mojawapo ya kuimarisha mawasiliano katika ukanda wa Afrika Mashariki. Suala hili litadumisha ushirikiano katika muungano, kwa mfano katika soko la pamoja na katika shughuli za kisiasa.

Isitoshe, kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu suala la sera ya lugha nchini Uganda (Utne, 2000; Tembe, 2008; Jjingo, 2011) na imegunduliwa kwa makubaliano kwamba dhima ya Kiswahili nchini Uganda kwa ujumla ilikuwa changamano. Kulipendekezwa 87tafiti nyingine kufanywa katika mawanda mengine kuhusu maendeleo ya Kiswahili. Kwa hivyo, hakuna ushahidi uliojitokeza kuwa kuna utafiti ambao ulikuwa umefanywa kuhusu suala la sera ya lugha na mchango wake katika ukuzaji na ukuaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda. Hivyo basi kuacha pengo la kutafitia ambalo ndicho kilikuwa kiini cha utafiti huu.

Kwa hivyo, matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa watafiti wengine, walimu, wasomi, watunzi wa mitaala na wapangaji wa sera ya lugha katika kutambua utegemeano au mchango wa sera ya lugha ya elimu na ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda.

Utafiti huu pia unalenga kuongeza maarifa yaliyopo kuhusu suala la sera ya lugha na maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda, jambo ambalo litahamasisha watafiti wa siku zijazo na kuwapa ari ya kutafitia suala husika katika mawanda mengine mbalimbali.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

1.6.1 Upeo

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza utekelezaji wa sera ya lugha katika elimu kwa kuangazia maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda. Kwa hivyo, ulijikita katika mipaka ya mfumo wa elimu nchini Uganda na wala si sekta nyingine za jamii. Utafiti huu ulifanyika jijini Kampala katika wilaya ya Kampala nchini Uganda. Mtafiti aliteua Jiji

la Kampala kwa sababu ya uwezekano wa kuwapata watafitiwa aliowalenga. Hii ni kwa sababu makao makuu ya ofisi za taasisi mbalimbali za kiserikali pamoja na za kibinafsi zinazohusika katika masuala ya uundaji na utekelezaji wa sera ya lugha hususan Kiswahili hupatikana jijini humu. Pia jiji la Kampala hutangamanisha watu mbalimbali kutoka makabila mbalimbali kote nchini.

1.6.2 Mipaka

Kwa kuliteua jiji la Kampala na mfumo wa elimu pekee, haiwezekani kujumuisha matokeo ya utafiti huu kwa sekta nyinginezo za jamii na taifa zima la Uganda. Hata hivyo, utafiti huu umetoa mwanga wa kinachoendelea kuhusiana na juhudi za kukuza Kiswahili kisera nchini Uganda.

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unachangia maarifa katika uwanja wa kiusomi kuhusu sera ya lugha. Pili, unabainisha rasilimali za kufundishia Kiswahili kwa Wanauganda ambao kwao Kiswahili ni lugha ya kigeni. Pia unabainisha jinsi ya kuchuma nafuu ya rasilimali ili kukuza lugha. Utafiti huu umeonyesha mwanya kati ya sera ya lugha iliyotangazwa na utekelezaji wa sera hiyo, pamoja na kuonyesha utegemeano na utegemezi katika kukuza lugha nchini.

Matokeo ya utafiti huu pia yametoa mwongozo kwa wadau wanaojihusisha na utunzi wa sera pamoja na wanaohusika na uendelezaji wa Kiswahili nchini Uganda, kama vile wakuza mitalaa na walimu katika kutambua changamoto zinazokikumba Kiswahili na kupendekeza mikakati mwafaka ya kukabiliana na changamoto hizo.

Utafiti huu pia unadhihirisha ufanisi na ufaafu wa nadharia ya upangaji lugha ya Haugen kwamba sera rasmi kuhusu uchaguzi wa lugha ya taifa au rasmi ni muhimu kupewa kipaumbele na kutekelezwa kwa ajili ya ukuzaji wa lugha husika iliyoteuliwa.

1.8 Muhtasari wa Sura

Sura hii kwa ujumla, imeelezea misingi ya utafiti. Imeanza kwa kujadili usuli na suala la utafiti. Sura hii pia imejadili malengo na maswali ya utafiti. Aidha, imeelezea sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka pamoja na umuhimu wa utafiti ulioendeshwa.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MWIMO WA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tutapitia tafiti zilizotangulia kuhusu upangaji lugha, sera ya lugha kiujumla na kisha tuangazie upangaji lugha na Sera ya lugha katika elimu. Aidha, sura hii itajadili mwimo wa nadharia uliotumika katika kuendesha utafiti huu.

2.1 Mapitio ya Maandishi

2.1.1 Dhana ya upangaji lugha

Schiffman (1996); Hult (2010) anadai kwamba, upangaji lugha ni juhudi za kimakusudi katika kusuluhisha matatizo yote kuhusu lugha na ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa lugha husika. Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1991) inasema kuwa upangaji lugha ni jitihada za kuweka sera mbalimbali za lugha ambazo husaidia kutatua tatizo la mawasiliano katika jamii kwa kuchunguza lugha na lahaja zilizopo ili kuteua zinazofaa kutumika. Kwa hivyo, hii inamaanisha kwamba serikali fulani huchukua sera fulani kuhusiana na lugha zinazozungumzwa katika jamii fulani na kutekeleza sera hiyo kwa njia ya upangaji lugha.

Haugen (1966); Sung (2020) anadai kwamba upangaji lugha ni utathmini wa mabadiliko ya lugha. Ni shughuli ya kutayarisha tahajia, sarufi na kamusi sanifu kuwaongoza wazungumzaji hasa katika jamii za wingi lugha. Aidha, upangaji lugha huchukulia lugha kama amali na rasilimali ya jamii inayoweza kufanyiwa mabadiliko na inayohitaji hatua zilizopangwa au zilizoratibiwa kupitia juhudi za pamoja za mamlaka za kisiasa, kielimu, kiuchumi na kiisimu (Rubin na Jernudd, 1971). Kadhalika, Rubin na Jernudd (1971) wanaonelea kuwa Upangaji lugha ni juhudi za kuleta mabadiliko katika lugha ya maandishi au mazungumzo au zote mbili

zinazochukuliwa na taasisi zilizoundwa kutekeleza jambo hili. Hunuia kumaliza matatizo ya lugha kwa kuchukua uamuzi ulio bora zaidi. Kwa hivyo, upangaji wa lugha unamaanisha maendeleo, utekelezaji na utathmini wa mbinu maalumu za kutatua matatizo mahsusi ya lugha. Kwa ujumla, upangaji lugha ni utatuzi wa matatizo yanayotokana na lugha ili kuleta mabadiliko katika matumizi ya lugha fulani katika jamii.

Upangaji lugha unaangazia ngazi mbili ambazo ndizo huzalisha uteuzi wa lugha moja au zaidi ambayo hutambuliwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali nchini au katika jamii husika (Hornberger, 2006; Sung, 2020). Ngazi hizi ni: Upangaji lugha kihadhi; Hii ni ngazi ambayo inahusu ukuzaji wa matumizi ya lugha kwa kuzingatia dhima au nafasi ya lugha yoyote iwayo katika jamii na mara nyingi ni ngazi inayoamuliwa na nguvu za kisiasa. Ilihali upangaji lugha kikongoo, ni ngazi inayohusu maumbo na muundo wa lugha yenyewe. Ngazi hii hulenga kukuza msamiati na matawi yote ya sarufi ya lugha ambayo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kwa hivyo, ni jitihada za kimakusudi katika kuboresha ngazi mbalimbali za sarufi ya lugha (Jernudd na Gupta, 1971; Abdulaziz, 1993; Jjingo, 2011). Hivyo basi, ufidianaji wa suala la upangaji lugha kihadhi pamoja na upangaji lugha kikongoo ni muhimu sana na uliupa utafiti huu mwanya wa kuchunguzia suala zima kutokana na misingi ya nadharia inayotumika. Upangaji lugha ni muhimu hasa katika jamii zenye wingilugha pale panapohitajika kujenga utaifa miongoni mwa watu wenye tamaduni tofauti tofauti (Haugen, 1987; Carreras 2018). Madai haya yanaafikiana na muktadha wa Uganda ambako kuna lugha tofauti zaidi ya arobaini na tano kutoka makabila mbalimbali. Kwa hivyo, upangaji lugha kwa ajili ya kutekeleza na kuendeleza Kiswahili nchini Uganda hasa kupitia elimu, ni muhimu sana kwa ajili ya kutatua matatizo ya mawasiliano na kujenga utaifa miongoni mwa Wanauganda.

2.1.2 Dhana ya sera ya lugha

Kaplan na Baldauf (1997) wanaelezea sera ya lugha kuwa jumla ya sheria au kanuni ambazo zimetungwa na taasisi zenye mamlaka kama vile serikali ikiwa kama mojawapo ya shughuli za upangaji lugha. Hata hivyo, si lazima kuwa sera zote za lugha zipangiwe au zitambulikane kimataifa. Schiffman (1996) na Hult (2010) wanadai kuwa, sera ya lugha pia ni suala la kijamii. Hushirikisha taratibu za kisheria na utekelezaji wa sheria hizo, hata hivyo hujihusisha na suala zima la utamaduni wa lugha husika kama vile, mifumo ya imani, mielekeo, mila, dini na masuala mengine ya kitamaduni yanayoleta pamoja wazungumzaji wa lugha husika.

Kwa mujibu wa Hornberger (2006), kazi mbalimbali kuhusu sera ya lugha ziliongezeka zaidi katika miaka ya 1990. Mifano ya wataalamu waliojitokeza na kazi mbalimbali kuhusu sera ya lugha ni kama vile Grabe (1994), Hornberger & Ricento's (1996), Huebner na Davis (1999) na Ager's (2001). Fettes (1997), akibainisha uhusiano ulioko kati ya upangaji lugha na sera ya lugha anahitimisha kwamba, upangaji lugha ni muhimu kushirikiana na kuenda sambamba na ukuzaji kikamilifu wa sera ya lugha. Johnson (2013) anadai kuwa watafiti wengi hukubaliana kuwa sera ya lugha na upangaji lugha ni masuala mawili yaliyo na uhusiano ulio wa karibu sana ingawa hizi huwa ni shughuli mbili tofauti. Wengine hudai kuwa upangaji lugha hujumlisha sera ya lugha (Kaplan na Baldauf, 1997) huku wengine wakidai kuwa sera ya lugha hujumlisha upangaji lugha (Schiffman, 1996). Kuna makisio kwamba kuna mipango ambayo hukusudia kuathiri mifumo ya lugha. Hata hivyo, kuna mifano ya sera ya lugha ambayo haipangiwi. Kwa hivyo, masuala mawili haya, upangaji lugha na sera ya lugha huoana na kushiriki pamoja kwa vile huwa na makusudio na malengo yaliyo na uhusiano (Hornberger, 2006)

Aidha, shughuli ya upangaji lugha huweza kuelekeza au kutokana na utunzi wa sera ya lugha na serikali au taasisi au mtu aliyepewa jukumu na serikali. Kwa hivyo, Sera ya lugha ni jumla ya dhana, kanuni na masharti, sheria na vitendo kwa malengo ya kutekeleza maendeleo ya lugha iliyopangwa katika jamii, makundini ya watu au katika mfumo fulani (Kaplan na Baldauf 1997; Johnson 2013), Gazzola (2016). Hali kadhalika, Spolsky (2012): Jjingo (2021) anafasili sera ya lugha kuwa ni zao la maamuzi ya upangaji lugha. Ni seti ya sheria rasmi kuhusu aina za lugha na matumizi katika nchi.

Fettes, (1997) akichunguza ni suala lipi hutangulia lingine kati ya upagaji wa lugha na sera ya lugha, maoni yake huoana na ya Schiffman, (1996) na Ricento, (2000) kuwa si lazima sera ya lugha itokane na upangaji lugha. Hata hivyo, sera yaweza kutungwa kivyake bila kuihusishwa sana na upangaji wa lugha (Fettes, 1997; Hornberger, 2006). Aidha upangaji lugha si lazima uwe na malengo ya kufikia utunzi wa sera ya lugha kwa sababu upangaji lugha ni suala linalokusudia kuleta mabadiliko katika jamii (Rubin na Jernudd, 1971; Cooper, 1989; Tollefson, 1991). Kwa mujibu wa Rubin na Jernudd (1971), Sera ya lugha na upangaji lugha ni masuala yanayopachana katika kushughulikia matumizi, uamilifu na ruwaza za miundo mbalimbali ya lugha katika jamii.

Fathi, (2018) anasisitiza kwamba, Sera ya lugha yoyote ile inafaa kuambatana na kuakisi matakwa ya jamii husika kisiasa, kiuchumi na kijamii. Upangaji lugha hutoa dhima mpya kwa lugha kama vile; kufundishia katika viwango mbalimbali vya kielimu, kutumika kiutawala, na katika shughuli nyingine mbalimbali za kiserikali (Mekacha (2000); Utne na Halla, 2004).

Anne-Marie (2004) anadai kwamba, Sera ya lugha ina jukumu la kubainisha dhima ya kila lugha nchini ili kujiepusha na mitafaruku miongoni mwa watumiaji wa lugha mbalimbali nchini. Kwa mfano mitafaruku inayoweza kutokana na lugha fulani kuangaliwa kama ndiyo muhimu zaidi kuliko lugha nyingine. Anafafanua kuwa sera ya lugha huundwa na taasisi zinazohusika za serikali kama vile bunge au mahakama au taasisi za kibinafsi kwa niaba ya serikali ilihali utekelezaji hushughulikiwa na taasisi mbalimbali za kiserikali au za kibinafsi hasa zilizo katika mawanda ya elimu na dini. Marrie (2004), Blackledge (2008), wanaoanisha madai kuwa wapangaji wa lugha hasa katika nchi zinazoendelea kuwa mara nyingi hawazingatii hali halisi ya matakwa ya kijamii kuhusu lugha bali hutegemea maamuzi ya serikali tawala kuhusu lugha ipi ipewe hadhi au ni gani iendelezwe.

Abdulaziz (1993), Mekacha (2000) na Ogechi (2009) wanaendeleza mjadala huu wakidai kwamba Sera ya lugha inaweza kuangaliwa kwa mitazamo miwili; mtazamo wa kwanza, ni pale lugha ngeni inapopewa hadhi na kutumika kama lugha rasmi au lugha ya taifa na nchi fulani. Ogechi (2009) anadai kwamba, katika nchi ambapo lugha ngeni hupewa hadhi na kuinuliwa kama lugha ya taifa au rasmi, asilimia ndogo sana ya raia huwa na uwezo kutumia lugha hiyo kama lugha yao ya kwanza. Baadhi ya nchi barani Afrika ambazo zimechukua mwelekeo huu ni kama vile Kameruni na Kodivaa huku wakitumia Kifaransa; Angola na Msumbiji wakitumia Kireno, Uganda na Zambia wakitumia Kiingereza.

Mtazamo wa pili ni pale nchi fulani inapoamua na kupatia hadhi lugha mojawapo ya lugha zake za kiasili kutumika kama lugha rasmi au lugha ya taifa. Barani Afrika, baadhi ya nchi ambazo zimefaulu katika kuchukua mwelekeo huu ni kama Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania wakitumia Kiswahili, Uhabeshi pamoja na Somalia wakitumia lugha ya Kiamhari.

Ogechi & Kembo-Sure (2006) hata hivyo, wanadai kwamba shughuli ya upangaji lugha inafaa kuzishughulikia lugha zote katika jamii na kuziendeleza kwa pamoja kama vyombo vya mawasiliano katika ngazi mbalimbali. Abdulaziz (1993) na Jjingo (2011) wanaendelea kueleza kuwa, kupewa hadhi na kuendeleza lugha mojawapo ya zile za kienyeji hapa baarani Afrika, huweza kusababisha ugomvi miongoni mwa lahaja au lugha nyingine ambazo zinakuwa hazijatambuliwa. Basi kwa mujibu wa madai kama haya, tukitoa mfano wa nchi ya Uganda, mgongano kati ya Kiswahili na Kiganda ni bayana kuwa unaweza kuwa tishio kubwa katika uendelezaji wa Kiswahili nchini humo kwa sababu hili limebainika kuwa ni suala la kihistoria. Kiganda ni lugha ya kabila la Waganda na ndiyo inayozungumzwa sana na takribani Wanauganda 4,130,000 (Keith, 1995; Lewis, 2009). Msanjila (2009) anatofautiana na dai hili akisisitiza kuwa mitafaruku miongoni mwa jamii mbalimbali kwa mfano nchini Rwanda, Burundi au Somali, haisababishwi na hali ya kuwa na lugha moja bali ni kwa sababu ya harakati za kupigania utawala na kujinufaisha kijamii na kiuchumi.

Pia kuna Sera ya lugha mseto kama mtazamo mwingine wa Sera ya lugha ambao ni ule unaotoa hadhi sawa kwa lugha mojawapo ya zile za kiasili pamoja na lugha moja ya kigeni na kuziendeleza kisambamba katika muktadha wa nchi fulani (Cobarrubias (1983), Richard (1995), Legère (2002). Lo Bianco (1987) na Tembe (1998) wanakubaliana na wataalamu hawa kuhusu mwelekeo huu na kuwasilisha mfano wa Australia kama nchi mojawapo inayoendeleza mwelekeo huu wa sera ya lugha mseto kwa kuendeleza Kiingereza sambamba na lugha zake za kiasili.

Barani Afrika, baadhi ya nchi ambazo zimeendeleza mtazamo huu wa sera ya lugha mseto ni kama vile Malawi, Kenya, Uganda, Botswana, Uswazi na Jamhuri ya Afrika ya kati. Nchi hizi zote zimeendeleza lugha ngeni moja sambamba na lugha nyingine moja ya kiasili. Kwa mfano, tukirejelea nchi ya Uganda, kwa mujibu wa katiba yake ya 1995, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005, kifungu cha pili katika ibara ya sita, ilitangaza Kiswahili kama lugha rasmi ya pili, ingawa utekelezaji bado unayumba, badala yake imeendelea kuendeleza Kiingereza (Legère, 2002; King’ei 2010).

Sera ya lugha huangaziwa kwa ngazi tatu ambazo ni; ngazi ya kirasmi, kielimu, na kiujumla. Ngazi ya kirasmi, hubainisha ni lugha gani ambayo itatumika katika ofisi za serikali, katika shughuli za utawala, bungeni, mahakamani, na mikutano rasmi ya kiserikali. Kwenye ngazi ya kielimu, sera ya lugha hubainisha ni lugha gani inafaa kufundishia shuleni (Noss, 1971; Fathi, 2018). Kwa mfano nchini Uganda, Kiingereza hutumika katika viwango hivi vya kirasmi a kielimu; kama lugha rasmi pamoja na lugha ya kufundishia shuleni kwa viwango mbalimbali vya kielimu. Ni katika darasa la kwanza hadi darasa la tatu ambapo lugha ya kiasili kulingana na eneo ndiyo hutumika kama lugha ya kufundishia na hili hutumika katika maeneo ya vijijini. Katika maeneo ya mijini, Lugha ya Kiingereza hutumika kama lugha ya kufundishia kutoka darasa la kwanza hadi la saba.

2.1.3 Sera ya lugha katika elimu

Durrani (2012) anadai kwamba, uchaguzi wa lugha yoyote ile kama lugha rasmi bila utekelezaji kwa kuipa hadhi ya kuwa lugha ya kufundishia au kufundishwa shuleni, bila kuiandalia othografia na hata bila kusanifisha msamiati wake, ni suala ambalo halirahisishi matokeo ya utekelezaji katika maendeleo ya lugha hiyo. Aidha, Groff (2016, 2017) anaendeleza maoni haya akidai kwamba lugha yoyote ile kutamkwa

katika hati za serikali kama lugha rasmi hata ikishughulikiwa kiothografia kwa ajili ya kuitambulisha na kuikuza kijamii au kikanda, lakini ikiwa haijapewa fursa ya kufundishwa shuleni au katika taasisi nyinginezo za kielimu kwa ajili ya matumizi yake katika mazungumzo, lengo la utekelezaji wa maendeleo ya lugha hiyo, halitakuwa rahisi kutimia. Shughuli yoyote ya upangaji lugha ambayo haijalenga uchaguzi wa lugha rasmi tu bali hata na kulenga kuendeleza matumizi yake katika jamii hasa ya wingi lugha kama lugha ya pili kwa kuzingatia na kupitia nyanja za elimu, dini, kazi pamoja na kushughulikia usanifu wa othografia yake, na upanuzi wake kileksia, hurahisisha utekelezaji wa maendeleo ya lugha husika katika jamii.

Nchini Uganda, lugha ya kufundishia katika mifumo yote ya elimu ni Kiingereza (GoU, 1992). Aidha, Kiingereza hutumika kama lugha ya kufundishia katika shule za maeneo ya mijini. Shule katika maeneo ya vijijini kutoka darasa la kwanza hadi la tatu hutumia lugha ya jamii husika kama lugha ya kufundishia. Kiingereza hubaki lugha ya kufundishia katika madarasa mengine (Tembe, 2008; Jjingo 2011, 2018).

Nchini Tanzania, lugha ya kufundishia katika shule za msingi za serikali ni Kiswahili halafu Kiingereza hutumika kama lugha ya kufundishia katika shule zote za kiwango cha sekondari na katika taasisi za masomo ya kiwango cha juu pamoja na katika baadhi ya shule za msingi za kibinafsi (Mochiwa, 1998; Msanjila na wenzake, 2009; King'ei, 2010, Jjingo, 2018, 2021). Lugha ya kufundishia nchini Tanzania, imetumika katika ngazi tofauti kama vile imeelezwa hapo juu. Suala hili limeathiri wanafunzi katika uelewa wao wa lugha ya kufundishia pamoja na uelewa wa dhana mbalimbali katika masomo yao darasani. Suala hili pia ni bayana katika muktadha wa shule za msingi nchini Uganda baada ya wanafunzi kumaliza darasa la tatu hasa kutoka vijijini wanapokabiliana na lugha mpya ya kufundishia ambayo ni Kiingereza. Suala hili

huathiri uelewa wa dhana mbalimbali na ufahamu wao masomoni (Tembe, 2008). Inadaiwa kwamba, baadhi ya wanafunzi Watanzania hawapati changamoto katika mitihani tu kwa sababu ya ufahamu mdogo wa lugha bali pia ujuzi mdogo wa Kiingereza cha kutosha huchangia kutofaulu kwa baadhi yao (King'ei, 2010). Aidha, Senkoro (2005) anadai kuwa matatizo ya umilisi wa kutosha katika Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam huwanyima wanafunzi fursa na uhuru wa kujieleza katika Lugha ya Kiingereza huku wakizungumza na wahadhiri wao. Jjingo (2011) pia, akirejelea gazeti la *Mwananchi* la tarehe 19 Desemba, 2009 ukurasa wa tano, anadai kwamba ukosefu wa umilisi wa kutosha katika Kiingereza huwaathiri wanafunzi Watanzania katika matokeo ya mitihani yao. Pamoja na hili, Msanjila na wenzake (2009) wanadai kwamba, Uganda ni nchi mojawapo kati ya nchi za Afrika ambazo bado zinaendeshwa kwa misingi ya sera za lugha za kikoloni. Baadhi ya sera hizi ziliundwa na wakoloni na baadaye zikachukuliwa kikatiba au kutokana na matamko ya marais kama lugha rasmi kwa ajili ya kutimiza matakwa na madai ya watawala wa nchi hizo. Baadhi ya nchi hizi zimelazimika kutumia sera za lugha za kikoloni kama vile matumizi ya Kiingereza, Kifaransa, Kireno na nyingine kama lugha zao rasmi, kama lugha za kufundishia kutoka madarasa ya kwanza hadi taasisi za elimu ya juu na katika ofisi za umma (Zell, 2018).

Heller (1995, 1999) na Blackledge (2008) wanadai kwamba matumizi ya daima ya lugha za kikoloni huweza kusababisha ufinyu wa mshikamano na umoja miongoni mwa wanajamii (Kandagor 2013b; 2016) na huenda suala hili likaibusha mitafaruku mbalimbali katika jamii. Mfano unatolewa na Christine na Tucker (2003) wanapozungumzia mitafaruku iliyoibuka Afrika Kusini miaka ya 1976 na kuendelea,

miongoni mwa wanafunzi wakigomea matumizi ya lugha za kikoloni kama lugha za kufundishia.

Groff (2016) anabainisha kuwa ufanisi wa sera ya lugha hutokana na mchakato unaofaa wa utekelezaji wake. Mchakato kama hiyo huakisi ukuzaji wa lugha zote hasa lugha zinazofaa kuwa na hadhi sawa. Katika muktadha wa Uganda, Kiswahili kilipewa hadhi kama lugha rasmi ya pili baada ya Kiingereza. Kwa hivyo, juhudi za utekelezaji wa sera ya lugha ya elimu zinafaa zishughulikiwe katika mchakato mzima wa sera ya lugha na upangaji lugha. Ili utekelezaji wa sera ya lugha utimie kikamilifu, ni lazima kuweko na uungaji mkono wa wanasiasa, yaani ukubalifu wa serikali katika shughuli nzima ya uundaji na utekelezaji wa sera ya lugha pamoja na upangaji lugha (Legere, 2002) na Kandagor (2012; 2013a).

Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba tafiti kadhaa zimefanywa zikijihusisha na suala la upangaji lugha pamoja na sera ya lugha. Hizi zimechangia na kutoa msingi wa maarifa na majadiliano katika utafiti huu. Hata hivyo, tafiti hizi hazijaangazia mchango wa sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda na kwa hivyo kuacha pengo la utafiti ambalo utafiti huu umeshughulikia.

2.2 Mwimo wa Nadharia

Nadharia ni mkusanyiko wa makisio na madai fulani ambayo husaidia kuelezea jambo au suala fulani la utafiti (Ogechi, 2021). Mwimo wa nadharia ni kifaa cha madai fulani ambacho mtafiti hukitumia ili kukuza uelewa wake kuhusu suala linalofanyiwa utafiti. Akiwarejelea Mugenda na Mugenda (1999), Ogechi (2021), amedai kuwa taaluma au masuala ya kiutafiti hufanyiwa uchunguzi, data hukusanywa na kusasambuliwa kisha ruwaza fulani huweza kuibuka kutokana na data hizo.

Ruwaza hizo zinajumlishwa pale ambapo madai yanafanywa na kutumiwa kuelezea tafiti kadhaa zinazolingana na utafiti uliozalishwa. Madai hayo ya kijumla ndiyo huitwa nadharia.

2.2.1 Nadharia ya Upangaji Lugha (UL) ya Einer Haugen (1966, 1983)

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya upangaji lugha (UL) iliyoasisiwa na Einar Haugen (1966) na kufanyiwa marekekebisho (1983). Haugen (1966), anadai kwamba upangaji lugha ni mojawapo ya matokeo ya utekelezaji wa uamuzi unaofanywa na wapangaji wa lugha. Nadharia hii hujikita katika dhana ya upangaji lugha kihadhi na upangaji lugha kikongoo.

Haugen (1966), Kloss (1969) na Cooper (1989) wanabainisha kuwa upangaji lugha kihadhi ni juhudi za kimaksudi za kuathiri na kuleta mabadiliko katika majukumu ambayo lugha inatwikwa. Upangaji lugha kikongoo ni kusanyiko la data za semi zilizoandikwa au kunukuliwa ambazo hutumiwa kama kianzio cha ufafanuzi wa kiisimu. Upangaji lugha kikongoo unahusika na muundo wa ndani wa lugha. Mambo yanayozingatiwa hapa ni pamoja na kuunda othografia kwa lugha ambazo bado hazijaandikiwa, kuanzisha mabadiliko katika tahajia, kubuni maneno mapya na kuchapisha vitabu vya sarufi na makamusi. Upangaji wa aina hii unahusu kuendeleza mbinu za kujifunza lugha iliyoteuliwa kupitia mifumo ya elimu. Upangaji kikongoo pia unahusu kupanua ufunzaji na ujifunzaji wa lugha kimaksudi.

Nadharia hii ya UL ya Haugen (1983) imejengwa kwa mihimili minne ambayo ni: uteuzi, ukuzaji msimbo, utekelezaji na upanuzi. Haugen alizichukulia hatua hizi nne kama mihimili muhimu katika ukuzaji wa lugha. Mfano wa UL hutoka wakati ambapo kuna uchaguzi wa lugha kutokana na lahaja yoyote ile ili kuwa lugha ya jumua na hatimaye lugha hiyo inakuwa lugha sanifu.

Kifuatacho ni kielelezo cha nadharia ya UL ya Haugen;

Jedwali 2.1: Nadharia ya UL ya Einer Haugen (1966, 1983)

	Upangaji Sera	Ukuzaji lugha
Jamii (Upangaji lugha kihadhi)	Uteuzi (Mchakato wa uamuzi) a. Utambuzi wa mahitaji b. Uteuzi wa lugha	Utekelezaji (Kupitia elimu) a. Michango na marekebisho b. Tathmini
Lugha (Upangaji lugha kikongoo)	Ukuzaji msimbo (mchakato wa usanifishaji) a. Othografia/uandikaji wa tahajia b. Utungaji wa sarufi c. Utungaji wa kamusi	Upanuzi a. Uboreshaji wa istilahi kulingana na wakati uliopo. b. Ukuzaji mtindo

Asili: Imetafsiriwa kutoka kazi ya Fathi (2017)

2.2.1.1 Uteuzi

Hatua hii hujihusisha na uchaguzi wa lugha na hudhihirika kutokana na matamko rasmi ya serikali. Isitoshe, inahusisha utunzi wa sera ya lugha kirasmi kwa lengo la ukuzaji wa lugha husika. Haugen (1966) anaeleza kwamba uteuzi wa kawaida unahusu uteuzi wa lugha kwa kutunga sheria rasmi inayohusu lugha fulani.

2.2.1.2 Ukuzaji msimbo

Hatua hii hulenga kuimarisha lugha iliyoteuliwa. Ukuzaji msimbo hufuata uteuzi wa lugha. Pia hatua hii hujihusisha na usanifishaji wa lugha. Hapa ndipo taasisi za lugha huunda makamusi, misamiati, mfumo wa uakifishaji na miongozo ya matamshi ya lugha husika. Katika muktadha wa Kiswahili nchini Uganda, hatua hii imekwishafikiwa kwa vile Kiswahili tayari kilisanifishwa na Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki katika mwaka wa 1930 (Hans, 2017; Jjingo, 2018). Aidha kamusi za Kiswahili zimeandaliwa na taasisi mbalimbali pamoja na watunzi au makampuni ya uchapishaji mbalimbali, ziko za kutosha na zinarejelewa.

2.2.1.3 Utekelezaji

Hatua ya utekelezaji inahusu shughuli za taasisi za serikali na za kibinafsi katika uendelezaji wa lugha iliyoteuliwa. Taasisi hizi ni pamoja na zile zinazohusiana na utunzi wa sera na mitaala; ufundishaji wa lugha iliyoteuliwa (lugha sanifu) katika shule na vyo mbalimbali. Elimu huwa nguzo muhimu katika hatua hii kwa ajili ya ukuzaji wa lugha iliyoteuliwa. Utekelezaji pia huhusisha shughuli za wadau na jinsi waandishi walivyoithamini na kuipokea lugha sanifu iliyoteuliwa. Shughuli nyingine kama vile uandishi wa vitabu, magazeti na matumizi ya lugha husika katika vyombo vya habari ni njia mojawapo pia ya utekelezaji wa lugha iliyoteuliwa.

2.2.1.4 Upanuzi

Hatua hii huhusika na upanuzi wa uamilifu wa lugha na uasisi wa ishara mpya mbalimbali hasa za kisayansi na kiteknolojia katika lugha. Shughuli ya kugeuza upya au kufanya lugha kuwa ya kisasa ni mojawapo ya shughuli katika hatua hii ya upanuzi. Katika muktadha wa Uganda, hatua hii ya uendelezaji wa lugha, hasusani Kiswahili, ingepata maana zaidi baada ya hatua ya utekelezaji kutimia.

Utafiti huu uliendeshwa kwa kuongozwa na mhimili wa utekelezaji ili kuchunguza maendeleo ya lugha ya Kiswahili kupitia mfumo wa elimu kama lugha ambayo iliteuliwa na kupewa hadhi nchini Uganda.

Tume ya Kujubi ya mwaka 1989 iliyopitia upya masuala ya elimu nchini, ilipendekeza kuwa lugha ya Kiswahili, ifundishwe kama somo la lazima katika shule zote za msingi na za upili (RoU, 1992). Aidha, kulingana na katiba ya taifa la Uganda ya mwaka 1995, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005, kifungu cha pili katika ibara ya sita, kinasema kwamba; “Kiingereza ni lugha rasmi ya taifa la Uganda, Kiswahili kitakuwa lugha rasmi ya pili ya taifa wakati bunge litakaporidhia kisheria”. Kauli ya

“Kiswahili kitakuwa lugha rasmi ya pili”, ina maana kwamba Kiswahili kilipewa hadhi kutumika katika ofisi za serikali na mikutanoni rasmi, kama vile Kiingereza kinavyotumika. Kwa mujibu wa matamko hayo ya serikali kuhusu Kiswahili, ni bayana kwamba Kiswahili kiliteuliwa na kupewa hadhi. Kwa hivyo, mhimili wa utekelezaji katika nadharia ya UL ya Haugen uliongoza utafiti huu kuchunguza ufaafu wa sheria na matamko haya ya serikali katika kuendeleza Kiswahili nchini Uganda kupitia elimu. Pia mhimili huu ndio ulifaa na kuongoza uchunguzi wa shughuli za taasisi mbalimbali ambazo zinawajibika kuendeleza Kiswahili nchini Uganda, ufundishaji wa Kiswahili shuleni na vyuoni, uandishi wa vitabu vya Kiswahili vya wanafunzi na miongozo ya walimu pamoja na shughuli nyingine zinazolenga ukuzaji wa Kiswahili.

Vilevile, Haugen (1966), anazungumzia mhimili wa utekelezaji kuwa ni shughuli za taasisi mbalimbali za kiserikali au za kibinafsi katika kutekeleza sera kuhusu lugha. Shughuli hizi zinahusu kutumia lugha husika katika shughuli za kijamii, kielimu pamoja na uandishi wa vitabu. Kwa mujibu wa Ricento (2000:3), nadharia hii pia ilihakikiwa na kuendelezwa na Fishman, Ferguson & Das Gupta (1968) na Rubin & Jernudd (1971) wakiangazia upangaji lugha kihadhi kama msingi wa uteuzi wa lugha ya taifa kwa malengo ya maendeleo na ujenzi wa taifa mpya.

Nadharia ya upangaji lugha ya Haugen (1983), ni mduara kwani upangaji lugha kihadhi unaweza kutokana na upangaji lugha kikongoo na vilevile kinyume chake. Hali kadhalika, upangaji lugha kikongoo ukifaulu au ukifeli, utaathiri upangaji lugha kihadhi (Fishman, 1974; Clyne, 1997). Kwa hivyo, katika muktadha wa ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda, nadharia hii ilifaa utafiti huu katika kutathmini juhudi za utekelezaji na changamoto zinazokumba maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda.

2.3 Muhtasari wa Sura

Sura hii imeanza kwa kuwasilisha mapitio ya maandishi yanayojihusisha na suala linalotafitiwa hasa kwa kuangazia upangaji lugha pamoja na sera ya lugha katika elimu. Aidha, sura hii imejadili mwimo wa nadharia uliotumika katika kuendesha utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inajadili mkabala na msuko wa utafiti ulioendeshwa. Aidha, inabainisha eneo, watafitiwa, usampulishaji, vifaa, taratibu, ukusanyaji na uwasilishaji wa data, uchanganuzi wa data na desturi za utafiti.

3.1 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu uliongozwa kwa mkabala wa utafiti usio wa kitakwimu ambao hujihusisha na matukio na mambo yasiyohusiana na vipimo kihisabati (Creswell, 2009). Ogechi (2021) anadai kwamba mkabala huu hutumia njia za kukusanya data zisizo funge wala numerali ambazo hazichanganuliwi kwa njia za kitakwimu. Utafiti wa aina hii huazimia kueleza na kufafanua mahusiano, hali, michakato, mifumo na watu. Mkabala huu uliongoza mtafiti kutambua jinsi mambo yalivyo katika jamii. Kwa hivyo, mtafiti alipata fursa ya kufanyia utatuzi suala lake la utafiti kwa vile mkazo uliwekwa kwa mawazo, majibu na imani za watafitiwa (Hancock, Ockleford, & Windridge, 2009). Katika mkabala huu, mtafiti alijaribu kuelewa tatizo na kuibuka na taswira changamano na pana kwa kutumia maneno, na kuripoti kwa undani mawazo au maoni ya watafitiwa kutokana na utafiti ulioendeshwa katika mazingira asilia ya kila siku.

3.2 Msuko wa Utafiti

Kothari (2004) hudai kuwa msuko ni kiunzi cha dhana ambacho kwacho utafiti huendeshwa kwa kuzingatia jinsi data inavyokusanywa, utathmini na uchanganuzi wa data hiyo. Msuko wa utafiti huelezea taratibu zote za kijumla kuhusu uendeshaji wa utafiti (Creswell, 2009:3).

Msuko wa utafiti wa kifano kimaelezo ndio uliongoza utafiti huu. Sababu za kuteua msuko wa kifano ni kwamba msuko huu husisitiza maelezo ya kina na maelezo huwa na dhima ya kuchangia uelewa wetu wa jamii zetu. Kwa hivyo, mtafiti alijaribu kuchunguza jinsi sera ya lugha imechangia maendeleo ya Kiswahili kupitia elimu pamoja na kuchunguza changamoto ambazo zinatinga maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda. Hili lilitimia kutokana na data zilizokusanywa na kuchanganuliwa kutokana na watafitiwa kumi na watatu kutoka taasisi kumi na tatu. Kama wanavyodai Baxter & Jack (2008), Msuko wa kifano uliziwezesha data zilizokusanywa kuchangiana na kufidiana kwa vile zilikuwa zimekusanywa kutoka kwa watu na taasisi mbalimbali.

3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo data za utafiti zinakusanywa (Kothari (2008). Utafiti huu ulifanyika wilayani Kampala. Kampala ndilo jiji kuu la nchi ya Uganda na hupatikana katikati mwa Uganda. Wilaya ya Kampala ina idadi ya watu takribani milioni 1.35 kati ya jumla ya watu milioni 37 nchini kote (World Population Review, 2019). Lugha ya Kiganda ndiyo lugha ya eneo hilo kwa maana ndiyo lugha inayotumika sana katika shughuli mbalimbali za kila siku. Mbali na Kiingereza kutumika kama lugha rasmi, Kiswahili pia huzungumzwa wilayani na jijini Kampala hasa katika shughuli za kibiashara ingawa kwa kiwango kidogo. Wilayani Kampala kunazungumzwa lugha zaidi ya 45 kutokana na watu wanaotoka kila sehemu ya nchi kwa vile ndilo jiji kuu la Uganda. Miongoni mwa lugha hizi, kuna lugha za Kibantu ambazo huzungumzwa katika sehemu za kusini, magharibi, mashariki na katikati nchini Uganda. Kunazungumzwa pia lugha za Kinailotiki ambazo huzungumzwa na watu kutoka sehemu za kasikazini mwa Uganda (Walusimbi, 1973; King'ei, 2010).

Wilaya ya Kampala inapatikana kwenye vipimo vya latitudo $0^{\circ}19'$ Kasikazini na longitudo $32^{\circ}35'$ Mashariki na kwenye futi 3,900 au mita 1,189 juu ya ufuko wa bahari. Wilaya ya Kampala imo ndani ya mviringo wa Wakiso.

Utafiti huu ulifanyika kimaksudi jijini Kampala kwa sababu wilaya ya Kampala imesheheni ofisi za taasisi mbalimbali za kiserikali pamoja na za kibinafsi zinazohusika na masuala ya uundaji na utekelezaji wa sera mabalimbali hususan sera ya lugha. Hivyo basi, maafisa wanaohusika walihojiwa ili kupata data za msingi kwa ajili ya utafiti huu.

Jijini Kampala pia, kuna wepesi wa upatikanaji wa ofisi za wachapishaji mbalimbali wa vitabu ambao pia wana mchango mkubwa katika kuandaa vifaa vya kufundishia shuleni. Pia kuna urahisi wa upatikanaji wa taasisi mbalimbali nyingine za kielimu zinazotangamanisha watu kutoka sehemu na makabila mbalimbali kote nchini ambao waliweza kuchangia data za kutosha kuendeshea utafiti wetu.

3.4 Utafiti Mwigo

Mtafiti alifanya utafiti mwigo katika shule ya OK. Shule hii ilichaguliwa kwa sababu ya juhudi na sifa za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili zilizofaa utafiti huu. Utafiti mwigo ulifanywa na mtafiti kabla ya utafiti kamili ili kukagua uwezekano, gharama, na makadirio ya muda ambao ungehitajika pamoja na kanuni za kuzingatia. Masuala mengine ambayo yalizingatiwa katika utafiti mwigo kati ya mtafiti na washiriki ni pamoja na kupima uwezo wa kuelewa maswali yaliyosomwa na mtafiti kutokana na ratiba ya mahojiano pamoja na dodoso, maneno yaliyotumika, orodha na urefu wa maswali pamoja na maoni mengine ya washiriki.

Kusudi kuu la utafiti mwigo katika mradi huu wa utafiti ulikuwa ni kutambua maswali yasiyowazi au yenye shida na upungufu katika vifaa vya utafiti pamoja na

utaratibu mzuri wa matumizi ya rekodi ya simu na mikutano ya mtandaoni (*zoom*) kabla ya utekelezaji wa utafiti kamili. Aidha, utafiti mwigo ulimwezesha mtafiti kupima mbinu, mwelekeo, mikakati, na maswali ya uchunguzi huu na kupunguza makosa, uzembe, na kuchanganyikiwa na utaratibu wa mahojiano.

Mahojiano mafupi kwa njia ya simu na mkutano wa mtandaoni yaliendeshwa kwa mshiriki mmoja ili kujaribu na kupima uwazi wa maagizo na maswali kwenye ratiba ya mahojiano. Majibu yalirekodiwa, na mtafiti aliona kuwa ukusanyaji wa data uliendelea vizuri. Hata hivyo, matokeo ya utafiti mwigo yaliunda msimamo thabiti wa njia ya uchambuzi wa data. Aidha, matokeo ya utafiti mwigo yalionyesha kuwa maagizo na maswali ya ratiba ya mahojiano yalikuwa wazi isipokuwa swali moja tu ambalo halikueleweka waziwazi. Hata hivyo, hili lilifanyiwa marekebisha kwa ajili ya kuwa wazi na fupi.

3.5 Watafitiwa

Watafitiwa ni kundi la watu (au vitu) ambao hushirikishwa katika mchakato wa kukusanya data za utafiti (Kombo & Tromp, 2006; Tuckman, 1994; Odiya, 2009). Si lazima watafitiwa wawe watu wote ambao wanaishi katika eneo la utafiti bali humaanisha watu au vitu katika kategoria fulani inayoweza kushiriki katika utoaji na ukusanyaji data za utafiti unaoendeshwa (Denscombe, 2014).

Watafitiwa katika utafiti huu walikuwa ni maafisa au wahusika kutoka: Wizara ya elimu (CC), Vyuo vikuu viwili ambavyo vilikuwa ni MU na KU, hivi vyote ni vyuo vikuu vya serikali na viko katikati mwa jiji la Kampala. Vyuo vikuu hivi hutoa mafunzo ya ualimu wa Kiswahili. Mtafiti pia alitembelea shule ya msingi ya GH ambayo ni shule ya kibinafsi iliyojitolea na kuanzisha mafunzo ya Kiswahili kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la sita licha ya kutotathminiwa na Baraza la

mitihani ya kitaifa. Shule ya upili ya LB, ambayo pia iko katika wilaya ya Kampala, hujishughulisha na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika ngazi zote za sekondari. Aidha, kampuni ya uchapishaji ya FP pia ilitembelewa na afisa wake kuhojiwa. Kampuni hii ya uchapishaji kwa miaka mingi imejishughulisha na uchapishaji wa vifaa vya Kiswahili ambavyo hurejerewa katika ngazi mbalimbali za kielimu nchini Uganda. SP ambayo ni taasisi ya mafunzo ya kiufundi ambako Kiswahili hufunzwa kama somo la lazima kwenye ngazi hiyo, ilitembelewa na data ikakusanywa. UNEB, ambayo wajibu wake ni kutunga mitihani ya kitaifa kwa shule za msingi na sekondari ambamo Kiswahili huwa miongoni mwa mitihani hiyo hasa katika ngazi ya sekondari. Afisa wa masuala ya Kiswahili kutoka NCDC, kituo cha kitaifa cha ukuzaji mtaala nchini Uganda. Taasisi hii ina idara ya Kiswahili na wataalamu wa lugha ya Kiswahili wanaosimamia uundaji na utekelezaji wa mtaala wa Kiswahili. ESC, taasisi inayoshughulikia ajira ya watumishi katika elimu, Chama cha wadau na watetezi wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda (CHAKITAU) pia walihojiwa pamoja na mhusika kutoka chuo cha walimu wa shule za msingi cha GB ambako Kiswahili pia hufunzwa kama somo la lazima. Mwishowe data ilikusanywa kutoka NCHE, taasisi inayoongoza vyuo vya elimu ya juu. Taasisi hizi hujihusisha na ama uundaji wa sera ya lugha ya elimu au utekelezaji wake pamoja na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Waliohojiwa walitakiwa kuonyesha taasisi ambazo walifanyia kazi au / na jukumu lao katika taasisi hizo. Taarifa hiyo ilikuwa muhimu katika kutoa habari muhimu juu ya hali, tajriba na majukumu ya wahojiwa katika utafiti na kuwa na uhakika kwamba wahojiwa watakuwa na taarifa muhimu kwa maswali ya utafiti.

Watafitiwa hawa waliteuliwa kimaksudi kwa msingi wa kupatikana wilayani Kampala kama vile inavyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 3.1: Watafitiwa

Msimbo wa mtahiniwa	Msimbo wa taasisi	Mhusika	Idadi
MT1	CC	Afisa elimu	1
MT2	NCDC	Afisa Kiswahili	1
MT3	UNEB	Afisa Kiswahili	1
MT4	MU	Mkurugenzi	1
MT5	NCHE	Mkurugenzi	1
MT6	ESC	Mkurugenzi	1
MT7	CHAKITAU	Mwenyekiti	1
MT8	KU	Mkuu wa Idara ya Kiswahili	1
MT9	GB	Mdarisi wa Kiswahili	1
MT10	SP	Mdarisi wa Kiswahili	1
MT11	LB	Mwalimu wa Kiswahili	1
MT12	GH	Mwalimu wa Kiswahili	1
MT13	FP	Meneja uchapishaji	1
Jumla			13

Asili: Mtafiti.

3.6 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni sehemu ya idadi nzima ya watafitiwa katika eneo la utafiti fulani (Kothari, 2004). Kwa hivyo, usampuli ni njia au utaratibu wa kuteua washiriki wachache kutokana na kundi la watafitiwa wote (Best na Gall, 1996).

Usampuli wa kimaksudi ulizingatiwa ambapo maafisa kutoka taasisi za serikali pamoja na za binafsi zinazohusiana na masuala ya uundaji na utekelezaji wa sera ya lugha hususan Kiswahili walilengwa kuhojiwa kimaksudi. Maafisa au wahusika 13 kutoka taasisi kumi na tatu waliteuliwa kwa ajili ya kuhojiwa kuhusu suala lililotafitiwa kwa sababu mtafiti aliamini kuwa walikuwa na habari inayofaa kujibu maswali ya utafiti.

Usampuli wa kimaksudi hutumika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa walio na sifa mahsusi kulingana na malengo ya utafiti unaoendeshwa (Anney, 2014). Isitoshe, usampuli wa kimaksudi hutumika kwa kuchagua watafitiwa ambao wana sifa zinazotarajiwa ili kujibu maswali ya utafiti. Aina hii ya usampuli huchangia pakubwa katika upatikanaji wa data kwa vile watafitiwa huchaguliwa kimaksudi kwa msingi wa uwezo wao wa kutoa data zinazotarajiwa (Creswell, 2012:16). Kwa hivyo, aina hii ya usampuli iliongoza utafiti huu kuzalisha data ya kutegemewa katika kuchunguza mchango wa sera ya lugha ya elimu katika kuendeleza Kiswahili nchini Uganda.

3.7 Ukusanyaji wa Data

Creswell (2003) anadai kwamba mkabala wa utafiti usio wa kitakwimu unazo njia mbalimbali zinazoweza kutumika katika ukusanyaji wa data ambazo kwa kiwango kikubwa ni shirikishi. Hii ndiyo sababu watafiti wengi wanaotumia mkabala huu hupendelea kushirikisha watafitiwa kikamilifu katika uzalishaji wa data kuhusu suala linalofanyiwa utafiti. Kwa hivyo, kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti huu, njia ya mahojiano, upekuzi wa nyaraka maktabani na uchambuzi wa data za kiyaliyomo zilitumika katika uzalishaji wa data za utafiti huu kama inavyoelezwa katika sehemu zilifuatazo.

3.7.1 Mahojiano

Data zilikusanywa kwa mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa. Mahojiano ni njia ya ukusanyaji data ambapo watu wawili au zaidi hushiriki katika kuulizana na kujibizana kwa ajili ya kupata ujuzi juu ya tajriba, maoni, imani, mila, ujuzi, maono na fikra zao kuhusu kadhia lengwa na mtafiti huitumia fursa hiyo kuelewa muktadha na mitazamo ya washiriki kuhusu suala linalofanyiwa utafiti (Schostak, 2005). Lugha za Kiingereza na Kiswahili zilitumika katika mahojiano kwa ajili ya mawasiliano kamilifu kati ya mtafiti na mhojiwa. Mkakati huu uliwezesha utafiti huu kuzalisha data za msingi za

kutegemewa. Mahojiano yalimwezesha mtafitiwa kujieleza kwa utondoti kifikra na kimaoni kuhusu suala la utafiti. Baadhi ya mahojiano yalikuwa ya ana kwa ana na mengine yalikuwa kwa njia ya mikutano ya mtandaoni (*zoom*). Mahojiano mengine yaliendeshwa kwenye simu na kupitia dodoso isiyo funge kwa njia ya baruapepe kwa sababu ya janga la ugonjwa wa virusi vya korona lililokuwa limegubika dunia nzima wakati huo. Watafitiwa walihojiwa kwa ajili ya kuzalisha data za msingi kuhusu msimamo wa sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia elimu nchini Uganda. Aidha, data zilizalishwa kuhusu changamoto zilizokumba ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda pamoja na suluhu za changamoto hizo. Katika mahojiano, mtafiti aliweza kuuliza au kuomba ufafanuzi zaidi kuhusu majibu yaliyotolewa na mtafitiwa. Pia mtafitiwa aliombwa kufuata utaratibu wa kujibu maswali kulingana na jinsi alivyoongozwa na mtafiti. Njia ya mahojiano ilimpa fursa mtafiti kupata mwanga zaidi kuhusu jibu lililotolewa na mtafitiwa kwa ajili ya kuepukana na makosa yoyote au taarifa isiyo kamili au isiyo ya kweli. Waliohojiwa walikuwa mkurugenzi wa elimu. Maswali ya msingi kwa mtafitiwa huyu yalikuwa juu ya msimamo wa sera ya lugha na athari yake katika ukuzaji wa Kiswahili. Aidha, mahojiano kuhusu juhudi za serikali kupitia wizara ya elimu na michezo katika harakati za ukuzaji wa Kiswahili kupitia sekta ya elimu pia yaliendeshwa. Mahojiano haya yalimpa mtafiti habari kuhusu matamko mbalimbali ya sera ya lugha kuhusu Kiswahili pamoja na juhudi zilizokuwa zimewekwa na kupendekezwa kuendeleza Kiswahili kupitia mfumo wa elimu. Kisha mtafiti aliendesha mahojiano na wadau mbalimbali kwa usawa na kukusanya maoni anuwai.

Mtafiti alihoji pia wataalamu wa Kiswahili katika Kituo cha Kitaifa cha Ukuzaji Mitaala kupata uelewa wa kina na uzoefu wao wa uundaji wa sera na ukuzaji wa mtaala wa lugha ya Kiswahili. Mahojiano na wataalam wa mtaala yalilenga athari ya

sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia elimu, masuala ya mtaala wa Kiswahili na rasilimali za kusaidia katika utekelezaji wa mtaala huo pamoja na changamoto zilizokumba utekelezaji wa mtaala wa Kiswahili. Kwa ujumla, mtafiti aligundua kuwa habari iliyopatikana kutoka kwa mkurugenzi wa elimu ilikuwa sawa na ile ya wataalam wa Kiswahili. Hili lilimsaidia kujiamini katika uhalali wa matokeo yake ya utafiti.

Mahojiano na walimu na wahadhiri wa lugha ya Kiswahili katika ngazi ya vyuo vikuu, vyuo vya walimu, vyuo vya kiufundi, sekondari na shule za msingi yalifanywa baadaye pia. Maswali katika mahojiano na walimu yalilenga stadi za lugha zilizosisitizwa katika ufundishaji, ajira kwa walimu wa Kiswahili, athari ya sera ya lugha ya shule katika ukuzaji wa Kiswahili, muda uliopewa mafunzo ya Kiswahili kulingana na ratiba pamoja na vifaa vya kurejelea na vizuizi vyovyote vilivyoathiri ukuzaji wa Kiswahili.

Mwishowe, mahojiano yalifanyika kwa wachapishaji na wanaharakati wa Kiswahili ambao pia wako kwenye usukani wa kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Hawa walipewa jukumu la kufunua habari muhimu juu ya hadhi ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili na changamoto ambazo maendeleo ya Kiswahili hukabili hasa kupitia sekta ya elimu.

Mtafiti alianza kila mahojiano kwa kutaja mada ya utafiti na madhumuni ya utafiti. Baada ya hapo, fomu za idhini zilisomwa kwa washiriki na idhini ilitolewa kwa maneno. Mtafiti alijaribu iwezekanavyo kujenga uhusiano na washiriki na mwishoni mwa mahojiano alihisi kwamba habari muhimu ilipatikana. Mtafiti alichagua mahojiano kwa ajili ya kuchangia na kufidia data iliyotokana na uchambuzi au upekuzi wa hati mbalimbali pamoja na dodoso isiyo funge. Hata ingawa uchambuzi

wa hati mbalimbali ulitoa ufahamu mzuri juu ya matamko ya sera, mtafiti alihitaji kusikia kutoka kwa washiriki kwani mahojiano yalitoa nafasi ya kutafuta habari za kina.

3.7.2 Utafiti wa maktabani

Njia nyingine iliyotumika kuzalisha data katika utafiti huu ni upekuzi wa nyaraka za maktabani. Nyaraka mbalimbali zilizohifadhiwa maktabani au mtandaoni zinazohusiana na suala la utafiti zilitathminiwa. Mtafiti alitathmini na kufasiri data maktabani kwa makini. Hii ni kwa sababu anavyodai Altheide (2000) kwamba ushirikisho wa njia ya upekuzi wa nyaraka za maktabani pamoja na njia nyingine za utafiti usio wa kitakwimu, humwezesha mtafiti kudadavua kwa utondoti na kupata maarifa kuhusu suala linalofanyiwa utafiti. Kwa hivyo, njia hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza na kupata maarifa kuhusu sera ya lugha pamoja na nyaraka nyingine zilizo na uhusiano na suala la utafiti. Owen (2014) anadai kwamba, nyaraka zinazoweza kufanyiwa uchunguzi katika njia hii ni kama vile matangazo, mipango mikakati, orodha za mahudhurio, kumbukumbu za mikutano, miongozo ya mafunzo, ikisiri za kazi za mawasilisho, kazi za tafiti, vitabu na vipeperushi, shajara na majarida, ratiba za matukio mbalimbali, barua na taarifa zilizoandikwa, ramani na chati kuhusu taarifa zenye uhusiano na suala linalofanyiwa utafiti, magazeti, ilani na matoleo mbalimbali, mapendekezo ya miradi, fomu za maombi na mihtasari ya taarifa muhimu, maandishi ya vipindi vya redio na televisheni, ripoti za data za makampuni au taasisi, na nyaraka za serikali, miongoni mwa nyaraka nyingine.

Nyaraka za serikali zinazohusika na sera ya lugha kama vile katiba, mitaala, ripoti za tume mbalimbali, maamuzi ya mahakama, kielelezo cha sera, matamko ya wanasiasa, na sheria za bunge zilitathminiwa. Pia, makala ya magazeti kuhusu suala la utafiti yalipekuliwa na kuchanganuliwa. Haya yalikuwa ni makala yaliyo na uhusiano au

yanayozungumzia sera ya lugha na shughuli za kuendeleza Kiswahili kupitia mfumo wa elimu au yale yanayozungumzia ukuzaji wa Kiswahili kwa ujumla.

3.7.3 Uchambuzi wa data za kiyaliyomo

Aina nyingine ya ukusanyaji wa data ilikuwa uchambuzi wa data za kiyaliyomo. Mtafiti alikusanya hati rasmi na zisizo rasmi, ambazo zilikuwa muhimu na zilizopatikana kwa ajili ya kuendeshea utafiti huu. Mtafiti alinukuu maoni na mahitimisho yaliyoweza kusimbwa kutokana na ufasiri wa hati mbalimbali za sera ambazo zilikuwa zinafaa kwa ajili ya kujibu maswali ya utafiti. Nyaraka rasmi zilikuwa nyaraka ambazo zilikusanywa na kuchambuliwa na shirika kwa madhumuni maalumu na zilirasimishwa na shirika kupitia muhuri wa shirika hilo; kwa mfano, ratiba za shule, ripoti mpya ya mwaka wa masomo, ripoti za kila mwaka za kitaaluma na kanuni za shule. Taarifa na takwimu kutoka kwenye wavuti wa Wizara ya Elimu na michezo, NCDC, UNEB, ESC, NCHE, magazeti miongoni mwa nyaraka zingine, yalimpa mtafiti habari muhimu ya msingi juu ya mfumo wa elimu, mtaala, hali ya shule, na pia hati tofauti za sera. Kutokana na njia hii, mtafiti aliweza pia kupata habari kuhusu matamko ya sera kuhusu maendeleo ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu.

Mwishowe, nyaraka kama mtaala unaozingatia umilisi kwa ngazi ya chini ya sekondari, hati za sera: Katiba ya Uganda, ripoti ya Kajubi, hati maalumu ya serikali ya 1992, (*Government White Paper*), nakala za magazeti kati ya zingine zilichanganuliwa ili kubaini msimamo wa sera ya lugha katika ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia sekta ya elimu.

3.8 Vifaa vya Kukusanya Data

Ratiba ya mahojiano ilitumika katika mchakato wa ukusanyaji data kupitia njia ya mahojiano. Katika kielekezi hiki cha ratiba ya mahojiano, mtafiti aliandaa maswali ambayo yalikusiana na madhumuni ya utafiti. Mtafiti alitumia maswali yale kama mwongozo tu, kwa sababu alikuwa na uhuru wa kuuliza maswali ya ziada kulingana na jibu lililotolewa au vile hali ilivyokuwa.

Kwa mshiriki mmoja (MT1) ambaye muda haukutosha wa mahojiano kupitia njia ya mkutano wa mtandaoni (*zoom*), dodoso isiyo funge iliambatishwa kwenye baruapepe yake ambayo alijaza na data hiyo ilifidia na kuchangia data iliyotokana na mkutano kati yake na mtafitiwa mtandaoni.

Katika ukusanyaji wa data za maktabani na uchambuzi wa data za kiyaliyomo, mtafiti alitumia kielekezi cha tathmini za nyaraka. Hiki kilitumika kumwongoza mtafiti kutafuta na kuchambulia hati au nyaraka zilizokuwa zinafaa kutoa data kulingana na maswali ya utafiti. Mtafiti pia alitumia kalamu na karatasi ili kurekodi dondoo zozote zilizopatikana katika njia za ukusanyaji data.

Mtafiti pia alirekodi mahojiano kwa kutumia simu ya rununu. Kwa sababu ya ugonjwa wa virusi vya korona, asilimia kubwa ya mahojiano yalikuwa kupitia simu, na sauti za mahojiano zilirekodiwa. Kwa hivyo mtafiti aliunda hifadhidata kwenye kompyuta na rekodi zote ziliwekwa hapo. Rekodi hizo zilichukua dakika 25-35 baada ya mtafiti kufikia kiwango cha kuridhika na data kulingana na jinsi alivyoongozwa na ratiba ya mahojiano. Kabla ya rekodi za simu, mtafiti aliwaongoza washiriki kupitia njia ya utafiti na mahojiano, akielezea kuwa chochote ambacho wangepanya kingebaki kuwa siri. Mtafiti aliwaarifu washiriki kwamba wangeweza kuchagua ikiwa watashiriki au kutoshiriki katika rekodi za mahojiano au kuwa huru kuacha mahojiano

wakati wowote. Aliwahakikishia pia kuwa chochote ambacho kingerekodiwa, majibu yao yasingejulikana na hakuna majina ambayo yangetajwa katika ripoti ya rekodi hiyo.

Washiriki waliulizwa ikiwa wangejipendekezea majina bandia wakati wa rekodi za sauti na mahojiano ili kuhakikisha kutokujulikana wakati wote. Hata hivyo, hakuna aliyependekeza. Mtafiti aliachiwa uhuru wa kubuni majina bandia ya chaguo lake. Katika mchakato wa kurekodi data za mahojiano kwa kutumia kinasa sauti cha simu, mtafiti pia alitumia daftari kuandikia dondoo kadhaa. Umuhimu wa njia hii ya kurekodi ni kwamba huondoa hali ya upotoshaji au kushuku kwamba data zilizopatikana siyo za kweli (Opie, 2004:123) Aidha, kielekezi cha tathmini za nyaraka kilitumika kuhakikisha data inayohusika na suala la utafiti (Kiambatisho v)

3.9 Taratibu za Ukusanyaji Data

Mchakato mzima wa ukusanyaji wa data ulianza na kuomba idhini ya kufanya utafiti kutoka idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret – Kenya. Njia za uzalishaji data za mkabala wa utafiti usio wa kitakwimu ndizo zilitumika katika utafiti huu. Kwa hivyo, mtafiti alipitia na kujizoesha na njia za mahojiano pamoja na upekuzi wa nyaraka za maktabani ili apate kuzama kwa undani katika matumizi ya njia hizi na kutambua wajibu wake kama mtafiti. Mtafiti alifanya utafiti mwigo katika shule ya OK. Shule hii ilichaguliwa kwa sababu ya juhudi na sifa za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili zilizofaa utafiti huu. Watafitiwa kamili hawakutumika katika utafiti mwigo kwa ajili ya majibu yao kuwa ya kutegemewa katika utafiti kamili (Kinchin na Edwards, 2018; Ogechi, 2021). Kwa washiriki watarajiwa wa mahojiano, mtafiti aliwasiliana nao kibinafsi kwa njia ya simu na kupanga miadi ya kufanya nao mahojiano katika wakati wao kupitia kwa simu. Kisha

mtafiti alifanyia mahojiano hayo katika mahali penye utulivu bila kelele wala usumbufu wowote.

Kabla ya kushirikishwa katika mahojiano ya utafiti huu, mtafiti aliwasomea washiriki lengo la utafiti huu na kuwapa nafasi ya kuuliza swali lolote juu ya chochote ambacho wangeweza kuwa hawajaelewa. Mtafiti alijibu swali lolote lililoulizwa kutoka kwa washiriki. Aidha, mtafiti aliomba idhini ya kurekodi mahojiano mwanzoni. Baada ya kujibu maswali yote, alimaliza mahojiano na kuwashukuru washiriki kwa ushiriki wao. Baada ya kunasa mahojiano, alichambua data. Baada ya kumaliza utafiti huu na kuidhinishwa, mtafiti atatuma ripoti ya muhtasari wa matokeo kwa washiriki. Atahakikisha kuwa anahifadhi nakala katika sehemu iliyo salama na katika kompyuta yake inayolindwa na nywila katika ofisi yake ya kibinafsi ya nyumbani.

3.10 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Uchanganuzi wa data ni kuzitathmini data zilizopangwa katika ruwaza mbalimbali ili kufanya maamuzi na mahitimisho. Ni kitendo cha kuthibitisha na kupanga vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo husaidia kujibu maswali ya utafiti (Taylor & Bogdan, 1984). Kwa mujibu wa Gay (2012:465), uchanganuzi wa data katika mkabala usio wa kitakwimu hujihusisha na utoaji wa data za nyanjani katika namna inayofaa na kukubalika kwa ajili ya uwasilishaji wa matokeo ya utafiti isiyotiliwa shaka na wasiwasi. Uchanganuzi wa data katika mkabala usio wa kitakwimu huwa ni shughuli endelevu kutoka mwanzo hadi mwisho wa mchakato mzima wa utafiti (Lodico, 2010:180). Kwa hivyo, dondoo na rekodi zote kutoka nyanjani, zilitathminiwa na kuwekwa katika misimbo iliyo wazi. Creswell (2007) anadai kwamba uchanganuzi wa data katika utafiti usio wa kitakwimu huhusisha uandikaji na ufasiri wa data kutokana na kumbukumbu za uwanjani, yaani dondoo, nukuu, picha au rekodi ili zipate kuchanganuliwa kwa kupunguzwa na kupangwa kidhamira

au kimaudhui kupitia mchakato wa usimbaji kwa kuzisimba kimpango na mwishowe kuziwasilisha kimasimulizi na kimaandishi. Kwa hivyo, data kutoka uwanjani zilipangwa kimaudhui ili zipate kufasiriwa na kutathminiwa kulingana na malengo pamoja na maswali ya utafiti.

Data zilipangwa kimaudhui huku zikihusishwa na sera ya lugha na vile imechangia ufanisi au kufeli kwa ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda. Hata hivyo, data zilizozalishwa kutoka nyanjani zilichanganuliwa kwa hatua tano za uchanganuzi wa data za kimaudhui kwa mujibu wa Braun & Clark (2006) kwa kuongozwa na nadharia ya upangaji lugha ya Haugen.

Unukuzi wa data zilizorekodiwa kutokana na njia ya mahojiano ulifanywa kwa maneno halisi waliyoyatumia wahojiwa hasa yalivyosemwa kutokana na kinasasauti. Mtafiti alinukuu dondoo za rekodi za data huku akisisitiza vipengele vinavyohusu suala la utafiti. Alipendekeza vifungu vinavyojumuisha dhana zinazohusiana, aliunda misimbo, akatathmini na kueleza data kimaudhui. Usiri wa watafitiwa pia ulizingatiwa katika nukuu kwa kusimba majina yao au kwa kuwapa majina bandia.



Kielelezo 1.1: Mfumo wa hatua sita za uchanganuzi wa data za kimaudhui wa Braun & Clarke (Braun & Clarke, 2006)

3.11 Uhakikisho wa Uaminifu katika Utafiti

Utegemezi na uaminifu hudhirisha ukweli wa matokeo yanayowasilishwa kuwa ni ya ukweli na mahitimisho kuwa ni yenye mashiko na ya kutegemewa (Anney, 2014). Guba & Lincoln (1994) wamedai kwamba utegemezi na uaminifu katika kazi ya utafiti ni muhimu sana kwa ajili ya kupima ufaafu wa kazi ya utafiti husika. Uhakikisho wa uaminifu katika utafiti huu unajadiliwa katika vipengele vifuatavyo; ukweli, uhawilishi, utegemezi, na uhakika.

3.11.1 Ukweli

Ukweli ni imani mtafiti au msomi aliyonayo katika matokeo ya utafiti (Anney, 2014), (Gubana Lincoln, 1994). Ili kuhakikisha ukweli, mtafiti alitumia maswali ya ziada wakati wa mahojiano kwa ajili ya kupata ufafanuzi zaidi na ufasiri kamili wa majibu kutoka kwa mtafitiwa ili kuepukana na taarifa zisizo za ukweli.

3.11.2 Uhawilishi

Kipengele hiki hurejelea kiwango cha matokeo ya utafiti kukubalika katika miktadha mbalimbali ya watafiti wengine (Anney, 2014). Kuhakikisha uhawilishaji wa matokeo ya utafiti huu, mtafiti alieleza kwa undani kila kipengele ili kuonyesha jinsi matokeo ya utafiti huu yanavyoweza kutumika au kurejelewa katika miktadha mingine au hali mbalimbali. Suala hili pia litawapa wasomaji wa utafiti huu kuihukumu kazi yenyewe kwa ajili ya kuchunguza iwapo itaweza kurejelewa katika miktadha au hali zao.

3.11.3 Utegemeaji

Utegemeaji hurejelea kiwango cha jinsi matokeo ya utafiti husika yanavyoweza kutobadilika iwapo utafiti uohuo ungefanywa tena na watafiti wengine tofauti (Anney, 2014). Ili kuhakikisha utegemeaji katika utafiti huu, mchakato wa utafiti

mzima ulibainishwa wazi ili kutoa fursa kwa watafiti wa wakati ujao kurudufu kazi ya utafiti huu iwapo watakusudia kupata matokeo yaleyale.

3.11.4 Uhakika

Kipengele hiki kinahusika na uthibitishaji wa kwamba data iliyokusanywa na ufasiri wa matokeo si ghushi (Anney, 2014). Huzingatia suala nyeti kwamba, matokeo yanafaa yawakilishe na kuwasilisha kinachofanyiwa utafiti na isiwe imani, mielekeo, au upendeleo wa mtafiti (Morrow, 2005). Kama inavyopendekezwa na Gubana Lincoln (1994), uhakika wa utafiti huu ulizingatiwa kupitia uhifadhi na urejeleaji wa dondoo za nyanjani, uhifadhi wa rekodi za kumbukumbu za nyanjani; kutokana na nyaraka za maktabani na mahojiano pamoja na uhifadhi wa rekodi za data iliyochanganuliwa.

Shughuli hii itamsaidia yeyote kufuata kila hatua iliyochukuliwa katika mchakato mzima wa utafiti. Shajara iliyotumika kuandikia matukio ya kila siku nyanjani wakati wa ukusanyaji data ulikuwa ukiendeshwa, ilihifadhiwa.

3.12 Maadili katika Utafiti

Maadili ni suala muhimu sana la kuzingatia ili kufanikiwa kwa utafiti wowote ule. Kwa mfano, hatua ya kwanza ya mchakato wa utafiti huu ilikuwa ni kuomba idhini ya kufanya utafiti kutoka idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi Eldoret – Kenya. Aidha, mtafiti alikuwa na barua kutoka idarani ya kumtambulisha kwa watafitiwa, na watafitiwa walielezwa kuhusu suala la utafiti pamoja na malengo ya utafiti kabla ya shughuli yoyote ya ukusanyaji data (*KIAMBATISHO CHA KIBALI VI & VII*). Aidha, mtafiti aliomba idhini ya kuendesha utafiti jijini Kampala kutoka kwa ofisi ya Kurugenzi ya Elimu na Huduma za Kijamii ya Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji Kuu la Kampala (KCCA) ambako alielekezwa

kuomba na kupewa kibali cha utafiti kutoka kwa Kurugenzi ya Utawala na Rasilimali watu (*KIAMBATISHO CHA KIBALI VIII*). Mtafiti pia aliomba idhini ya kukubaliwa na taasisi pamoja na watafitiwa kabla ya zoezi la ukusanyaji data halijaanza (*KIAMBATISHO I, II, III na IV*). Mtafiti aliwahakikishia watafitiwa kuwa data au maoni yao yatatumika katika uwanja wa kiakademia tu. Baada ya makubaliano kati ya mtafiti na mtafitiwa, mahojiano yangeanzishwa kwa njia ya mazungumzo ya simu au kwa njia ya *zoom*. Mtafiti alihakikisha usiri na ufaragha wa watafitiwa wake katika mchakato wa ukusanyaji data hasa katika mahojiano kwa kuwapa wahojiwa wake majina bandia na misimbo ili kutotambulikana.

3.13 Muhtasari wa Sura

Sura hii imeanza kwa kuelezea utafiti usio wa kitakwimu kama mkabala ulioongoza utafiti huu, imejadili msuko wa utafiti kama msuko wa kifano kwa maelezo. Sura hii pia imejadili aina ya sampuli iliyotumiwa ambayo ilishirikisha watafitiwa kumi na watatu kutoka taasisi kumi na tatu, taratibu za ukusanyaji data, mchakato wa uchanganuzi wa data, uhakikisho wa uaminifu pamoja na jinsi vipengele vya maadili katika utafiti vilivyotekelezwa.

SURA YA NNE

NAFASI YA SERA YA LUGHA KATIKA UKUZAJI WA KISWAHILI

NCHINI UGANDA KUPITIA MFUMO WA ELIMU

4.0 Utangulizi

Katika sura hii, maudhui kutokana na mahojiano pamoja na nyaraka zilizopekuliwa yalichanganuliwa na kuwasilishwa kwa mujibu wa lengo la kwanza.

Lengo la kwanza la utafiti huu lililenga kujadili nafasi ya sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda. Data kuhusiana na lengo hili zilitokana na upekuzi pamoja na uchambuzi wa nyaraka mbalimbali zenye matamko ya sera kuhusu uendelezaji wa Kiswahili nchini Uganda. Nyaraka kama vile, mtaala unaozingatia umilisi kwa kiwango cha chini cha sekondari, hati za sera; katiba ya Jamhuri ya nchi ya Uganda, hati ya serikali ya sera ya elimu ya 1992, mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nakala za magazeti na nyaraka zingine zilichambuliwa ili kubaini msimamo wa sera ya lugha katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu.

Ili kufikia lengo hili, sehemu hii inawasilisha matamko ya sera (tume, mikataba, katiba, nyaraka za sera kati ya zingine) ambayo yameathiri maendeleo ya Lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Aidha, maoni ya washiriki yanaonyeshwa kuhusu hadhi ya sera ya lugha kuhusu Kiswahili katika sekta ya elimu nchini Uganda. Mtafiti alitumia nambari na misimbo badala ya majina ya washiriki na shule ili kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya kimaadili kama usiri, faragha, na kutokujulikana. Katika sura hii, mtafiti anawasilisha na kujadili matokeo ya swali la kwanza la: Sera ya lugha ina msimamo upi kuhusu maendeleo ya Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda? Yafuatayo ni maudhui yaliyojitokeza kutokana na data kuhusu nafasi ya sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu.

4.1 Matamko ya Sera ya Lugha Kuhusu Ukuzaji wa Kiswahili

4.1.1 Tume za serikali tangu uhuru

Changamoto za sera ya lugha nchini Uganda zimekuwepo kwa muda mrefu na suluhisho kwa hili bado linaonekana kuwa tata. Kwa miaka mingi, kumekuwa na matamko kadhaa, amri, tume, marekebisho na mikataba inayohusiana na ukuaji pamoja na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda na hasa katika sekta ya elimu. Tangu uhuru, kumekuwa na tume ambazo ziliundwa kuchunguza hali ya elimu nchini Uganda na kupendekeza jinsi mfumo wa elimu na mafunzo lazima yachangie maendeleo ya raia na jamii zao. Katika sehemu hii, mtafiti alichambua nyaraka za tume zinazotamka matumizi ya Kiswahili katika sekta ya elimu.

Itakumbukwa na kujadiliwa kwamba hata wakati ambapo makao makuu ya kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki yalipokuwa katika Chuo Kikuu cha Makerere-Kampala Uganda, 1950 - 1960, hali ya lugha ya Kiswahili nchini Uganda haikubadilika. Vilevile, baada ya uhuru, hali ya Kiswahili nchini Uganda ilibaki ileile. Nchi ya Uganda ilipata sera ya lugha katika elimu mnamo 1965 kutokana na ripoti ya tume ya Castle (1963) ambayo ilitoa mapendekezo kadhaa (Castle, 1963). Kwanza, lugha sita za Uganda zilipaswa kutumiwa kufundishia katika shule za msingi: Luganda, Akarimojong, Ateso, Lugbara, Luo, (Runyoro / Rutooro na Runyankole / Rukiga). Pili, watoto walipaswa kufundishwa kwa lugha yao katika miaka ya mapema ya shule. Tatu, Kiingereza kilitakiwa kufundishwa katika darasa la kwanza na kuendelea kama somo kwa miaka yote saba ya shule ya msingi. Masomo matano ya msingi ya Hisabati pamoja na Haiba na Michezo yalifundishwa kupitia lugha ya Kiingereza. Halafu Kiingereza kama lugha ya kufundishia ingeongezwa kwa Sayansi, Jiografia, Sanaa, Ufundi na Muziki katika mwaka wa tano. Katika darasa la sita na saba, masomo yote yangefundishwa kwa Kiingereza. Pamoja na ripoti ya Castle,

hakuna tamko lililotolewa au ufafanuzi wowote juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili licha ya kuwepo kwa lugha hiyo wakati huo.

Tume nyingine ya Kajubi (1987) ilituuliwa na Waziri wa Elimu ili kupitia Sera ya Elimu wa wakati huo mnamo Julai 1987. Majukumu yake yalikuwa: (i) Kupendekeza sera katika ngazi zote za elimu yaani msingi, sekondari na vyuo vikuu, (ii) Kupendekeza sera kuhusu malengo ya elimu, (iii) Kupendekeza sera kuhusu muundo wa mfumo wa elimu, na (iv) Kubainisha jukumu la sekta binafsi katika elimu (Muzoora, Terry, & Asiimwe, 2014).

Tume ilipendekeza utambuzi na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili shuleni nchini Uganda (Kajubi, 1989) kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi. Hata hivyo, Kiswahili kilibaki kufundishwa kama somo katika shule chache tu hasa katika maeneo ya wingi lugha (Ssekamwa, 2000).

Mnamo 1992, serikali ilitua kamati iliyotokana na hati maalumu (*White Paper*) ya kuchunguza na kubaini mapendekezo ambayo yangekubalika na yaliyowezekana kutekelezwa au kufanyiwa marekebisho kutokana na ripoti ya Kajubi. *White Paper* ilikubali kwa kiasi kikubwa mapendekezo ya Tume ya Kajubi na kupendekeza mabadiliko machache. Aidha, ilikipendekeza Kiswahili kama somo la lazima katika shule za msingi na sekondari.

Kuhusu mikakati ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotajwa, ilitakiwa kuanzisha ufundishaji wa Kiswahili katika mipango ya elimu ya watu wazima na katika vyuo vya kijamii vya kiufundi. Hali hii ilikuwa ni kuhakikisha kwamba ukuaji na ukuzaji wa Kiswahili unakubaliwa takribani katika mfumo mzima wa elimu kwa lengo la kuondoa tofauti za lugha kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla. Hata hivyo, *White*

Paper ya 1992 imebaki kuwa hati kuu ya Sera ya elimu katika sekta ya elimu hadi leo nchini Uganda.

4.1.2 Sheria ya Kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni muundo mwingine wa sera ambao unaongoza ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulisainiwa tarehe 30 Novemba, 1999 na ulianza kutekelezwa tarehe 7 Julai 2000 kufuatia kuridhiwa kwake na nchi tatu washirika - Kenya, Uganda na Tanzania. Katika ibara ya 137 ya lugha rasmi ya Jumuiya na kifungu 119 cha utamaduni na michezo, ilikubaliwa kati ya wanachama kwamba Kiswahili kitakuwa lugha ya Jumuiya ya Afrika mashariki. Aidha, Mataifa washirika yatakuza ushirikiano wa karibu kati yao kwa kuzingatia ukuaji na ukuzaji wa lugha za asili hasa Kiswahili kama lugha ya mawasiliano kikanda. Suala hili lilitoa msingi na nafasi ya kukuza Kiswahili bila kuvutia chuki kutoka maeneo ambayo kihistoria yalipinga Kiswahili (Chebet-Choge, 2012: 196).

Aidha, mkutano wa 35 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika kuanzia tarehe 30 Machi hadi 4 Aprili 2017 katika Makao Makuu ya Jumuiya jijini Arusha Tanzania, ulipitisha azimio muhimu la Bunge la Afrika Mashariki (EALA) kukuza matumizi ya Kiswahili na kuipitisha kama lugha rasmi ya Jumuiya. Baraza lilizingatia marekebisho ya ibara ya 137 ya Mkataba wa Jumuiya (EAC) kujumuisha Kiswahili kama mojawapo ya lugha rasmi za Jumuiya. Liliamuru nchi washirika kuunda Sera za Kitaifa za Lugha ya Kiswahili na kukuza utumiaji wa Kiswahili katika maeneo rasmi na kuanzishwa kwa Mabaraza ya Kiswahili ya Kitaifa na Vyama vya Kiswahili vya Kitaifa. Kwa hivyo, kukubalika kwa Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano na rasmi kikanda, ni hatua muhimu ya kuwaunganisha watu katika Jumuiya. Hali hii itazipa sekta za elimu Afrika Mashariki, hasa Uganda

kukubali kupitishwa kwa lugha ya Kiswahili kama somo la lazima katika taasisi za elimu, jambo ambalo litachangia pakubwa ukuaji na ukuzaji wa Kiswahili.

4.1.3 Katiba ya Uganda

Katiba ya Uganda ndiyo hati kuu ya sera inayoelezea hadhi ya lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Mnamo Septemba 2005, bunge la Uganda lilifanyia marekebisho kifungu 6 (2) na kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya pili baada ya Kiingereza.

Kwa mujibu wa katiba ya Uganda ya 1995 iliyofanyiwa marekebisho mnamo 2005 kifungu cha 6(2) kinatamka kwamba: “Kiswahili kitakuwa lugha ya pili rasmi nchini Uganda na kutumika katika hali husika vile sheria itakavyoamriwa na bunge”. Kulingana na kifungu hiki, lugha nyingine yoyote inaweza kutumika kama njia ya kufundishia shuleni au taasisi zingine za elimu au kwa sababu za kisheria, kiutawala au kimahakama bunge litakaporidhia (CoU, 2005).

Aidha, hili lilifuatiwa na kuzinduliwa kwa Sera ya Kitaifa ya Utamaduni ya Uganda (UNCP) mnamo 2006 na Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Jamii. Sera ya Kitaifa ya Utamaduni inatoa nafasi ya msingi wa kuanzishwa kwa sera ya kina ya lugha inayoweza kutilia maanani ufundishaji na ujifunzaji wa lugha (hasa Kiswahili) ambazo zipo katika vikundi mbalimbali vya lugha nyingi za Uganda (Jjinga, 2021).

Kwa hivyo, nyaraka hizi mbili zinaonyesha mwinuko wa hadhi ya Kiswahili nchini Uganda, hali ambayo ingeongoza sekta ya elimu kuchukua hatua katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika taasisi mbalimbali. Hata hivyo, tangu matamko hayo yatolewe, Kiswahili kama lugha imekuwa ikikabiliwa na vizuizi miongoni mwa raia wa Uganda na hadi sasa, ukuzaji wa Kiswahili bado ni changamoto kwa serikali (Nsookwa, 2014). Mikutadha ambamo Kiswahili kinafaa kutumika haijaainishwa,

hakuna magazeti ya Kiswahili, mikutano ya kisiasa inaendeshwa ama kwa Kiingereza au kwa lugha zingine za asili na sio katika Kiswahili.

Aidha, ikumbukwe kwamba, mnamo 2019, Baraza la Mawaziri la Uganda lilipitisha kanuni za kuanzishwa kwa Baraza la Kiswahili la Kitaifa kutimiza wajibu wa serikali kama Nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na kutekeleza kifungu cha 6 (2) cha Katiba ya Uganda. Hata ingawa hili halijatekelezwa kikamilifu, hali hii inatoa msingi na nafasi ya Kiswahili kuendelezwa katika sekta ya elimu nchini Uganda.

4.1.4 Mitaala ya elimu

Kiswahili kilianza kufundishwa na kutahiniwa nchini Uganda kabla ya uhuru ingawa bila mtaala wa kufundishia. Kwa kuzingatia hali hii, Serikali ya Uganda ilianza kuweka mikakati madhubuti ya ukuzaji na ufundishaji wa Kiswahili ili kuiweka nchi kwa kiwango sawa na Mataifa mengine washirika wa Afrika Mashariki.

Mnamo mwaka wa 2008, mtaala rasmi wa kwanza wa Kiswahili kwa shule za upili ulitengenezwa na Kituo cha Kitaifa cha Ukuzaji wa Mtaala (NCDC). Aidha, Kiswahili kiliendelea kutahiniwa kwenye viwango vyote vya sekondari na Bodi ya Mitihani ya Kitaifa (UNEB).

Katika 2019, Wizara ya Elimu na Michezo ilitangaza mtaala mpya wa shule za upili. Mtaala mpya wa sekondari kwa kiwango cha chini unabainisha kuongezeka kwa idadi ya masomo ya lazima likiwemo somo la lugha ya Kiswahili kufundishwa kwa vipindi viwili kila wiki kwa kidato cha kwanza na cha pili. Kituo cha Kitaifa cha Kukuza Mitaala pia kimeandaa mtaala mpya wa kidato cha kwanza hadi cha nne wa lugha ya Kiswahili katika mtaala mpya. Wizara ya Elimu na Michezo inaeleza kuwa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili unachangia ukuzaji wa stadi za kusoma na kuandika na

mawasiliano yanayokuza kufikiria kwa kina. Mtaala huu tangu wakati huo umekuwa ukitekelezwa na unatumika katika kidato cha kwanza.

Aidha, mtaala wa Kiswahili wa shule ya msingi pia umekabili changamoto katika juhudi za utekelezaji wake. Silabasi ya Kiswahili ya shule za msingi iliasisiwa na Kituo cha Kitaifa cha Ukuzaji Mitaala mnamo 2012 licha ya kutoanzishwa na kufundishwa shuleni hadi leo. Hali hii inaacha pengo katika juhudi za ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda. Nsookwa (2014) anabainisha kuwa mtaala wa Kiswahili wa shule za msingi unapendekeza Kiswahili kufundishwa kwa vipindi viwili tu kwa wiki huku lugha nyingine za kiasili kama Kiganda kikipewa vipindi 3 kwa wiki. Ikiwa ufundishaji wa Kiswahili utanza katika shule za msingi, je, vipindi viwili vitawapa wanafunzi muda wa kutosha wa kufahamu lugha hiyo? Kwa sababu ya hali ya utekelezaji kama hii wa mtaala, Kiswahili kiko hatarini nchini Uganda.

Hivi sasa, sera ya lugha ya Uganda inahitaji kwamba shule za vijijini zinapaswa kuchagua lugha kuu ya kiasili kutumika kama lugha ya kujifunza na kufundisha kwa miaka mitatu ya kwanza ya shule ya msingi wakati Kiingereza kinafundishwa kama somo. Mwaka wa nne wa masomo ni mwaka wa mpito ambapo Kiingereza huanza kutumika kama lugha ya ujifunzaji na ufundishaji. Sera kama hiyo ya lugha inakipa Kiswahili mwanya mdogo kuendelezwa, hasa kupitia sekta ya elimu.

Ripoti tofauti za tume za elimu zilipokelewa kwa maoni tofauti kutoka kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya sekta ya elimu hasa kuhusu mapendekezo ya lugha ya Kiswahili (Ssekamwa, 2000: 134; Ssekamwa na Lugumba, 2001: 27). Hata hivyo, mengi ya mapendekezo hayo yamechukua muda mrefu sana kutekelezwa na mengine hayajawahi kutekelezwa kikamilifu. Kwa mfano, baadhi ya tume zilipendekeza lugha

ya Kiswahili kufundishwa katika shule za msingi na sekondari kama somo la lazima lakini wizara ya elimu haijalitilia mkazo suala hili. Hali hii imepunguza kasi ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda.

Licha ya matamko yaliyoainishwa katika tume zilizojadiliwa hapo juu; za kikoloni na za baada ya ukoloni, Mkataba wa Katiba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Katiba ya Uganda na mtaala wa elimu ya msingi na sekondari kati ya zingine, sera ya lugha ya Uganda haijawahi kuwa na utekelezaji kamili huku nchi kadhaa barani Afrika zimependekeza sera za lugha wazi na kuzitekeleza kwa umakini. Hali hii inaendelea kuweka nafasi ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili katika hali dhaifu ambayo inaweza kuhatarishwa kwa urahisi. Vivyo hivyo, nadharia ya upangaji lugha ya Haugen inachangia kukuza wazo kwamba katika kuchagua lugha kwa kusudi maalumu kama lugha ya kitaifa, sera rasmi kuhusu lugha hiyo lazima ifanyiwe utekelezaji kikamilifu.

4.2 Hadhi ya Sera ya Lugha katika Elimu Kuhusu Kiswahili

Kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti huu la kujadili nafasi ya sera ya lugha kuhusu maendeleo ya Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda, mtafiti alishirikisha washiriki kwa kuchunguza maoni na maarifa waliyokuwa nayo kuhusu suala hilo. Washiriki hasa mkurugenzi wa elimu, watunzi wa mitaala, walimu, mwakilishi wa chama cha kitaifa cha utetezi wa maendeleo ya Kiswahili na wengine, walishirikishwa katika kujibu maswali kuhusu walichojua juu ya sera ya lugha kuhusu Kiswahili. Asilimia themanini na tano ya washiriki hawa walikiri kujua matamko ya sera ya lugha yaliyoko yanayoathiri maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika sekta ya elimu. Walitaja nyaraka za sera kama katiba ya Uganda ambayo inatambua lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya pili ya Uganda baada ya Kiingereza, ripoti ya Kajubi na hati ya serikali ya sera ya elimu ya 1992 ambayo inapendekiza ufundishaji wa

lugha ya Kiswahili katika taasisi za elimu hasa kwenye ngazi ya msingi. Aidha, mwakilishi wa CHAKITAU alisisitiza kwamba matamko kama haya ndiyo yamewapa fursa na msingi wadau mbalimbali kupigania na kutetea haki ya maendeleo ya Kiswahili.

Washiriki walitambua fursa katika mtaala mpya kwa kiwango cha sekondari unaozingatia umilisi ulioanza kufundishwa mnamo 2020 kama msingi wa ukuaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda. Mtaala huu unatamka kuwa lugha ya Kiswahili ni somo la lazima katika kidato cha kwanza na pili, jambo ambalo washiriki waliamini litatengeneza na kuboresha njia ya ukuaji wa Kiswahili kwani mtaala huu umekipa Kiswahili jukwaa la kushindana na lugha nyingine. Aidha, washiriki walifunua kuwa katika enzi za utawala wa Iddi Amin, alikuwa ametoa amri ambayo ilifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Uganda. Amri hiyo haijawahi kufutwa, kwa hivyo, bado inaweza kudai kutekelezwa.

Washiriki pia walirejelea mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Uganda ni nchi mwanachama. Mkataba unapendekeza Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano kikanda kwa hivyo ni jukumu la Uganda pia kushiriki katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Washiriki walidai kuwa suala hili litatoa fursa na jukwaa thabiti kwa vyama vya wadau wa utetezi, shule, vyuo vya mafunzo ya ualimu na taasisi nyingine za elimu kukuza lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, asilimia kumi na tano (15%) ya washiriki walikosa ufahamu wa kutosha wa sera ya lugha iliyopo katika elimu na athari zake katika ukuaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Hawa pia walibaini kuwa kulikuwa na sera isiyoeleweka ya lugha na kwa hivyo kusababisha hali ya Kiswahili isiyoeleweka katika sekta ya elimu na taifa kwa ujumla. Pamoja na hilo, washiriki walioonyesha

uelewa wa hati za serikali zinazotaja Kiswahili, walikashifu serikali kwa kuchukua muda mrefu bila kuwezesha utekelezaji wa matamko ya sera mbalimbali kuhusu ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Hali hii ilimfanya mshiriki mmojawapo adai kwamba lugha ya Kiswahili ina hadhi isiyoeleweka na yenye utata katika sekta ya elimu.

Nukuu 1:

Kiingereza

...the policy about actually Kiswahili in Uganda is that it is by constitution actually it is the second official language, and when we come to education, it is supposed to be taught in all secondary schools. Actually, the programs of being taught in primary schools is on the way and I think NCDC talked of Kiswahili also to be taught but could be assessed under continuous assessment. Then the new curriculum of lower secondary schools also Kiswahili being compulsory in Senior one and Senior two then the upper, the Senior three and Senior four, it becomes optional (IP2, September 2020).

Kiswahili

Kwa mujibu wa katiba ya nchi ya Uganda, Kiswahili ni lugha rasmi ya pili, na katika elimu, Kiswahili kinapaswa kufundishwa katika shule zote za upili. Hata hivyo, mipango ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi inaendelezwa na Kituo cha Taifa cha Kuendeleza Mitaala (NCDC). Halafu katika mtaala mpya wa shule za sekondari, Kiswahili ni somo la lazima katika kidato cha kwanza na pili, halafu ni somo la hiari katika kidato cha tatu na nne (MT2, Septemba 2020).

Katika baadhi ya nchi za Afrika ambazo ni za wingi lugha, suala la sera ya lugha kwa kuzingatia uchaguzi wa lugha katika elimu ni msingi wa mjadala juu ya jukumu la elimu katika nyanja zote za maendeleo katika bara hili. Ikumbukwe kwamba masuala ya elimu na lugha ni magumu sana barani Afrika hasa kwa sababu ya hali ya makabila mengi, lugha nyingi kama vile hali ilivyo nchini Uganda. Hali inakuwa mbaya zaidi wakati lugha rasmi ya taifa hilo ni tofauti na lugha yoyote ya asili. Kuna changamoto kila wakati kuhusu lugha ya kutumia shuleni hasa katika kiwango cha chini cha elimu ya msingi katika jamii za wingi lugha (Owu-Ewie, 2006). Hii ni changamoto kama

ilivyoonyeshwa hapo juu ambapo Uganda imekuwa ikipambana nayo kwa miaka kadhaa.

Aidha, ilibainika kutoka kwa asilimia thelathini na nane (38%) ya washiriki kwamba baadhi ya matamko yanayotambulika ya sera ya lugha hayakusaidia ukuaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Licha ya kuweko kwa matamko pamoja na amri za kisiasa, washiriki walilaumu kutokuwepo kwa mikakati ya kutekeleza sera hasa kuhusu Kiswahili katika elimu. Walisema kuwa hakukuwa na utaratibu maalumu wa kutekeleza sera ya lugha ambayo inaelezea wazi hali na miktadha ya matumizi ya Kiswahili katika elimu. Walidai kuwa ndiyo sababu shule zingine hazikufundisha lugha ya Kiswahili licha ya kuwa lugha ya pili rasmi kikatiba. Hata hivyo, ilibainika kuwa walioizungumza katika baadhi ya shule na taasisi za kielimu waliadhibiwa kama wazungumzaji wa lugha ya kiasili. Kwa hivyo, baadhi ya wanafunzi hawaelewi kiini cha kujifunza au kuzungumza lugha ya Kiswahili iwapo hawapewi nafasi ya kujieleza katika lugha hiyo. Mshiriki alibaini kuwa:

Nukuu 2:

Kiingereza

“I don’t think there is a good policy that enables learners of Kiswahili language to benefit from the knowledge of the language. I mean how many jobs are there for Kiswahili speakers. How many scholarships are there for those that have learnt Kiswahili? How do you expect a language like Kiswahili to develop when there is no much value attached to knowing Kiswahili?” attaching benefits and value to learning Kiswahili would be a good strategy and motivation for people to learn and develop Kiswahili language (Ip 8 Septemba 2020)

Kiswahili

“Sidhani kuwa kuna sera nzuri inayoweza wanafunzi wa lugha ya Kiswahili kufaidika na maarifa ya lugha hiyo. Kwa mfano, kuna kazi ngapi kwa wasemaji wa Kiswahili. Ni wangapi wanaweza kupata ufadhili wa kujiendeleza masomoni eti kwa sababu wamesoma Kiswahili? Je! Unatarajia lugha kama Kiswahili ikue wakati hakuna thamani kubwa inayoambatana na kuijua? ”

...kuambatanisha faida na thamani ya kujifunza Kiswahili itakuwa mkakati mzuri na motisha kwa watu kujifunza na kukuza lugha ya Kiswahili (MT8 Septemba 2020)

Washiriki pia walizungumzia suala la serikali kushindwa kuwezesha utekelezaji wa sera zilizopo. Walitoa mfano wa hati ya serikali ya sera ya elimu ya 1992 ambayo haijatekelezwa kikamilifu kwa kukuza Kiswahili. Washiriki walilinganisha suala hili na sera zinazohusiana na lugha ya Kiingereza na jinsi zilivyo wazi, ambazo ziliweza kusababisha ukuaji mkubwa wa lugha ya Kiingereza hasa katika sekta ya elimu:

Nukuu 3:

Kiingereza

Aaaah! The policy in most cases, you know it has remained on paper but it has not worked well actually. Practically it has not worked, it has remained on paper. As I said it is supposed, they had actually talked that Kiswahili should be taught in all secondary schools but remained like that. It was not implemented because as I talk, the teachers have not been given jobs, have not been employed by the government (IP2, September, 2020)

Kiswahili

Sera kuhusu Kiswahili haijatimizwa, imebaki tu katika machapisho. Iisemekana kwamba Kiswahili kilipaswa kufundishwa katika shule zote za upili lakini hilo halikutekelezwa. Hata walimu wa Kiswahili hawajaajiriwa na serikali (MT2, Septemba, 2020)

Nukuu 4:

Kiingereza

According to me,.... about the Kiswahili language policy, in Uganda, to me I don't find a well laid Kiswahili language policy. I find that is not a formal policy that any institution should rely on because a policy is meant to be passed by the parliament, passed by all educational sects and respected and used in all formal sectors by law but when you look at what was passed, and what is being implemented in the new curriculum, it is just an overhaul that they put, but to me there is nothing like language policy that is functional in secondary schools (Ip7...October 2020)

Kiswahili

Kwangu mimi sioni sera ya lugha ya Kiswahili iliyo wazi. Ninaona kwamba hiyo si sera rasmi ambayo inafaa kutegemewa na taasisi yoyote kwa sababu sera inafaa kupitishwa na bunge, vitengo husika

vya kielimu na sekta rasmi za serikali. Kwa hivyo, kwangu mimi, sioni sera ya lugha ambayo inatekelezwa katika shule za upili (MT7... Oktoba 2020)

Nukuu 5:

Kiingereza

About the school language policy, my school being in the central setup, there is a lot of influence on the first language, a lot of first language influence compared to Kiswahili. when Kiswahili was introduced, it was given limitations and one of the limitation was, not everyone should offer Kiswahili. That is the school language policy, that the priority is given to Luganda until 2020 when the new curriculum came in that the current S1 should learn Kiswahili but from 2019 backwards, the policy has been that Luganda takes first priority and you find that in a class of senior one, senior two where we have seven streams or eight, four are restricted to doing Luganda, the rest the other languages like Swahili, French and Arabic....so you find Kiswahili fighting for the remaining few students (Ip7...October 2020)

Kiswahili

Kuhusu sera ya lugha, shule yangu inapatikana katika jimbo la kati ambako kuna athari kubwa ya lugha ya kwanza dhidi ya Kiswahili. Kiswahili kilipoanzishwa, hakikupewa kipaumbele, siyo kila mwanafunzi anapaswa kusoma Kiswahili shuleni. Hiyo ndiyo sera ya lugha ya shule, kipaumbele kilipewa Luganda hadi 2020 wakati mtaala mpya wa sekondari ulipoanzishwa unaotaja Kiswahili kama somo la lazima katika kidato cha kwanza. Katika miaka ya nyuma, sera imekuwa kwamba Luganda inapewa kipaumbele. Ugepata kwa mfano katika kidato cha kwanza, idadi kubwa ya wanafunzi ndio wanasoma Luganda halafu lugha nyingine kama Kiswahili, Kifaransa na Kiarabu, zinapigania wanafunzi wachache waliosalia (MT 7... Oktoba 2020)

Mifumo mingi ya elimu katika nchi mbalimbali za Afrika ina mizizi yake katika kipindi cha ukoloni. Mfumo wa elimu rasmi wa Uganda ulianzishwa na wamishonari wa Kikristo katika miaka ya 1800 na hadi sasa baadhi ya sera zimekwamia katika mawazo ya enzi hizo za ukoloni. Kwa hivyo, sera nyingi za elimu hazijavunja mkururo huo kutoka zamani. Nchi nyingi za Afrika zimekuwa na sera za kitaifa kwa muda mrefu na wakati mwingine zilizoanzia nyakati za ukoloni, kwa matumizi ya lugha za kitaifa katika elimu. Lakini kwa miaka mingi imekuwa dhahiri kuwa

kukubalika kwa sera hii kitaifa si kwa urahisi. Kwa mfano, baadhi ya raia ambao wanaweza kujimudu, hata ikiwa ni pamoja na kuwa watetezi na watekelezaji wa sera ya kitaifa ya lugha katika elimu, wamependelea kupeleka watoto wao katika shule ambazo hazitumii lugha za mama au lugha za kitaifa kabisa, hata wengine wametumia shule zile ambazo hazitumii lugha hizo kama masomo ya kufundisha (Muzoora et al., 2014). Kwa hivyo, vile suala la utekelezaji lilivyo mhimili muhimu katika nadharia ya upangaji lugha ya Haugen, utekelezaji kamili wa matamko ya sera ya lugha kuhusu hali na miktadha ambamo lugha ya Kiswahili inafaa kutumika utabainisha mipaka ya sera ya lugha ya elimu ya kitaifa pamoja na sera ya lugha ya shule kwa ajili ya kukipa Kiswahili hadhi na kipaumbele kuendelezwa kupitia elimu nchini Uganda.

Aidha, katika hali nyingine, sera hiyo ya kufundishia katika lugha za jamii imeshindwa kabisa. Kwa mfano nchi mbili za Burkina Faso na Guinea hapo awali walikuwa wafuasi wakuu wa sera hii ya kufundishia katika lugha za jamii, lakini kwa sasa wamerudi kufundisha kwa lugha ya kimataifa peke yake iliyopitishwa kwa idhini ya serikali (Fyle, 2003).

Dhana hii ina maana kwamba sera ya matumizi ya lugha katika elimu haiwezi kustawi isipokuwa imelinganishwa na sera ya matumizi ya lugha hiyohiyo katika mawasiliano ya kitaifa. Mazoea kama haya hayafai sana kuwekezea juhudi katika elimu ya lugha mama na kusahau lugha ambayo manufaa yake yanatazamwa kwa kiwango cha kitaifa, kikanda na kimataifa, sio tu katika masomo ya shule lakini hata katika kusoma na kuandika kwa jamii za vijijini. Kwa hivyo, mahitaji ya kijamii siyo kwa lugha ya mama au lugha ya jamii tu bali hata kwa lugha rasmi na ya kimataifa (Fyle, 2003).

Kwa upande mwingine, huku asilimia 38 ya washiriki wakilaumu sera zilizopo za lugha kwa kutofanikisha ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu,

wengine waliamini kuwa kuna juhudi ambazo zimefikiwa katika shughuli za ukuzaji wa Kiswahili ambazo hazipaswi kupuuzwa. Asilimia 54 ya washiriki walieleza wazi kwamba matamko katika nyaraka za serikali mbalimbali kuhusu sera ya lugha na hususani Kiswahili, yamechangia pakubwa katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Walidai kwamba ufundishaji wa lugha ya Kiswahili uliopo kwa sasa katika taasisi nyingi ulitokana na mifumo na matamko kama hayo. Kwa hivyo, matamko ya sera hutoa msingi ambao wadau wa elimu wanategemea kukuza Kiswahili. Mshiriki mmoja alibaini kuwa Profesa Emmanuel Karoro na Mwalimu Milton Rwabushaija walianzisha na kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika Chuo cha Kitaifa cha Ualimu cha Kakoba, magharibi mwa Uganda. Mshiriki huyu aliendelea kudai kwamba Profesa E. Karoro pamoja na Mwalimu Milton Rwabushaija wanafaa kukumbukwa katika historia ya ukuzaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda, kama waanzilishi wa ufundishaji na uhamasishaji kuhusu lugha ya Kiswahili. Walijitolea kuanzisha mafunzo ya Kiswahili huku wakiongozwa na kuchochewa na matamko ya sera zinazohusu lugha ya Kiswahili licha ya changamoto zilizokuwepo hasa bila msaada wowote wa serikali. Juhudi hizi zilichangia katika uzalishaji wa walimu waliokubali kupewa mafunzo hasa waliotoka magharibi mwa Uganda. Hata hivyo, washiriki walikuwa na matumaini kwamba juhudi ziko na zilikuwa zinaendelezwa ili kurahisisha mikakati ya utekelezaji wa sera za kuendeleza lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Ushuhuda huu unadhihirishwa kama ifuatavyo:

Nukuu 6:

Kiingereza

...revamping of the teaching of Kiswahili came after the 1992 White Paper on education, I remember that when Profesa Karoro in NTC Kakoba started Kiswahili, because having read that, I was one of the people, I think, that started in the third cohort and he insisted that

Kiswahili is going to be taught and he would quote that White Paper that government is willing (IP6, September 2020).

Kiswahili

Ufundishaji wa Kiswahili ulianza baada ya hati ya serikali juu ya elimu ya 1992, ninakumbuka wakati huo Profesa Karooro akianzisha Kiswahili katika Chuo cha ualimu cha kitaifa cha Kakoba, nilikuwa miongoni mwa wanafunzi na alisisitiza ufundishaji wa Kiswahili na angenukuu tamko katika hati hiyo ya serikali lililotaja kuhusu ufundishaji wa Kiswahili (MT6, Septemba 2020).

Nukuu 7:

Kiingereza

The history of Kiswahili in my view, the white paper gave it a lime light. It is after the White Paper personally I can say the Kajubi commission which it started its work in 1987 and institution like Kakoba picked the interest and started training teachers for Kiswahili, then after the completion of the White Paper, institutions like UNEB started examining Kiswahili at 'O' level and 'A' level consequently the graduates of Kakoba started enrolling for Bachelor's at Makerere University. That one to me are the positive effects of the white paper. Now the subsequent pronouncement of the 1995 follows the White Paper but there comes the revival of the East African Community. Now having known that Uganda is part of the East African Community. I think that the chairman of the constitution knew that and know that Kiswahili is very important that would partly influence putting it in constitution and putting it in constitution could also partly influence some of the schools started teaching it now the recent pronouncement in parliament were parliament allowed NCDC to implement the teaching of Kiswahili in senior one and two is another for Kiswahili as a result of that pronouncement by parliament because it pronounced itself to be part of the compulsory subject (IP5 ..Septemba 2020)

Kiswahili

Kulingana na historia ya Kiswahili, hati ya serikali ya 1992 kuhusu elimu, ilikipa Kiswahili fursa kubwa. Ni baada ya matokeo ya hati hiyo iliyozingatia mapendekezo ya tume ya Kajubi kwamba taasisi kama Kakoba zilipata ari na kuanza kufundisha walimu wa Kiswahili. Baada ya muda mfupi, Bodi ya Mitihani ya Kitaifa (UNEB) pia ilianza kutahini wanafunzi wa kidato cha nne na sita waliokuwa wamesoma Kiswahili. Aidha, wahitimu wa Kakoba walianza kujiendeleza kimasomo kwa Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu cha Makerere.

Kwangu mimi ninaona hiyo ilikuwa ni athari nzuri ya hati hiyo ya serikali kuhusu maendeleo ya kiswahili. Matamko mengine kuhusu Kiswahili yanajitokeza katika katiba ya 1995 pamoja na mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Matamko hayo yalitoa msingi wa

baadhi ya shule kuanzisha ufundishaji wa Kiswahili. Matamko mengine ya hivi karibuni yametokea mwanzoni mwa 2020 ambapo bunge limeridhia uanzishaji wa mtaala mpya wa sekondari ambao unatambua Kiswahili kama somo la lazima katika kidato cha kwanza na cha pili. (MT 5)

Nukuu 8:

Kiingereza

.....I remember some of us from Kakoba we were intentionally given, government gave us scholarship those who would pass well the diploma level would gain entrance to university for a Bachelor's Degree and of course that Bachelor, of course we would come with different subjects but they would insist you have to continue with Kiswahili at graduate level. NCDC as a government entity has been doing all the responsibility, regarding the syllabus ...regarding of the training and re-tooling of teachers of Kiswahili and other materials, teaching and learning materials like text books. In the way so they turn them, develop them, remember they even appointed Kiswahili special inspectors on regional level. I think there was Kampala, there is east such a thing even in UNEB, I think the Kiswahili specialists. The policy pronouncements about Kiswahili have played a big role also to develop Kiswahili in Education (IP1)

Kiswahili

..... Ninakumbuka baadhi yetu waliokuwa wamehitimu vizuri Kiswahili kwa kiwango cha stahhada kutoka Kakoba, tulipewa ufadhili na serikali ili kuendelea kusoma shahada ya Kiswahili chuoni. Hata ingawa tulikuwa tumehitimu masomo mengine likini msisitizo uliwekwa kwenye Kiswahili. Kituo cha Taifa cha Kuendeleza Mitaala (NCDC) kama taasisi ya serikali pia kimeasisi mitaala na kushiriki katika mafunzo ya kuimarisha stadi faafu kwa walimu wa Kiswahili pamoja na uandaaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vitabu vya kiada. Hata hivyo, magalacha na wakaguzi maalum wa Kiswahili wameajiriwa. Matamko ya sera kuhusu Kiswahili yamechangia pakubwa katika kukuza Kiswahili katika Elimu.... (MT 1)

Kutokana na matamko ya sera ya lugha nchini Uganda kama ilivyoelezwa na washiriki, Kiswahili kilipewa hadhi ya juu (rasmi) kuliko vile kilivyokuwa hapo awali; kwa hivyo, nadharia ya upangaji lugha ya Haugen ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu inajumuisha hadhi na majukumu ya lugha nchini Uganda.

Kila nchi ina changamoto zake katika kutekeleza sera za lugha. Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kiswahili ni lugha rasmi ya kitaifa. Hakuna kinachofanyika nchini Tanzania kukuza lugha zile nyingine licha ya nchi hiyo kuwa na zaidi ya lugha 100. Hata hivyo, hakuna uhasama au utafuta wa lugha wowote. Kiingereza kinakuzwa kama lugha ya elimu kutoka ngazi ya sekondari na kuendela. Elimu ya msingi hutolewa kwa Kiswahili, na hili kwa kiwango fulani husababisha changamoto za mabadiliko kutoka kwa Kiswahili kama lugha ya elimu kwenda kwa Kiingereza wakati wanafunzi wakiingia ngazi ya sekondari. Tafiti zinadai kuwa viwango vya elimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vimeshuka kutokana na sera hii kwa sababu nchi imeshindwa kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika ngazi za sekondari na vyuo vikuu (Abdulaziz, 2003). Nchini Kenya sera ya lugha inatamka kufundishia katika lugha mama katika miaka mitatu ya kwanza ya elimu ya msingi na Kiingereza kufundishwa kama somo. Kisha Kiingereza hutumika kama lugha ya kufundishia kuanzia darasa la nne hadi kiwango cha chuo kikuu. Kiswahili hufundishwa kama somo la lazima kuanzia darasa la nne hadi sekondari na hutahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne. Aidha, hutumika kama lugha ya kufundishia katika miaka mitatu ya kwanza katika maeneo ya miji tu yenye wanafunzi kutoka jamii tofauti (Mose, 2018:4). Kwa hivyo, kama ilivyowasilishwa na washiriki katika utafiti huu, matamko na sera zilizopo zimetoa msingi kwa taasisi za elimu kutumia na kukuza lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Aidha, ningependa kusema kwamba kuna msimamo na ushahidi kwamba sera ya lugha na elimu ya lugha hutumika kama vyombo vya kukuza uhai, utofauti, na utulivu wa lugha. Hii ndiyo sababu lugha ya Kiswahili hasa nchini Uganda inapaswa kupewa kipaumbele sawa au zaidi katika uwanja wa elimu ya lugha kwa maendeleo ya haraka na kukubalika katika jamii.

4.3 Muhtasari wa Sura

Sura hii ililenga kujadili matokeo ya utafiti wa sera ya lugha katika mfumo wa elimu na athari zake katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Katika sura hii hasa, data imewasilishwa juu ya lengo la kwanza ambalo lilijikita katika kujadili nafasi ya sera ya lugha katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda

SURA YA TANO

CHANGAMOTO ZINAZOKABILI UKUAJI WA KISWAHILI KUPITIA

MFUMO WA ELIMU NCHINI UGANDA

5.0 Utangulizi

Sura hii inajadili na kuwasilisha data juu ya lengo la pili la utafiti huu lilijikita katika kufafanua changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu.

Ili kufikia lengo hili, mtafiti alishirikisha washiriki 13 waliochaguliwa kimaksudi kutoka taasisi 13. Hawa walikuwa watunzi wa sera, waratibu na watekelezaji sera za lugha. Data kutokana na mahojiano zilichanganuliwa na kuwasilishwa. Data zilizokusanywa zilijibu swali: Ni changamoto zipi zinazokabili ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu? Mtafiti alitumia nambari na misimbo badala ya majina ya washiriki na shule ili kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya kimaadili kama usiri, faragha, na kutokujulikana.

Ilibainika kwamba baadhi ya nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile Tanzania, Kenya, Burundi na Rwanda zilikuwa zimejitahidi kuendeleza ukuaji wa Kiswahili. Hata hivyo, juhudi za kuendeleza Kiswahili nchini Uganda bado zilikabiliwa na vikwazo mbalimbali. Asilimia hamsini na nne (54%) ya washiriki walidai kwamba ukosefu wa utashi wa kisiasa, ni mojawapo ya changamoto nyingi zinazokabili ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda.

5.1 Ukosefu wa Utashi wa Kisiasa

Mojawapo ya masuala muhimu yaliyoibuka kutokana na mahojiano ni upungufu wa umakini wa kisiasa ili kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda kwa kurejelea matamko ya sera yaliyokuwepo. Washiriki walionyesha ukosefu wa utashi wa

wanasiasa katika juhudi za maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda licha ya kuichukulia kuwa lugha ambayo ingeunganisha Wanauganda. Hii ni kwa sababu Uganda ni jamii ya wingi lugha na hakuna kabila linalodai kumiliki lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, hali hii ya ukosefu wa utashi kutoka kwa serikali na maafisa wake hasa wanasiasa, ilihofiwa kuwa tatizo sugu katika mchakato wa kukuza Kiswahili nchini Uganda.

Washiriki walikuwa na mashaka juu ya viongozi wengi wa kisiasa kuunga mkono maendeleo ya lugha ya Kiswahili kwa sababu ya madai na visingizio vya fedha kidogo au wakati mwingine hakuna fedha au bajeti maalumu inayotengwa kwa shughuli za ukuzaji wa Kiswahili. Washiriki walibainisha kwamba serikali na viongozi wa kisiasa walikuwa wameendelea kuzingatia urithi wa sera za lugha za kikoloni licha ya juhudi za bunge kuelezea hadhi ya Kiswahili kama lugha rasmi ya pili ya Uganda kikatiba. Licha ya kuwa na ripoti wazi zilizo rasmi za serikali na matamko ya sera ya lugha kuhusu nini kifanyike kueneza lugha ya Kiswahili nchini Uganda, washiriki walielezea kuwa watungaji sera na watekelezaji hawajatia bidii kufanikisha hili:

Nukuu 9

Kiingereza

...the political will is very weak. I mean no body is there to push for Kiswahili but there were people to push local languages, the banyankore pushed, baganda pushed and whatever, the policy has been there but with Swahili people to push? So that has been the weak patronage because the policies are there but the political will. (IP3....Oktoba 2020)

Kiswahili

Utashi wa kisiasa umekuwa dhaifu. Kumekuwa hakuna watu wa kutetea utekelezaji wa Kiswahili lakini badala yake kumekuwa na wantetezi wa lugha za kiasili. Sera imekuwepo lakini kumekuwa hakuna wadau wa kushinikiza uendelezaji wa Kiswahili kama hali ilivyokuwa katika lugha nyingine. Kwa hivyo Kiswahili kimekosa utetezi. Hata ingawa sera imekuwepo, utashi wa kisiasa umekuwa dhaifu kuhusu Kiswahili.(MT3 .. Oktoba 2020)

Nukuu 10***Kiingereza***

Failure by government to make Kiswahili a compulsory subject in Ugandan schools ... for a while, this has remained a challenge to the ministry even at the part of the government itself.... (IP6).

Kiswahili

Kwa muda mrefu, serikali imeshindwa kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule nchini Uganda... Suala hili limebaki kuwa changamoto kwa wizara hata kwa upande wa serikali yenyewe.... (MT6).

Nukuu 11***Kiingereza***

... so what can finally change is a stronger political will to assert, to affirm and it becomes right away, otherwise most of the things needed to implement Kiswahili are there, the teachers are there, the institutions are there, the books are there.... (IP3)

Kiswahili

... Kwa hivyo, kinachohitajika ni utashi wa kisiasa thabiti ili kuthibitisha utekelezaji na uendelezaji wa Kiswahili moja kwa moja. Mambo mengine yanayohitajika kutekeleza Kiswahili yapo, kwa mfano, walimu wapo, taasisi zinazofundisha na zinazoweza kuanzisha ufundishaji wa Kiswahili zipo pamoja na vitabu vya kufundishia Kiswahili vipo...(MT 3)

Spolsky (2004) anadai kwamba sera ya lugha pamoja na upangaji lugha kwa kiwango kikubwa ni masuala yanayoongozwa na maamuzi ya kisiasa. Masuala ya sera ya lugha mara nyingi huamuliwa kwa misingi ya kisiasa badala ya kiutendaji. Kutokana na mawasilisho hayo hapo juu, inaelekea kuwa serikali imekuwa na mwendo wa kinyonga katika kutekeleza sera zilizopitishwa. Jaribio la kwanza la kutangaza Kiswahili kama lugha rasmi lilitokea mnamo 1973 ilipoamriwa na Rais Iddi Amin kama lugha ya kitaifa. Mnamo 2005 katika marekebisho ya katiba, lugha ya Kiswahili ilitamkwa tena mara ya pili kama lugha rasmi ya pili na ilitarajiwa kwamba watekelezaji wa sera waweke mikakati ya kukiendeleza kwa kiasi kikubwa ingawa hali haijawa hivyo. Kwa hivyo, kuna haja ya utashi wa kisiasa ili kuendeleza lugha hii inayozungumzwa na watu zaidi ya milioni 100 katika bara zima la Afrika. Hili

lingeifanya lugha hii kukubaliwa na kutumiwa na jamii za Uganda hasa kupitia katika sekta ya elimu.

Ijapokuwa Kiswahili kina jukumu muhimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama lugha ya mawasiliano, bado kinakabiliwa na changamoto kadhaa kama ilivyodaiwa na washiriki, ukosefu wa utashi wa kisiasa ni moja wapo ya changamoto. Ni bayana kwamba nchi za Tanzania na Kenya kama wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zimekipa Kiswahili hadhi na mapenzi mema kijamii na kisiasa (Habwe, 2009). Sera zilizo wazi zimetamkwa na kwa kiwango kikubwa zimetokelezwa kuhusu matumizi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili.

Nchini Tanzania, Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ndicho chama kikuu cha kisiasa kimeunga mkono ukuaji na ueneaji wa Kiswahili kwa kuunda taasisi za kuendeleza ukuaji na ueneaji wa Kiswahili kama Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Hata hivyo, ikumbukwe kuwa pamoja na kuwepo kwa ubepari na changamoto za utandawazi, kuna mwelekeo wa nchi nyingi zinazozungumza Kiingereza kama lugha rasmi hasa Uganda kuelekea kuendeleza usomaji wa Kiingereza jambo ambalo linaaminika na kuchukuliwa kama fursa ya ajira kwa watoto wao kwenye kiwango cha kimataifa. Jambo hili linaweza kuelezea kwa nini Uganda hadi sasa bado haijakipa Kiswahili kipaumbele licha ya mapendekezo katika ripoti ya Profesa Kajubi na hati ya serikali ya 1992 ambayo inasisitiza mahitaji ya ukuaji wa lugha ya Kiswahili hasa kupitia sekta ya elimu.

Hati ya Serikali ya 1992 iliyoandikwa kujibu na kutekeleza mapendekezo ya ripoti ya tume ya kukagua sera ya elimu kwenye kauli mbiu ya 'Elimu kwa Ujumuishaji na Maendeleo ya Kitaifa', ilipendekeza kwamba Kiswahili na Kiingereza viwe masomo ya lazima katika kipindi chote cha elimu ya msingi katika maeneo ya vijijini na

mijini. Mnamo 2003, serikali iliamuru Wizara ya Elimu kuanzisha mafunzo ya lazima ya Kiswahili katika ngazi zote za shule ili kufikia malengo ya Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya Kiswahili kutumika kama lugha ya kikanda. Hadi leo, serikali bado haina utashi madhubuti wa kisiasa ili kutekeleza kikamilifu mapendekezo katika ripoti hizi ambazo zingeongoza maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda. Inaweza kuchukuliwa kwamba suala hili limekuwa kikwazo kwa Kiswahili kuhusiana na juhudi za kueneza na kukuza lugha. Kiswahili ndiyo lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo ina Tume ya Kiswahili ya kukuza matumizi yake kikanda na kusaidia nchi wanachama katika masuala yoyote ya ukuzaji wa Kiswahili. Hata ingawa uanachama wa Uganda katika Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unajumuisha pia jukumu la kukuza matumizi ya Kiswahili, bado kuna ukweli dhahiri juu ya ukosefu wa utashi thabiti wa kisiasa na ufanisi ambao bado unadhoofisha juhudi na sera zilizopo za kukiendeleza Kiswahili na kukubalika kwa raia. Inaweza kusemwa kuwa Uganda haijapata watu wenye nguvu za kisiasa kama Julius Nyerere wa Tanzania kuongoza maendeleo ya Kiswahili nchini Uganda.

Nchini Ghana, kwa mfano, harakati za Kwame Nkrumah za umoja wa Waafrika na utetezi wa kupitishwa kwa Kiswahili kama lugha ya bara, hali hii iliunda msingi wa Kiswahili kuanzishwa katika baadhi ya taasisi nchini Ghana na Waghana wengi kupata ari ya kujifunza Kiswahili (Dzahene-Quarshie, 2013). Nchini Kenya, kulikuwa na vikundi vitatu vilivyoathiri sera ya lugha. Wamishonari walitaka kukuza Lugha za kienyeji, ambazo zilikuwa zaidi ya arobaini kwa madhumuni ya elimu ya msingi na katekisimu. Walowezi walipendekeza sana Kiswahili na lugha za wenyeji, huku wafanyakazi wa serikali ya Uingereza waliona ni bora Kiingereza kianzishwe mapema iwezekanavyo katika mfumo wa elimu kama njia bora ya kuhakikisha maendeleo ya Afrika (Ouane, 2003).

5.2 Ukosefu wa Mikakati ya Kutekeleza Sera ya Lugha kuhusu Kiswahili

Washiriki wa utafiti huu walikashifu ukosefu wa mikakati madhubuti ya kutekeleza sera ya lugha ya Kiswahili licha ya kuwepo kwa matamshi na ripoti kadhaa. Waligundua kuwa matamko na sera za lugha zilikosa ufadhili na mikakati ya makusudi ya ukuzaji na uimarishaji wa lugha ya Kiswahili. Ilikuwa wazi katika hisia za washiriki kwamba serikali imeshindwa kutekeleza kwa uwazi matamko ambayo yangekifanya Kiswahili kuwa somo la lazima katika taasisi zote za ujifunzaji. Hata hivyo, walibaini kuwa kulikuwa na utekelezaji wa sera kwa njia isiyofaa lugha ya Kiswahili kutokana na idadi ya masomo yanayotolewa kwenye ngazi ya juu ya sekondari.

Aidha, washiriki walibaini kuwa utata kati ya sera hasa sera ya shule na matamko ya sera ya lugha ya elimu hufanya juhudi za kukuza Kiswahili kuwa dhaifu. Ilibainika kuwa wakati wizara ya elimu inasema kwamba shule zinapaswa kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kuandika na kuzungumza lugha ya Kiswahili, sera nyingi za shule haziruhusu kuzungumzwa kwa Kiswahili katika maeneo ya shule kwani wanaona ni lugha ya kawaida ambayo inahitaji adhabu iwapo mwanafunzi atapatikana akiiongea. Kiswahili kama lugha nyingine yoyote inahitaji mazoezi ya uzungumzaji na hali kama hiyo ya kuzuia wanafunzi kuitumia katika mazungumzo shuleni inaleta changamoto kwa ukuzaji wake. Washiriki walidokeza kuwa hali hii inaweza kuwa ni kwa sababu ya ukosefu wa mikakati ya kutekeleza sera ya lugha kuhusu Kiswahili hasa kupitia sekta ya elimu.

Hii ni dhahiri katika nukuu za washiriki kama ifuatavyo:

Nukuu 12

Kiingereza

.....Kiswahili was laid down as an official language after English to be used, but unfortunately, Uganda has lacked a coherent policy

on language development, so it leaves Kiswahili in an ambiguous position.... (IP7)

Kiswahili

Kiswahili ni lugha rasmi ya pili baada ya Kiingereza, lakini kwa bahati mbaya, Uganda imekosa sera madhubuti juu ya ukuzaji wa lugha, kwa hivyo imekiacha Kiswahili katika hali isiyoeleweka (MT7)

Nukuu 13

Kiingereza

.....the policy in most cases, you know it has remained on paper. It has not worked well actually, practically it has not worked, it has remained on paper. As I said it is supposed, they had actually talked that Kiswahili should be taught in all secondary schools but remained like that, it was not implemented because as I talk, the teachers have not been given jobs, have not been employed by the government so you cannot say that the subject should be taught but again you do not deploy the teachers. So it has not impacted on it, actually it has remained passive (ip2).

Kiswahili

Sera ya lugha imebaki kwenye karatasi. Kiswahili kilipaswa kufundishwa katika shule zote za sekondari lakini hilo halikutekelezwa kwa sababu walimu hawajaajiriwa na serikali. Haina maana kusema kuwa somo linapaswa kufundishwa na huajiri walimu. Kwa hivyo sera haijaathiri uendelezaji wa Kiswahili. (MT 2)

Kategoria ya lugha za mawasiliano mapana haijafahamika wazi nchini Uganda licha ya kutangazwa sana na Muungano wa Umoja wa Afrika na pia UNESCO kwa kiwango fulani na nchi wanachama wenyewe katika Muungano kwa miaka iliyopita. Siyo kwamba Uganda haiamini umuhimu wa lugha hizo lakini ni kwa sababu zimekuwa hazijatiliwa maanani hasa katika elimu (Fyle, 2003). Nchi za Tanzania na Kenya zimekuza na kuendeleza Kiswahili katika nyanja zote za maisha ya kila siku. Uganda imekosa sera madhubuti ya serikali juu ya ukuzaji wa lugha na msimamo wa Kiswahili nchini Uganda umekuwa wa kutatanisha sana (Pawliková-Vilhanová, 1996; Nakayiza, 2013; Jjingo, 2018). Ni nchi chache za Kiafrika hadi sasa ambazo

zinajulikana kujaribu kusuluhisha hili. Kwa mfano, ni katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo lugha nyingi za kiasili zimetumika kama chanzo cha msamiati wa utajiri wa lugha ya kitaifa ambayo ni Kiswahili. Nchi kama Uganda ambayo haina lugha moja ya mawasiliano ingepaswa kujifunza kutokana na suala kama hili.

Aidha, ni jambo la aibu kwamba nguvu za kisiasa na kiuchumi bado zina uwezo mkubwa kuamua kuhusu sera ya lugha katika elimu bila kuzingatia mahitaji ya kijamii, kisaikolojia na ufundishaji. Ukweli hata hivyo ni kwamba, nchi za Kiafrika Uganda ikiwemo, zinaendelea kuhamia na kutoka katika matumizi ya lugha za kienyeji na pia lugha za kigeni kama lugha za kufundishia bila utekelezaji wa matakwa ya sera ya lugha ya asili iliyo wazi.

5.3 Serikali Kutoajiri Walimu wa Kutosha wa Kiswahili

Washiriki walielezea ukosefu wa kazi za kufundisha Kiswahili licha ya kuongezeka kwa upatikanaji wa walimu wa Kiswahili. Washiriki wengi walibaini kuwa kuna ukosefu wa ajira katika serikali na taasisi za kibinafsi. Waliilaumu serikali ambayo imekuwa ikitangaza nafasi chache ikilinganishwa na nafasi zingine za lugha kama Kiingereza. Jambo hili limezorotesha ukuzaji na ukuaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu.

Katika utafiti huu, ilibainika pia kuwa ukosefu wa ajira uliwavunja moyo wanafunzi wasiendeleo na usomaji wa lugha ya Kiswahili kama mojawapo ya masomo yao kwa sababu ya kutopatikana kwa walimu wa Kiswahili katika shule zao. Vivyo hivyo, washiriki wengine walisema kwamba kulikuwa na nafasi chache za kufundisha hasa kwa upande wa shule za kibinafsi kwani baadhi ya wakuu wa shule wanaona ni upanuzi wa gharama kwa shule. Kwa hivyo, shule zinashindwa kuajiri walimu wa Kiswahili waliopo. Kwa mfano;

Nukuu 14

Kiingereza

... I want to say, we have enough secondary school teachers, who have come out of all these universities in Uganda. From within and from out of the country. The only challenge that we have is that the government hasn't been in position to take them on, all of them so some schools have continued missing Swahili teachers not because that they are not there but because the government always says the wage bill is not big enough to take all of them (IP3).

Kiswahili

Ninataka kusema kwamba, tunao walimu wa kutosha wa shule za upili ambao wamehitimu kutoka vyo vikiu nchini Uganda na nje. Changamoto pekee tuliyonayo ni kwamba serikali haijawa tayari kuwaajiri. Kwa hivyo, baadhi ya shule zimeendelea kukosa walimu wa Kiswahili siyo kwa sababu hawako lakini kwa sababu serikali imekuwa na kisingizio cha kutokuwa na uwezo wa kuwaajiri wote eti kwa sababu ya bajeti ya mshahara usiotosha (MT3)

Mwishowe, ilibainika kuwa hakukuwepo na usawa wa upatikanaji wa walimu wa Kiswahili kimkoa au kimaeneo. Mshiriki alieleza kuwa walimu wa Kiswahili walipatikana sana katika magharibi mwa Uganda kuliko mikoa mingine nchini. Suala hili pia lilijadiliwa kama changamoto mojawapo iliyosababisha kutoenea kwa Kiswahili kiusawa katika mikoa yote nchini Uganda. Madai haya yalidhihirishwa hivi:

Nukuu 15

Kiingereza

About many Kiswahili teachers in Western Uganda, when I talk or bring it like that, that there are more teachers of Kiswahili on payroll in western Uganda than any other region in the country, someone who doesn't understand.....the history of Kiswahili in Uganda ...would think it is deliberate move by government. The lay man's reason I can give; it was possibly because Kakoba was in western Uganda. It produced more teachers of Kiswahili. So after the phasing off of Kakoba, still Kabale is in western Uganda and starting Kiswahili it was an initiative of the principal of NTC Kakoba. He was called Professor Karoro Emmanuel. The same I will put a blame to other principals of the other NTCs in other regions who didn't attach value to Kiswahili. I will also look at the MOE, it has been reluctant and possibly the imbalance could be all along Kiswahili has been an optional subject. So it was upon

schools to decide and now western Uganda having the labor they decided and possibly had more teachers on payroll. I will also say, partly government erred, it could look into it and have these people distributed evenly in the whole country. But never late than never...(ip5)

Kiswahili

Ninapozungumzia kuhusu walimu wengi wa Kiswahili ambao wameajiriwa na serikali katika eneo la magharibi mwa Uganda kuliko mkoa wowote mwingine nchini, mtu asiyelewa historia ya Kiswahili nchini Uganda anaweza kufikiria kwamba serikali ilikusudia hivyo. Sababu iliyo bayana ni kwamba Chuo cha Ualimu cha Kitaifa cha Kakoba kilikuwa magharibi mwa Uganda. Chuo hiki kilitoa walimu wengi wa Kiswahili. Hata hivyo, kilipofungwa, mafunzo ya Kiswahili yaliamishwa hadi Chuo cha Ualimu cha Kitaifa cha Kabale ambacho pia kilipatikana magharibi mwa Uganda. Ufundishaji wa Kiswahili chuoni Kakoba ulikuwa umeanzishwa na mkuu wa Chuo hicho aliyeitwa Profesa Karooro Emmanuel. Vivyo hivyo nitawalaumu wakuu wa Vyujo vya Ualimu vya Kitaifa katika mikoa mingine wakati huo ambao hawakutambua thamani ya Kiswahili. Wizara ya Elimu na Michezo kushindwa kufanya Kiswahili somo la lazima, pia kumeathiri upatikanaji wa walimu wa Kiswahili kote kwa usawa. Kwa hivyo, hiyo ndiyo sababu ya magharibi mwa Uganda, kuwa na walimu wengi wa Kiswahili kuliko mikoa mingine kwa sasa. Hata hivyo, huenda ni makosa ya serikali kwa sababu walimu hawa wangeweza kusambazwa kwa usawa nchini kote. Hata hivyo, hawajachelewa sana.... (MT 5)

Mulokozi (2016) anadai kwamba changamoto mojawapo ya ukuzaji wa Kiswahili kupitia sekta ya elimu inahusika sana hasa na ufundishaji kuliko njia za kisiasa na kiutamaduni. Hii inamaanisha kuwa Kiswahili bado kinakabiliwa na vikwazo kupitia njia ya ufundishaji na ujifunzaji katika sekta ya elimu. Kwa hivyo, madai ya kuanzisha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili shuleni yamepuuzwa mara kwa mara kwa misingi na madai ya kutokuwa na rasilimali ya kutosha. Kama ilivyodaiwa na Ssekamwa (2000) kwamba ilikuwa ghali kuzalisha walimu wenye ufasaha mzuri wa Kiswahili, na jinsi ilivyokuwa ikidaiwa kwamba hakukuwa na walimu wa kutosha, vitabu vya kiada, istilahi na vifaa vya kufundishia Kiswahili, hili ni jambo ambalo lilikanushwa kutokana na madai ya washiriki wa utafiti huu. Hakika, nadharia ya upangaji lugha ya Haugen inatoa hoja madhubuti ya ukuzaji wa lugha kwamba

utekelezaji na uendelezaji wa lugha yoyote utapata njia bora ya maendeleo kupitia sekta ya elimu.

Kama ilivyodaiwa na washiriki katika utafiti huu, serikali ilionekana kuwa na sera kuhusu utaratibu na kikomo cha ajira kila mwaka kwa sababu ya hofu ya gharama kubwa kupitia mishahara. Kwa hivyo suala hili limeathiri ukuzaji na ukuaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu kwani baadhi ya walimu wa Kiswahili huacha Kiswahili na kutafuta stadi za kufundisha masomo mengine yaliyo na soko kielimu.

5.4 Uhaba wa Vifaa na Rasilimali za Kufundishia na kujifunzia Kiswahili

Wakati wa mahojiano, ilibainika kwamba kulikuwa na uhaba wa fedha za kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika taasisi nyingi za kielimu. Washiriki walieleza kuwa hali hii ilisababisha mazingira duni ya kujifunzia. Kwa hivyo hili lilikuwa ni tishio kubwa kwa ukuaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Hata hivyo, ilibainika kuwa shule nyingi hasa za kibinafsi hazikuwa na uwezo wa kununua vitabu vya kutosha vya wanafunzi. Kwa hivyo, baadhi ya taasisi huchagua kutosajili wanafunzi wanaohitaji kusoma lugha ya Kiswahili na bodi ya mitihani ya kitaifa kwa vile si somo la lazima hasa kwenye kidato cha nne.

Pia, ilibainika kuwa kulikuwa na ukosefu wa muda wa kutosha kwenye ratiba za taasisi mbalimbali zilizokuwa zimeanzisha ufundishaji wa Kiswahili. Walijiuliza ni vipi lugha ya Kiswahili ingeendelezwa kama masomo mengine kwa mfano lugha ya Kiingereza iwapo haitapewa muda wa kutosha kwenye ratiba za shule na taasisi zinazohusika.

Nukuu 16

Kiingereza

.... yeah the curriculum support materials, that's where we still have a challenge as a country. Apparently, there are efforts being made to generate some, truly even some people have written some, but not

until the government buys them officially or distributes them officially to schools, shall this point hold water..... (IP3).

Kiswahili

Kuhusu vifaa vya kufundishia, hapo ndipo bado tuna changamoto kama nchi. Hata hivyo, juhudi za kuandaa na kuzalisha vifaa vinavyohitajika zinaendelea, hata kuna baadhi ya watu ambao wameandika vitabu lakini changamoto hii itasuluhishwa wakati serikali itakaponunua na kusambaza vitabu hivyo katika kila shule. (MT3),

Ilibainika pia kuwa kulikuwa na soko kidogo au hakukuwa na soko lolote wakati mwingine la vifaa vya Kiswahili. Jambo hili lilielezwa kuwa lilikuwa limeathiri upatikanaji wa miswada ya vifaa vya Kiswahili kwa vile waandishi wengi hawakuvutika kuingia katika tasnia hii. Kwa hivyo, hii pia ilijadiliwa kama sababu iliyoendelea kudhoofisha juhudi za kuandika na kutoa vitabu vya kurejelea vya Kiswahili.

Nukuu 17

Kiingereza

.... on our part as publishers, first of all, much as we have published some number of Kiswahili titles, the authors are also few to compete and produce quality work..., for us we have the interest to publish but you find that it is still a challenge.... Even when it comes to editing and proofreading, people to have that structure of how the book should look like, how should the content flow...we still lack the human resource, the authors in that direction... and also publishing is a business, so we put our coin where we know the dividend will also be high... why we have a few publications, there is little market, where are the people to buy them....(IP6).

Kiswahili

Kwa upande wetu sisi kama wachapishaji, hata ingawa tumechapisha baadhi ya vitabu vya Kiswahili, waandishi pia bado ni wachache. Sisi tungekuwa na hamu ya kuchapisha lakini upatikanaji wa miswada ya kuchapisha bado ni changamoto.... Aidha, wataalam ambao tunaweza kutumia katika kuhariri kazi za kiswahili ni wachache pia. Hata hivyo sisi tunawekeza tunakotarajia faida. Ukosefu wa soko la vitabu vya Kiswahili ndiyo sababu pia ya machapisho machache (MT6)

Kama ilivyodaiwa na Zell (2018) mustakabali wa ukuaji wa tasnia ya uandishi wa vitabu vya Kiswahili lazima uwe kujitolea na kujitegemea kwa waandishi na

wachapishaji licha ya vikwazo vya masuala ya kiuchumi na kisiasa. Kwa hivyo, waandishi pamoja na wachapishaji wa vitabu vya Kiswahili nchini Uganda, wanafaa kutia bidii na kujitolea kwa ajili ya kutoa mchango thabiti katika ukuaji wa Kiswahili. Hata hivyo, washiriki walidai kuwa kulikuwa na msaada mdogo kwa waandishi wazawa wa Uganda ambao walidhani inaweza kuwa sababu nyingine inayozuia kupatikana kwa vifaa vya kutosha vya rasilimali. Ilibainika kwamba kulikuwa na matumizi ya kazi za fasihi za kigeni ambayo haikuzingatia miktadha iliyo wazi ya nchini Uganda. Walisema kwamba iwapo kungekuwa na ununuzi wa vitabu vya kutosha vinavyozingatia muktadha wa Uganda, huenda wanafunzi wangevutika na kuongeza ari ya kusoma Kiswahili. Haya yote yalionekana kama vizuizi katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Maoni haya yamenukiliwa hivi:

Nukuu 18

Kiingereza

...more especially at secondary, the government has not bought enough teaching materials like books. Even those few that are provided, are for Kenyans and Tanzanians and some use high pitched language. Even when you feel you want to use a projector to teach, there are very few schools with projectors and even electricity especially in those rural areas. You find it very hard, you find there is an instructional material you want to use and you can't find it (ip 12)

Kiswahili

Kwenye ngazi ya sekondari, serikali haijanunua vifaa vya kurejelea vya kutosha kama vile, vitabu. Hata vile vichache vinavyopatikana, vimeandikwa na Wakenya na Watanzania na wametumia lugha ya kiwango cha juu. Hata ukitaka kutumia kifaa kama projekta kufundisha, ni vigumu kuipata, kuna shule chache sana zinazoweza kuwa na projekta au hata na umeme (MT 12)

Kama ilivyodaiwa na washiriki, uhaba wa vifaa vya kufundishia na rasilimali vilihatarisha ukuaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Washiriki walisisitizia mahitaji ya kuwepo kwa vitabu vya kurejelea na jinsi kungesaidia uendelezaji wa Kiswahili. Ingeonekana dhahiri kuwa vitabu vinapaswa kupatikana katika lugha zinazozungumzwa na idadi kubwa ya watu wa nchi au ukanda kwa

mfano lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, umakini mdogo hupewa uchapishaji wa lugha za asili kama hizi.

Katika nchi nyingi zinazoendelea za Afrika na kwingineko, vitabu vingi vinachapishwa kwa lugha za kigeni. Barani Afrika, vitabu vingi vinachapishwa kwa Kiingereza, Kifaransa, Kireno, au lugha nyingine ambazo si za Kiafrika (Ogechi & Bosire-Ogechi, 2002). Suala kama hili huzorotesha ukuaji na maendeleo ya lugha ya kienyeji kama lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, Zell (2018) anasisitiza kuwa kuchapisha kwa lugha za Kiafrika hutokea ingawa kwa nadra kwa sababu ni nyingi na watafsiri wanahitajika, mfumo wa maandishi wa baadhi ya lugha haujaendelezwa, pia ni ghali mno kuchapisha katika kila lugha. Aidha, serikali kutowekeza katika ununuzi wa vitabu vya kurejerea pamoja na ukosefu wa wasomi wa kazi mbalimbali ambazo zimechapishwa ni changamoto katika tasnia ya uchapishaji. Zaidi ya hilo, ilibainika pia kwamba mazoea au tabia ya usomaji wa vitabu vilivyochapishwa miongoni mwa Wanauganda, bado ilikuwa ya kiwango cha chini sana. Suala kama hili wakati mwingi limewavunja moyo waandishi wa lugha ya Kiswahili kushiriki kikamilifu katika uandishi na uchapishaji.

Kulingana na nadharia ya upangaji lugha ya Haugen, upangaji na ukuzaji wa lugha unahitaji shughuli za kuandaa na kutoa uandishi wa kawaida wa sarufi, kamusi, miongozo ya uakifishaji na matamshi kwa waandishi na wazungumzaji hasa kutoka jamii za wingi lugha. Uandishi na utayarishaji wa nyenzo kama hizo za lugha unaweza kuwa na athari kubwa katika kukuza na kuendeleza lugha kwa mfano Kiswahili katika muktadha wa Uganda. Hali hii inamaanisha kuwa siyo waendelezaji wa lugha tu wanaotabiri ufanisi wa lugha hiyo kulingana na maarifa yaliyoko, lakini ni juhudi za makusudi za utekelezaji wake (Haugen, 1959).

5.5 Mvutano Kati ya Lugha za Kiasili na Kiswahili

Washiriki wa utafiti huu walidai kuwa katika mazingira ya wingi lugha hasa Jijini Kampala na nchi nzima kwa ujumla, kuna ushindani kati ya lugha za makabila mbalimbali. Wengi wao waliendelea kusema kwamba kuna baadhi ya Wanauganda ambao mara kwa mara wameonekana kupinga uendelezaji wa Lugha ya Kiswahili wakihofia mabadiliko ya lugha zao kimatumizi. Suala hili lilielezwa kuwa tishio la ukuzaji wa Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Aidha, hata ingawa Kiswahili kimepewa hadhi rasmi ya lugha ya pili kikatiba, maoni ya washiriki wengi yalidokeza kwamba ni Wanauganda wachache tu ambao walikuwa tayari kujitolea kuunga mkono ukuzaji wa Kiswahili kwa kuhofia ufifiaji kimatumizi wa lugha zao za kiasili. Jambo hili lilionekana kama tishio kwa lugha za kienyeji hasa katika jimbo la katikati ambamo lugha ya Kiganda ndiyo eneolugha. Hata hivyo, ilifunuliwa kwamba dhana hii ya upendeleaji wa ukuzaji wa lugha za kiasili dhidi ya Kiswahili inahamishwa kutoka kwa wazazi kwenda kwa wanafunzi katika taasisi nyingi na hasa katika wilaya za jimbo la katikati. Waliamini kuwa maoni haya bado yanazuia kukubalika kwa lugha hiyo kati ya wanafunzi na idadi kubwa ya watu wengine. Suala hili limesababisha ukosefu wa utetezi kwa lugha ya Kiswahili nchini Uganda kwa vile haina kabila lolote linalojitokeza kuunga mkono ukuaji na ukuzaji wake. Kwa hivyo, ndiyo sababu watu wengi bado wanahisi kuwa Kiswahili ni lugha ya kigeni ambayo wanalazimishwa kuzungumza. Wengi pia walifunua kwamba Wanauganda wengi hudai kwamba tayari wana lugha ya Kiingereza inayowawezesha kuzungumza na watu kutoka makabila mbalimbali, kwa hivyo kuongezewa lugha nyingine isiyo na asili dhahiri ya kikabila itapata vikwazo kukubalika kabisa na jamii mbalimbali hasa Kampala ambapo Kiganda kinajulikana na kuzungumzwa na wengi.

Ilibainika pia kwamba maoni haya siyo ya hivi karibuni tu lakini yameanza hata wakati wa kabla ya ukoloni, wakati Kiswahili kilipohusishwa na Uislamu na kuchukuliwa kama tishio kwa lugha asili za Kiafrika, utamaduni na Ukristo. Washiriki walielezea kwamba watu wengi wana uzalendo wa kikabila unaowafanya kutetea wazi lugha zao za kiasili. Kwa hivyo, wanafunzi waliokwisha ambukizwa kwa fikra au hisia kama hizi, wanaona ni vigumu sana kukubali kujifunza lugha ya Kiswahili badala ya lugha yao ya asili. Maoni haya yanadhihirishwa kama ifuatavyo:

Nukuu 19

Kiingereza

... I want to call it ethnic patriotism... there are some ethnic communities that feel that are well placed and therefore they want to advocate for their languages and therefore, this promotes tribalism. And the very essence of Kiswahili presence is to fight that and the fighting is always backed up by the mindset (IP3).

Kiswahili

... Ninataka kuuita uzalendo wa kikabila... kuna baadhi ya jamii ambazo hudai hadhi ya juu kuliko jamii nyingine. Kwa hivyo, jamii hizo hupendelea kupigania na kutetea lugha zao, jambo ambalo hupalilia ukabila. Wakati mwingine hicho ndicho chanzo cha mtazamo hasi miongoni mwa wanajamii kwa kufikiria kwamba kuwepo kwa Kiswahili kutaathiri lugha za jamii zao (MT 3)

Nukuu 20

Kiingereza

.....the mother tongue influence. They want to relate everything with their language which becomes a major challenge to Kiswahili and its implementation...you will even hear some of the top administrators saying that it is a language for thieves...how do you teach a language for thieves? “Kabasome oluganda lwaabwe”. So, that attitude and bias, has affected Kiswahili a lot (1p 10).

Kiswahili

....athari ya lugha mama. Wakati mwingi, wanataka kuhusisha kila kitu na lugha yao. Jambo hili linakuwa changamoto kwa Kiswahili na utekelezaji wake... Hata baadhi ya viongozi wakuu wa shule husikika wakisema kwamba Kiswahili ni lugha ya wezi. ... “unawezaje kufundisha lugha ya wezi? Kabasome oluganda lwaabwe”.(Eti wanafaa kusoma lugha yao ya kienyeji). Kwa hivyo, mtazamo hasi kama huo, umeathiri Kiswahili sana. (1p 10)

Lugha huchangia katika uundaji wa utambulisho wa kikabila kwa misingi ya kijamii na kisaikolojia. Ukabila wakati mwingine ni nguzo katika ujenzi wa jamii unaoendeleza ushirikiano miongoni mwa kikundi fulani ambacho kawaida huwa na watu wachache nchini (Awuor, 2019). Watu wa kabila moja huwa na baadhi ya sifa bainifu za kitamaduni zilizo sawa kama vile, lugha yao. Kwa hivyo, uhusiano kati ya lugha na kabila hutegemea lugha inayotumika katika jamii yaani ile ya kiasili. Kuna utata sana katika masuala ya elimu na lugha katika nchi nyingi za barani Afrika kwa sababu ya hali ya makabila mengi na lugha nyingi.

Aidha, hali inakuwa mbaya zaidi wakati lugha rasmi ya taifa hilo ikiwa ni tofauti na lugha yoyote ya asili. Kuna mjadala mkubwa wakati mwingi juu ya lugha gani ya kutumia shuleni hasa katika ngazi za chini za elimu ya msingi katika jamii za wingi lugha (Owu-Ewie, 2006). Mashindano ya lugha za kikabila yana mizizi katika enzi za kabla ya ukoloni. Kabla ya ujio wa utawala wa kikoloni, hakukuwa na sera dhahiri za lugha isipokuwa katika maeneo yaliyotawaliwa na Uislamu au na wakristo kwa upande wa Ethiopia. Kabla ya kugawanywa kwa Afrika mnamo miaka ya 1880 na kuja kwa wakoloni, hakukuwa na mipaka wazi iliyogawanya vikundi vya lugha za kikabila barani Afrika. Badala yake, mgawanyiko wa kikabila ulitokana na makazi ya watu, mara nyingi waliokaa sehemu fulani na kuhamahama. Hata hivyo, katika hali nyingi mgawanyiko huo uliwekwa na maumbile ya mazingira au hali asili za kijiografia (Abdulaziz, 1991). Licha ya hali hii ya wingi lugha, mawasiliano yalikuwepo kupitia ushirikiano wa kijamii, kiuchumi na katika masuala ya kiulinzi na kijeshi. Hali hii iliwezesha mawasiliano na kukuza watu wenye uwezo wa kuwasiliana kwa lugha nyingi.

Ugawanyaji wa Afrika uliunda mipaka ya kijiografia ambayo ilipuuza kabisa hali halisi ya kuingiliana na kushirikiana kwa jamiilugha mbalimbali. Kwa mfano, kuna

baadhi ya maeneo kama Kameruni yenye lugha zaidi ya 100, huku kukiwa na nchi nyingine zilizo na lugha moja, kama vile Botswana, Burundi, Lesotho, Rwanda, Somalia, na Swaziland. Hata hivyo, katika nchi hizi, watu binafsi wanaweza kuwa na uwezo wa kuzungumza lugha nyingi, pamoja na angalau lugha moja ya Kiafrika au ya kimataifa. Kwa hivyo, suala la utambulisho wa kitamaduni unaweza kuangaliwa katika viwango mbalimbali. Kama vile, kiwango cha kikabila ambacho ni kiwango cha lugha za mama, kiwango cha jamii ambacho pia kinazingatia lugha za jamii, kiwango cha kitaifa ambacho ni kiwango cha lugha za kitaifa pamoja na kiwango cha kikanda yaani utamaduni wa Kiafrika kama lugha za kimaeneo kama vile, Kiswahili (Fyle, 2003).

Badala yake, nadharia ya Haugen ya upangaji lugha (1966,1983) inabainisha kwamba jukumu la lugha linapaswa kuwa wazi likijihusisha na lengo la umoja katika jamii, taifa, kikundi cha kidini, kikundi cha kisiasa, au aina nyingine za vikundi, lengo la kisasa, ustadi au demokrasia. Kwa hivyo, katika utekelezaji wa sera ya lugha katika elimu, ujifunzaji wa lugha ya pili usisababishe kupotea kwa lugha ya kwanza bali ni uendelezaji wa lugha zote mbili (Kembo-Sure, Mwangi, S., & Ogechi, N. (Eds.) (2006).

5.6 Mtazamo hasi kwa Kiswahili

Asilimia sitini na mbili (62%) ya washiriki walielezea kuwa mtazamo hasi kwa lugha ya Kiswahili bado unaathiri ukuzaji wake kupitia sekta ya elimu nchini Uganda. Baadhi ya walimu katika utafiti huu walionyesha kwamba kulikuwa na mtazamo hasi miongoni mwa baadhi ya wanafunzi, wazazi, wafanyikazi na hata wasimamizi kuhusu lugha ya Kiswahili katika taasisi nyingi za elimu. Walibaini kuwa kuna hata baadhi ya wazazi wanaowakatisha tamaa watoto wao kwa kuwaambia kuwa lugha hiyo haitawapeleka popote. Jambo hili linafanya wanafunzi kupoteza ari ya kujifunza

Kiswahili na hivyo kuishia kuacha somo. Isitoshe, ilibainika pia kuwa baadhi ya wasimamizi katika baadhi ya taasisi hupuuza somo la lugha ya Kiswahili na huichukulia kama lugha ya kienyeji. Kwa hivyo, huitengea muda mdogo kwenye ratiba za shule au wakati mwingine huifuta kabisa. Washiriki walihusisha hali hii na ukosefu wa uhamasishaji juu ya thamani na fursa za lugha ya Kiswahili.

Washiriki katika utafiti pia walifunua kwamba kulikuwa na uhusishaji wa lugha ya Kiswahili na ukatili wa tawala za Kihistoria kama vile katika enzi za dikteta Iddi Amini ambapo wanadai kwamba Kiswahili kilitumika kunyanyasa watu. Mitazamo kama hii bado inaleta upinzani kutoka kwa wadau wengi wa elimu. Hali hii imeweka mazingira magumu ya Kiswahili kuendelezwa shuleni na hata katika jamii wanakotokea wanafunzi. Hata hivyo, walimu walidokeza kwamba kulikuwa na athari za kitamaduni katika sera za shule kuhusu lugha ya Kiswahili hasa katika baadhi ya shule zilizojengwa kwa misingi ya baadhi ya falme nchini Uganda.

Mbali na sera ya elimu kwamba lugha ya eneo husika inafaa kutumika kufundishia kuanzia elimu ya awali hadi darasa la tatu, ilibainika kuwa kulikuwa na baadhi ya wazazi pamoja na baadhi ya viongozi wa shule mbalimbali ambao walipendelea sana watoto kujifunza lugha ya eneo husika badala ya Kiswahili hata kwenye ngazi za elimu ya juu. Ilikuwa bayana katika mahojiano kwamba kulikuwa na upendeleo wa lugha ya kimkoa dhidi ya Kiswahili. Kulingana na mazingira ya eneo la utafiti, lugha ya Kiganda ilipendekezwa zaidi kufundishwa katika shule za eneo hilo kwa vile ndiyo lugha ya eneo. Maoni haya yameonyeshwa katika nukuu zifuatazo:

Nukuu 21

Kiingereza

The mindset of the older generations in office some of them still cling on the earlier mindset which is not informed..... you know the history of Kiswahili in this country right away from the 1940s and all the forces that have been fighting it. So the mindset had been

hinged from the historical perspective more so during Iddi Amini Dada's misuse of the language. But people forget that it was not the language but it was people, so ethnic patriotism sometimes rides on that and some of these people are well placed, some of these cultural institutions are strongly placed in this country. So when few people are against Kiswahili on the basis of ethnic patriotism, of course it affects it.... but now that mindset is slowly fading, that's why Kiswahili is picking up (IP3).

Kiswahili

Kuna baadhi ya maafisa ambao bado wana fikra potovu kuhusu historia ya Kiswahili hasa kilipotumika vibaya katika nyakati za utawala wa Idd Amin Dada. Hata hivyo, baadhi yao husahau kwamba siyo lugha iliyotenda ila ni watu waliotenda chochote kilichotendeka. Kwa hivyo uzalendo wa kikabila wakati mwingine huendelezwa na fikra potovu kama hizo na baadhi ya makabila hudai hadhi za juu kuliko makabila mengine, jambo ambalo linaathiri maendeleo ya Kiswahili. Kwa hivyo, iwapo kutatokea baadhi ya watu watakaopinga Kiswahili kwa misingi ya uzalendo wa kikabila, bila shaka hili litaathiri Kiswahili. Hata hivyo, kwa sasa mawazo hayo yameanza kufifia polepole, na ndiyo maana Kiswahili kimeanza kuendelezwa (MT 3)

Nukuu 22

Kiingereza

The challenge I face while teaching Kiswahili is the negative attitude by the learners vile vile na wazazi..... Actually some parents tell their children that Kiswahili is not important in Uganda and it will not take them anywhere. ...even some teachers of other subjects, they don't value Kiswahili. For example, they come and teach in your lesson) saying after all Kiswahili is not important in Uganda. (ip10).

Kiswahili

Changamoto ninayokumbana nayo wakati wa kufundisha Kiswahili ni mtazamo hasi wa wanafunzi pamoja na wazazi Hata kuna baadhi ya wazazi ambao huwaambia watoto wao kuwa lugha ya Kiswahili si muhimu nchini Uganda na haitawapeleka kokote... Hata walimu wa masomo mengine, hawathamini Kiswahili. Kwa mfano, kuna wakati ambapo wanaingilia muda wa Kiswahili kwenye ratiba kimaksudi wakidai kwamba Kiswahili si muhimu nchini Uganda. (MT 10)

Nafasi ya lugha za Kiafrika katika elimu, afya, uchumi na utawala huhusiana na mtazamo wa kihistoria, kijamii, nguvu za kisiasa na kiuchumi kwa kuunda mipango na sera za lugha. Sera za lugha zinapaswa kujengwa kwa misingi ya mifumo iliyopo ya matumizi ya lugha na mitazamo kuhusu lugha katika jamii zinazohusika (Djite,

2008: Igboanusi, 2010). Baadhi ya juhudi za kueneza na kukuza lugha ya Kiswahili zimekuwepo ingawa mtazamo hasi kuhusu lugha umekuwa ni kikwazo. Suala la mitazamo kuhusu lugha juu ya uchaguzi wa lugha, maendeleo na sera katika jamii za wingi lugha halifai kupuuzwa (Adegbija, 1994; Batibo, 2005). Wazungumzaji wa lugha moja huwa na mtazamo mmoja tu kwa lugha yao kwa sababu hawana lugha nyingine ya kulinganisha na yao. Hata hivyo, katika jamii zenye lugha mbili au zaidi, kuna tabia ya kukuza mitazamo tofauti kwa kila lugha inayotumika pale.

Mitazamo hii, iwe chanya au hasi, hutegemea kiwango cha thamani ya kila lugha kijamii na kiuchumi. Nchini Uganda, lugha ya Kiganda ambayo ndiyo lugha ya mawasiliano katika mji mkuu wa Kampala, inaonekana kuwa wengi ndiyo lugha wanayopendelea kuzungumza. Hali hii inalingana na jinsi washiriki wengi walibaini kuwa wadau wengi kama wazazi, wanafunzi na walimu walipendelea watoto kujifunza lugha ya eneo ambayo ni Kiganda badala ya Kiswahili. Katika majibu mengi, ilionekana kuwa lugha ya Kiganda ilikuwa na upendeleo wa kieneo kama lugha ya watu wa eneo hilo na hali sivyo ilivyokuwa kuhusu Kiswahili. Aidha, Ssekamwa (2000: 134) anasisitiza kuwa sababu kuu mojawapo ya kupinga Kiswahili ni pamoja na kuihusisha lugha ya Kiswahili na dini ya Kiislamu ambayo wafuasi wake, hasa Waarabu, waliendeleza shughuli za utumwa ambazo zilionekana kuwa si za kidini na zilikashifiwa na wamishonari wa Kikristo. Hata hivyo nchini Uganda, ni vigumu kupendelea lugha moja asili kutoka kwa zingine kuunganisha vikundi vya tamaduni mbalimbali na kutumika kama lugha ya kitaifa na lugha ya kufundishia shuleni.

Changamoto zilizojadiliwa zinadhihirishwa katika kielelezo 5.1 kifuatacho:



Kielelezo 5.1 Changamoto zinazokabili maendeleo ya Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda

Kielelezo hicho hapo juu kinaonyesha changamoto kama zilivyofafanuliwa na washiriki zilizoathiri ukuaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda.

5.7 Muhtasari wa Sura

Sura hii imejadili matokeo ya utafiti wa sera ya lugha katika mfumo wa elimu na athari zake katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Hasa, data imewasilishwa juu ya changamoto zinazokabili maendeleo ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda.

SURA YA SITA

SULUHU ZA CHANGAMOTO ZINAZOKUMBA UKUAJI WA KISWAHILI

KUPITIA SEKTA YA ELIMU NCHINI UGANDA

6.0 Utangulizi

Katika sura hii, data zilizokusanywa zilijibu swali: Ni masuluhisho yapi yanayoweza kutatua changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu? Jumla ya washiriki 13 walichaguliwa kimaksudi na kuhojiwa katika utafiti huu. Hawa walikuwa watunzi wa sera, waratibu na watekelezaji wa sera za lugha. Katika sura hii pia, mtafiti alitumia nambari na misimbo badala ya majina ya washiriki na shule ili kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya kimaadili kama usiri, faragha, na kutokujulikana. Aidha, mtafiti aliwasilisha na kujadili matokeo ya lengo la tatu ambalo lilijikita katika kufafanua suluhu za changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu.

6.1 Uhamasishaji wa Kijumla

Washiriki wa utafiti huu walipendekeza uhamasishaji kwa watu wengi juu ya manufaa ya lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Aidha, shughuli hii ingebadilisha mtazamo hasi walionao watu wengi kuhusu lugha ya Kiswahili. Washiriki walielezea kuwa itakuwa muhimu sana kwa raia kutambua fursa zinazoweza kupatikana kutokana na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kitaifa, kikanda na kimataifa. Shughuli hii pia ingebadilisha maoni ya watu juu ya lugha hii inayochukuliwa kama tishio kwa lugha zao za kienyeji. Washiriki pia walibaini kuwa lazima kuwekwe juhudi za kufundisha wanajamii lugha ya Kiswahili ili kueneza uelewaji na uzungumzaji wake katika jamii.

Zaidi ya hayo, washiriki walipendekeza kwamba taasisi zote za kujifunzia zinapaswa kuwa na mazingira yenye maandishi ya Kiswahili kote uani ili kuongeza uzoefu wa

lugha hiyo kwa wanafunzi. Walitabiri mabadiliko chanya kwa wanafunzi iwapo uhamasisaji kwa wengi utafanyika, jambo hili lingeongeza idadi ya wanafunzi walio na ari ya kusoma lugha hiyo katika taasisi mbalimbali. Aidha, washiriki walipendekeza kuwa vyombo vya habari virushe vipindi vya Kiswahili hewani hasa vile vinavyojihusisha na elimu pamoja na kuchapisha makala muhimu ya kielimu kwa ajili ya kutoa mchango wa uenezaji wa Kiswahili. Hoja hii ilielezwa hivi:

Nukuu 23

Kiingereza

If the students changed the attitude, and had that good attitude of Kiswahili going to take them to another step, they can also look beyond being employed. Apart from employment if I had Kiswahili, would it help me to reach somewhere? If I went to Tanzania if I went to Kenya if I went to Rwanda with my Kiswahili, could it help me to do something and earn a living, so we should look beyond being employed by the government and to go to teach in the school, so sensitization, to sensitize those students and the parents, so that they can have that attitude which is positive. That would be number one... I think we have to use the media as much as we can and we talk about Kiswahili...(IP4).

Kiswahili

Iwapo wanafunzi wangepadilisha mtazamo hasi na kuwa na mtazamo chanya kuhusu Kiswahili, wangetambua manufaa mengine ya Kiswahili katika mawanda mbalimbali isipokuwa kuajiriwa tu kufundisha Kiswahili. Mtu anafaa ajiulize, kwamba iwapo atasafiri nje ya nchi kwa mfano katika nchi kama Tanzania, Kenya au Rwanda, Kiswahili chake kinaweza kumsaidia kwa njia yoyote? Kwa hivyo wanafunzi pamoja na wazazi wanapaswa kuhamasishwa ili kuangalia zaidi ya kuajiriwa na serikali kufundisha Kiswahili shuleni ili waweze kuwa na mtazamo mzuri. Vyombo vya habari pia vinafaa kutumika iwezekanavyo ili kusambaza uhamasishaji juu ya Kiswahili... (MT 4)

Nukuu 24

Kiingereza

We need to sensitize and bring on board all sectors. We are just focusing this on education but education is just one component, you will find out that there are those other supporting institutions that would also support Kiswahili in education sector. If we only look at education, what about these other domains, if we don't have Kiswahili in the publishing houses, media, if we don't use Kiswahili in our communities, if Kiswahili is not in the court, judicially, the

parliament its self that legislates doesn't use Kiswahili, then to me the challenges are still very many because we shall not achieve only in education when there are those other factors because they work hand in hand and education cannot live in isolation. We must involve the cultural leaders, we must involve the church and mosques, in order to make sure that Kiswahili in Education also takes root. (ip 11).

Kiswahili

Tunahitaji kuhamasisha kila mtu katika kila sekta. Tunajikita tu katika elimu lakini elimu ni njia moja tu. Kuna taasisi zingine ambazo pia zingesaidia Kiswahili kukua katika sekta ya elimu. Ikiwa tunaangalia tu elimu, vipi katika mawanda mengine? Ikiwa hatuna Kiswahili katika kampuni za uchapishaji, vyombo vya habari, ikiwa hatutumii Kiswahili katika jamii zetu, ikiwa Kiswahili hakipo mahakamani, bungeni, basi kwangu mimi changamoto bado ninaona ni nyingi sana kwa sababu hatutafanikiwa katika elimu tu. Lazima tuwashirikishe viongozi wa kitamaduni, lazima tuhusishe kanisa na misikiti, ili kuhakikisha kuwa Kiswahili katika Elimu pia kinakua. (MT 11)

Wanajamii pamoja na watu wa shuleni wanahitaji kuhamasishwa kwa ajili ya kujenga umoja wa taifa. Kama inavyodaiwa na wasomi wengi kwamba Kiswahili ndiyo lugha pekee ya Kiafrika ambayo haijikusishi wala kudaiwa kumilikiwa na kabila lolote katika bara la Afrika, kuna haja ya kuendeleza lugha moja tu ya Kiafrika kama lugha ya Kiswahili inayoweza kuwaunganisha watu wa Afrika (Pawliková-Vilhanová, 1996; Jjingo, 2011). Hali hii ya kukipa Kiswahili hadhi ya kiwango cha bara imetokana na juhudi, ushawishi na uhamasishaji unaofanywa na wanaisimu pamoja na wasomi wa lugha barani Afrika ambao wanaona kuwa ni aibu ya kutokuwa na lugha ya Kiafrika ya mawasiliano mapana barani (Mukuthuria, 2006).

Kutokana na madai haya, kuna haja ya kuhamasisha wadau na wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wa kufundisha lugha za asili katika mtaala uliopendekezwa ambao unatoa msingi na fursa ya ukuzaji wa Kiswahili. Kuwa na lugha ya kiasili kama Kiswahili kungechangia ukuzaji wa umoja miongoni mwa raia wa Uganda kama inavyodaiwa na nadharia ya upangaji lugha ya Haugen (1966,1983) kwamba malengo ya kukuza lugha yanapaswa kuwa wazi na yanayohusiana na lengo la kuendeleza

umoja katika jamii. Haya ni matokeo yanayowezekana ya lugha ya Kiswahili pindi ikiendelezwa nchini Uganda. Haugen anadokeza zaidi kuwa ili lugha ikue, inahimizwa kuendelezwa kupitia magazeti, uandishi wa vitabu vya kiada, na machapisho mengine pamoja na kupitia katika vyombo vya habari ili kuhamasisha jamii kwa ukamilifu juu ya lugha hiyo (Haugen, 1966).

6.2 Kozi za Uboreshaji wa Stadi za Ufundishaji kwa walimu wa Kiswahili

Hili ni suala muhimu pia ambalo lilitokana na mawasilisho ya washiriki. Hawa walipendekeza kwamba kunafaa kuweco na uendelezaji wa mafundisho ya uboreshaji wa mbinu za kufundishia kwa walimu wa Kiswahili kote nchini. Washiriki walitumai kuwa shughuli hii italeta maendeleo makubwa katika mchakato wa ukuzaji wa Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Shughuli hii pia ingechangia kutupilia mbali madai ya kusema kwamba idadi ya walimu haitoshi.

Aidha, washiriki walitumai kuwa kozi za aina hizi zingetoa fursa za kuwahudumia walimu katika kubadilishana mawazo na kuongeza uzoefu pamoja na kujifunza kutoka kwa wenzao. Hata hivyo, hili lingekuwa tena jukwaa la kujitathmini kama walimu wa Kiswahili kuhusu maendeleo ya mafunzo nyanjani pamoja na tathmini, matumizi ya mbinu mpya zinazoibuka kama vile teknolojia katika mafunzo ya Kiswahili pamoja na kuzungumzia mambo mengine ya kiusomi yanayohusu Kiswahili. Hisia na maoni hayo yalielezwa hivi:

Nukuu 25

Kiingereza

In 2011, NCDC started on retooling of Kiswahili teachers in Nakaseke Core Primary Teachers College, this was a very good move. But after retooling of those teachers, Kiswahili was not rolled out at primary level. Why did they waste all the money and time? Refresher courses are good because teachers will be updated on better skills and methods they can use while teaching. Even there are some workshops every year organized by CHAKITAU that teachers

meet and go through a number of ideas concerning Kiswahili teaching (IP 10).

Kiswahili

Mnamo mwaka wa 2011, NCDC ilianza kuwapa mafunzo ya kuwaimarisha na kuwarudisha upya walimu wa Kiswahili katika Chuo cha walimu wa shule za msingi cha Nakaseke, hii ilikuwa ni hatua nzuri sana. Lakini baada ya shughuli hiyo, Kiswahili hakikuanzishwa katika shule za msingi. Swali balagha ni; Kwa nini walipoteza pesa na wakati huo wote? Warsha za kozi kama hizo ni nzuri kwa sababu walimu hupewa ujuzi bora na mbinu faafu ambazo wanaweza kutumia wakati wa kufundisha. Hata kuna warsha kadhaa kila mwaka zinazoandaliwa na CHAKITAU pamoja na vyama vingine vinavyounganisha walimu wa Kiswahili kimaeneo ambazo walimu hukutana, huzungumzia na kujadiliana juu ya ufundishaji wa Kiswahili (MT 10)

Kama ilivyopendekezwa na washiriki, kuna haja ya kuwekeza katika walimu kwa kuwatayarisha kikamilifu ili waweze kutekeleza kazi ya ufundishaji ipasavyo. Bolman na Deal (2003:129) wanabainisha kuwa mashirika mengi yaliyofanikiwa yamejikita katika njia za ubunifu za kusawazisha mahitaji ya mtu binafsi na ya shirika. Yote haya yanaonyesha dhana kuu ya mfumo wa rasilimali watu kwa kutazama nguvukazi kama uwekezaji badala ya gharama.

Ukuzaji wa rasilimali watu ni muhimu sana katika kufanikisha shughuli au programu yoyote. Hii itajumuisha marudio ya mafunzo kwa walimu katika matumizi na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha, walimu wanahitaji kuwezesha katika kuandaa vifaa vya kurejelea katika ufundishaji (Owu-Ewie, 2006).

6.3 Uundaji wa Baraza la Kitaifa la Kiswahili

Uundaji wa baraza la kitaifa la Kiswahili ulifikiriwa kama mkakati mwingine wa shughuli muhimu ya kuongeza ueneaji na ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Pamoja na nchi wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutia saina mkataba wa kuwa na Kiswahili kama lugha ya mawasiliano kikanda, ilipendekezwa kuwa nchi zote za Afrika Mashariki zianzishie mabaraza ya kitaifa ya Kiswahili ili kuongoza na kuendeleza ukuaji wa Kiswahili. Kwa hivyo, washiriki walifunua kwamba baraza

litasimamia shughuli za Kiswahili na kujaribu kushinikiza serikali kutatua baadhi ya changamoto zilizokabili Kiswahili wakati huo.

Nukuu 26

Kiingereza

... some coordination has been lacking and we say, that's why we are saying we need an institution precisely meant for coordination for development, planning of Kiswahili. So that it can even advise government on the technical steps it takes and that is the establishment of the Kiswahili council (IP 1).

Kiswahili

... Uratibu fulani umekosekana na ndiyo sababu tunasema tunahitaji taasisi yenye jukumu la kuratibu maendeleo na upangaji wa Kiswahili. Hata hivyo, chombo au taasisi hii iweze kuishauri serikali juu ya hatua zinafaa kuchukuliwa. Kwa hivyo, kunahitajika kuanzishwa kwa baraza la Kiswahili (MT 1)

Ilipendekezwa zaidi kuwa kunafaa kuwekwa mikakati ya kuhakikisha ushirika wa kisiasa wa Afrika Mashariki ambao unadhaniwa kuondoa vikwazo vya kuvuka mipaka kwa raia wa nchi za Afrika Mashariki. Suala hili lingewezesha urahisishaji katika kuvuka mipaka na kuhakikisha mwingiliano wa watu, jambo ambalo lingechangia ukuaji wa Kiswahili.

Nukuu 27

Kiingereza

I think some people do not interact well with Kiswahili language. This could be limited by lack of enough movement across borders to interact with people who have used Kiswahili for a long time. You know it is not very easy to cross borders, so our learners for example will not understand situations where Kiswahili is a mass language. Governments can agree and ease easy cross border movement (IP12).

Kiswahili

Nadhani watu wengi hawajatangamana vizuri na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Ninafikiri hii ni kwa sababu wengi hawana fursa ya kuvuka mipaka kuingiliana na watu katika nchi ambako Kiswahili huzungumzwa sana. Kwa hivyo, wanafunzi wetu hawatatambua mikutadha tofauti ambamo Kiswahili hutumika. Serikali za Afrika Mashariki zinaweza kukubaliana na kupunguza viziwi vya mipakani ili kuendeleza mtangamano na mshikamano (MT12)

Owu-Ewie (2006) anapendekeza hatua mojawapo muhimu katika kuhakikisha mafanikio ya shughuli au programu yoyote kuwa ni ufuatiliaji au usimamizi na tathmini. Hii itahusisha wadau wote katika shughuli na kwa mbinu inayomshirikisha kila mtu. Kwa mfano kwenye kiwango cha shule, kunafaa kuwa na kamati ya lugha na mratibu ambaye atasimamia na kufuatilia masuala ya lugha shuleni. Jukumu lake pia linafaa kuwa ni kuhakikisha kuwa shida za lugha zinatatuliwa, na pia kusaidia walimu katika kutengeneza vifaa na nyenzo zinazofaa. Mratibu wa lugha hutumika kama mshauri kwa walimu kulingana na matumizi ya lugha shuleni.

Owu-Ewie (2006) anaendelea kupendekeza kwamba pia kunafaa kuweko na waratibu wa lugha wa wilaya na mkoa ambao watasimamia na kufuatilia ufundishaji wa lugha katika ngazi za wilaya na mkoa mtawaliwa. Mratibu wa mkoa huongoza Bodi ya Ushauri ya Lugha ya Mkoa ambayo inashughulikia masuala ya lugha katika mkoa huo. Katika ngazi ya kitaifa, kuwe na Bodi ya Kitaifa ya Ushauri wa Lugha juu ya elimu ambayo itashauri wizara ya elimu juu ya masuala yanayohusiana na sera ya lugha ya elimu. Katika ngazi ya serikali kuwe na Baraza la Kitaifa la Lugha ambalo litashauri serikali juu ya upangaji lugha na utekelezaji wa sera. Wizara husika ishirikiane na Bodi ya Kitaifa ya Ushauri wa Lugha kuanzisha sheria ambazo zitaimarisha na kulinda matumizi ya lugha za kiasili au lugha husika katika elimu na nchini.

Imebainishwa wazi na watungaji pamoja na watekelezaji wa sera kwamba, serikali ya Uganda ina ari ya kuwezesha na kukuza lugha za asili, kuanzisha na kuwezesha uundaji wa kamati za lugha ya Kiswahili, Baraza la Kitaifa la Kiswahili, kuhamasisha kwa ajili ya kubadilisha mitazamo hasi ya watu kuhusu Kiswahili kupitia kwa mawanda ya elimu na programu nyingine za kitaifa kwa lengo la ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili (Jingo, 2011).

6.4 Kuweka Mkazo kwenye Utekelezaji wa Matamko ya Sera kuhusu Lugha ya Kiswahili

Washiriki wa utafiti huu walipendekeza kwamba serikali na wadau wengine wanapaswa kutafuta njia mbadala za kuongeza juhudi za utekelezaji wa sera ya lugha ya Kiswahili hasa katika mfumo wa elimu. Walipendekeza utunzi wa sera ya lugha iliyo wazi zaidi hasa sera ya lugha ya Kiswahili. Suala hili lingefafanua wazi matumizi, miktadha na shughuli ambazo zinaweza kuongoza ukuaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Walipendekeza pia kwamba serikali na wizara ya elimu inapaswa kuweka wazi sera ambayo ingefanya Kiswahili kuwa somo la lazima katika ngazi zote za elimu. Walipendekeza zaidi kuwa ufundishaji wa Kiswahili unapaswa kuanza katika kiwango cha elimu ya msingi jambo ambalo litawapa wanafunzi hamasa na ari ya kuendelea kusoma Kiswahili. Aidha, sera kuhusu ajira zinafaa kurekebisha ili kutosheleza fursa sawa za ajira kwa walimu wa masomo yote. Washiriki walibaini kuwa yote yaliyotajwa hapo juu yangehitaji utashi na umakini wa kisiasa kwa kuanzisha sera wazi na dhahiri ya lugha ya Kiswahili.

Nukuu 28

Kiingereza

I know there are private institutions, the religious institutions like private schools like other people who would be willing to render like the development of Kiswahili in collaboration with government but what is important about Kiswahili about the government that it needs to make the policy clear and then if the policy is clear, it can call up the collaboration of other stakeholders like media houses all those people would be willing but the government has not been clear to them that this is what we want (IP1).

Kiswahili

Ninajua kuna taasisi za kibinafsi, taasisi za kidini, shule za kibinafsi na hata watu wengine ambao wangukuwa tayari kutoa mchango katika maendeleo ya Kiswahili kwa kushirikiana na serikali. Jambo muhimu linalohitajika ni serikali kuweka sera wazi. Iwapo sera itakuwa wazi, itapata ushirikiano wa vyombo vya habari na wadau wengine. Serikali inafaa kutamka wazi kuhusu jambo lenyewe inalotaka (MT1)

Nukuu 29

Kiingereza

...so we need a strong policy, then they actually follow it up and make sure that it works and not to remain on paper like that yeah, because we really need to move with this integration of EAC (IP 2).

Kiswahili

...kwa hivyo tunahitaji sera madhubuti, kisha waifuatilie na kuhakikisha kuwa imetekelezwa na siyo kubaki kwenye karatasi kama vile hali ilivyo kwa sasa, kwa sababu tunahitaji sana kusonga na jumuiya ya Afrika Mashariki. (MT2)

Nukuu 30

Kiingereza

.... for it to take root, we should start with primary. Yet in primary, much as the teachers are trained, the schools are not teaching Kiswahili,so there should be a policy enforcing the teaching of Kiswahili in the primary curriculum.... there needs to be an implementation strategy that focuses on teacher recruitment for the lower levels, that focuses on standards and policies (IP8).

Kiswahili

...ili Kiswahili kuendelea, kinafaa kuanzishwa katika shule za msingi. Hata ingawa walimu wa shule za msingi wamefunzwa, Kiswahili hakifundishwi kwenye ngazi hiyo,... Kwa hivyo, kunafaa kuwe na sera inayolazimisha ufundishaji wa Kiswahili katika mtaala wa shule za msingi.... kuna haja ya kuwa na mkakati wa utekelezaji ambao unazingatia ajira kwa walimu wa elimu ya msingi.(MT 8)

Utekelezaji kikamilifu wa matamko ya sera kuhusu Kiswahili hasa katika sekta ya elimu unaweza kuhakikisha ukuaji wa Kiswahili. Kama ilivyojadiliwa hapo juu, uundaji wa sera madhubuti katika elimu rasmi ni hatua bora ambayo karibu nchi zote za Kiafrika hasa Uganda zingehitaji. Baadhi ya nchi zimefanya maendeleo, ingawa nyingine nyingi bado hazijaanza hatua zozote kwa sababu ya visingizio vya gharama na ukosefu wa utaalamu pamoja na madai ya hadhi kwa baadhi ya lugha. Haya yote yanazuia uundaji na utekelezaji wa sera yoyote bora ya lugha. Kuhusiana na gharama, miaka kadhaa iliyopita, Umoja wa mataifa ya Afrika (OAU) ulijaribu kutafuta njia ya kupima gharama ya ufundishaji wa lugha ya mama au lugha ya jamii. Iwapo gharama itaweza kuthibitishwa, bila shaka itaamsha ari ya mataifa yenyewe mbalimbali

pamoja na ufadhili kutoka kwa mashirika mbalimbali na hivyo kupata msaada wa kuendeleza matumizi ya lugha za Kiafrika katika elimu. Hata hivyo, ni vigumu sana kupima kwa usahihi makadirio ya gharama ya shughuli yoyote ya kielimu.

Litakuwa ni suala muhimu sana kuona matokeo na mwelekeo wa utafiti huo. Hakuna matokeo yoyote yanayojulikana kwa sasa ambayo yameishachapishwa (Fyle, 2003). Kwa hivyo, kuna haja ya kuwekea mkazo au kupitia tena sera ya lugha nchini Uganda kwa kuandaa hati ya sera wazi ya kitaifa ya elimu bora kwa wote. Sera lazima kwa kiasi kikubwa ishughulikie masilahi na kushirikisha jamii ambazo humiliki na kutumia lugha husika. Mbinu kama hizo zinahitaji sera za lugha za kiutendaji katika elimu ambazo zinafaa zizingatie misingi ya kitamaduni na kikabila kwa ajili ya kupata uelewa wa maarifa ya kiasili ambayo yamejumuishwa katika lugha hizi. Hili linabainishwa wazi katika nadharia ya upangaji lugha ya Haugen (1966,1983) kuwa uchaguzi wa msimbo lazima upewe kipaumbele katika maendeleo yoyote ya lugha. Huu ndio uchaguzi na utekelezaji wa sera ya lugha kwa madhumuni maalumu. Hali hii inahusishwa na hadhi rasmi au majukumu ya kitaifa katika upangaji wa lugha kihadhi. Kwa hivyo, suala kama hili linapaswa kuongoza Uganda katika juhudi zake za kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili hasa kupitia sekta ya elimu.

6.5 Utoaji wa Vifaa vya Kutosha vya Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili

Suala hili liliibuka sana katika majibu ya washiriki takribani wote. Kwa hivyo, ilipendekezwa kuwa serikali na wadau wengine wanaohusika wanapaswa kuandaa na kusambaza vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia Kiswahili katika taasisi zote za elimu. Iidhaniwa kwamba upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya kutosha, kama vile vitabu vya kiada, vitabu vya wanafunzi, miongozo ya walimu na vifaa vingine kutarahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Suala hili pia litawafanya wanafunzi na walimu kutia ari katika somo la lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, walipendekeza kwamba serikali ingefaa kujikita zaidi katika uandalizi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia hasa kwenye ngazi ya sekondari ambapo vifaa vya Kiswahili kwa kiasi kikubwa havikutosha. Aidha, washiriki walipendekeza kwamba serikali inafaa kuwaunga mkono waandishi wa Kiswahili wazawa wa Uganda katika juhudi zao za kuandika na kuchapisha vifaa vya Kiswahili vinavyorejelewa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Baadhi ya washiriki pia walipendekeza kwamba inabidi serikali kununua vitabu vya waandishi wazawa wa Uganda kwa ajili ya kukuza uwekezaji, utafiti, na kuendeleza tasnia ya uandishi nchini Uganda. Suala hili litaendeleza uandaaji wa vifaa vinavyozingatia muktadha wa Uganda badala ya kuwekeza sana katika vifaa vya kurejelea kutoka nje ya nchi. Maoni haya ni dhahiri katika nukuu hizi:

Nukuu 31

Kiingereza

Okay, we might say that the learner's materials are not there, but I want to tell you that it's not the learners' materials, it's the government if by will flags off Kiswahili, publishers, printers, writers are all there. Just release it and people will write books, so long as you don't embrace it via that, then who will write? Because they don't see the market for it! But we are able to write books in English language, I mean here in Uganda without the governments consent and publishers publish them, why can't it happen to Kiswahili? Just putting that moderate situation where Kiswahili freely competes, allow it! Then you will see the magic that this language carries. Yeah, stakeholders will help the government in putting some of these things in place. (IP3).

Kiswahili

...tunaweza kusema kwamba vifaa vya kufundishia havipo, lakini nataka kukwambia kuwa changamoto yenyewe siyo vifaa. Ikiwa serikali itatekeleza uendelezaji wa Kiswahili, wachapishaji na waandishi wako. Iwapo serikali itatangaza utekelezaji wa Kiswahili, basi waandishi wataanza kuandika kwa sababu watakuwa wameanza kutarajia soko la vitabu. Ikiwa vitabu katika lugha ya Kiingereza vimewezwa kuandikwa na kuchapishwa hapa Uganda hata bila mkono wa serikali, kwa nini haiwezi kutokea kwa Kiswahili? Hali inafaa kuwekwa tu sawa ambapo Kiswahili kitakuwa huru

kushindana, hata hivyo wadau watasaidia serikali kutayarisha baadhi ya vifaa hivi.(MT3)

Nukuu 32

Kiingereza

...However, we need the strength of the political will. ...When he declared that COVID -19, schools are closed, it happened. But all in the name of saving the lives of Ugandans. If he said that for example, by 2023 or 2025, I want to see P7 writing national exams in Kiswahili, don't think about shortage of materials, people would write and people would buy. But the same applied in 1969 when Nyerere was talking about Kiswahili in Tanzania, he banged the table the same way! We are waiting for a similar banging...writers would write, publishers would get hold of the business, parents would find a way of adjusting their budgets, the way they are buying masks, teachers would automatically be taken on, and they would be teaching the language. So all the strategies rotate on political will (IP9).

Kiswahili

... Hata hivyo, tunahitaji nguvu ya utashi wa kisiasa. ... kwa mfano Rais alipotangaza kuwa shule zifunge kwa sababu ya Ugonjwa wa virusi vya korona (UVIKO-19) jambo hili lilitokea papo hapo. Haya yote aliyafanya kwa ajili ya kuokoa maisha ya Wanauganda. Kwa hivyo, iwapo angesema kwamba, ifikapo mwaka 2023 au 2025, anataka kuona wanafunzi wa darasa la saba wakiandika mitihani ya kitaifa ya Kiswahili, suala la ukosefu wa vifaa halitakuwa kisingizio. Watu wataandika na wengine watanunua. Mbinu na hali kama hiyo ilitumika nchini Tanzania mnamo 1969 wakati Nyerere alipozungumzia Kiswahili, alitamka na shughuli ilitekelezwa moja kwa moja. Kwa hivyo, tunahitaji juhudi kama hizo. Waandishi wangeandika, wachapishaji wangeshikilia biashara, wazazi wangepata njia ya kufanya marekebisha katika bajeti zao kama vile wanavyofanya kununua barakoa za wanafunzi shuleni za kujikinga virusi vya ugonjwa wa korona. Pia, walimu wangeajiriwa moja kwa moja kufundisha lugha. Kwa hivyo mikakati yote inategemea utashi wa kisiasa (MT9)

Kama ilivyoielezwa na washiriki, serikali ya Uganda na wadau wengine husika wanapaswa kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia kwa taasisi zote za elimu nchini Uganda. Imebainika kuwa matokeo ya uhamasishaji kuhusu uandishi na tafsiri za vitabu katika Kiswahili, kumechangia ukuaji wa istilahi za Kiswahili na kuongezeka kwa vifaa vya kujifunzia nchini Tanzania (Mulokozi, 2016). Kwa hivyo, iwapo mfano huo ungeigwa na kutekelezwa

hapa Uganda, kukua na kukuza lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu kunaweza kuimarishwa.

Ogechi & Bosire-Ogechi (2002) wanakiri kwamba elimu, hasa elimu rasmi, inahitaji vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika masomo na taaluma zote katika ngazi zote za kielimu. Kuchapisha kwa lugha ya mawasiliano mapana hakutapunguza tu gharama ya uchapishaji bali pia vifaa au vitabu vitawafikia watu wengi. Aidha, maoni haya yanakubaliana na vipengele muhimu vya nadharia ya upangaji lugha ya Haugen kwamba ili kukuza na kuendeleza lugha, mchakato wa usanifishaji unapaswa kupewa kipaumbele kwa kuwa ndio hujumuisha uandaaji na utoaji wa kamusi za lugha, vitabu, sarufi, miongozo ya mitindo, uakifishaji na miongozo ya matamshi.

6.6 Kukubali na Kuthamini Mtaala Mpya wa Sekondari Unaozingatia Umilisi

Mkakati mwingine wa kiutendaji ambao ulizungumziwa na washiriki ni kupitishwa kwa mtaala mpya unaozingatia umilisi wa wanafunzi. Washiriki hasa watungaji sera walihimiza wadau wote wa elimu kuunga mkono na kuthamini mtaala mpya unaozingatia umilisi hasa kwenye kiwango cha sekondari (kidato cha kwanza hadi cha nne) ambapo lugha ya Kiswahili ni somo la lazima. Walidai kwamba mtaala mpya unaozingatia umilisi, ni fursa nzuri ya kukuza lugha ya Kiswahili kote nchini. Washiriki wengi waliamini kuwa ukuaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili utaimarishwa kupitia sekta ya elimu kwani mtaala unaozingatia umilisi unapendekeza lugha ya Kiswahili kama mojawapo ya masomo kumi ya lazima katika kidato cha kwanza na cha pili. Mawaidha haya yanadhihirishwa katika nukuu zifuatazo:

Nukuu 33

Kiingereza

Now for me I see actually if we go by this new curriculum, you know. actually I like the curriculum you know people have tried to come up with talks about this and that, if the government actually supports this new curriculum that has been developed by the NCDC, it is a

very good curriculum for all the subjects that I should say, when we come to our Kiswahili..... because the competence, the major competence is to communicate, can communicate in Kiswahili, can he address the gathering in Kiswahili, can he maybe write a letter, do work? Communicate actually. (IP2).

Kiswahili

Sasa kwangu mimi, ninaona kweli tunafaa kufuata na kukubali mtaala huu mpya. Ndiyo, kuna baadhi ya watu wamejaribu kuuzungumzia vibaya lakini mimi ninaupenda sana. Ikiwa serikali itaunga mkono mtaala huu mpya ambao umetengenezwa na NCDC, ni mtaala mzuri sana kwa masomo yote. Tunapozungumzia Kiswahili chetu, ni mtaala mzuri sana kwa sababu lengo lake kuu ni kukuza stadi ya kuwasiliana, je! Mtu anaweza kuwasiliana katika Kiswahili, anaweza kuhutubia mkutano katika Kiswahili, anaweza kuandika barua, kufanya kazi? Yaani, muhimu ni mawasiliano (MT 2).

Inapendekezwa kwamba ikiwa Kiswahili kingekuwa lugha ya kufundishia katika elimu kwa ngazi ya shule za upili, na Kiingereza kufundishwa kama lugha ya kigeni, hali hii pia ingekuza lugha zote mbili bila kutatanisha mchakato wa ujifunzaji (Rubagumya, 1991). Nchi nyingi za Kiafrika zimeelekea katika matumizi ya lugha za kiasili katika sera ya elimu pamoja na kupendekeza lugha za Kiafrika katika elimu; hata hivyo upatikanaji wa ustadi wa kusoma na kuandika katika elimu haujafanikiwa kwa ukamilifu (Muzoora et al., 2014). Kwa hivyo, hali hii inazusha utetezi wa sera za lugha katika elimu kuhama kutoka ukopaji wa sera za kikoloni na kuwa sera za kiutendaji ambazo zinajikita katika ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi. Kwa kweli, Sera ya lugha ya Uganda bado ina mizizi katika sera za lugha za kikoloni ambazo zinapendekeza matumizi ya lugha za kiasili kwa madarasa ya chini ya shule za msingi au matumizi ya lugha ya kigeni kutoka darasa la kwanza la shule na kuendelea.

6.7 Kuandaa na Kufungua Vituo vya Kujifunzia Kiswahili katika jamii

Ilipendekezwa kuwa serikali na vyombo vingine vinavyohusika vinapaswa kufungua vituo vya kujifunzia Kiswahili katika jamii mbalimbali ili kusaidia kuenea na

kukubalika kwa lugha ya Kiswahili katika jamii wanamoishi wanafunzi. Washiriki walidhani kuwa huu utakuwa mkakati madhubuti wa kubadilisha mtazamo hasi wa watu juu ya Kiswahili na kukikubali. Walitumai kuwa kufungua vituo vya kujifunzia vya jamii kutawawezesha wazazi kusaidia watoto wao kuimarisha ujuzi na kujizoeshwa kuzungumza ikiwa watachagua Kiswahili katika kiwango chochote cha elimu yao.

Nukuu 34

Kiingereza

..... if the government would come up and encourage the teaching of Kiswahili to the local, the public, like the business community, because the business community needs it, if they would open up actually like that and they encourage the community, public, these business people maybe open some learning centers where they would be just going to study on how to communicate in Kiswahili basically that, it would be a good, venture actually. Previously, I hear the parliament used to have those programs where they used to learn Kiswahili, I do not know how far they went, such programs we really need them as a country (IP2).

Kiswahili

...Iwapo serikali ingetoa uhamasishaji juu ya ufundishaji wa Kiswahili kwa wanajamii, kwa mfano, jamii za wafanyabiashara, kwa sababu wanahitaji lugha ya Kiswahili. Ikiwa wangefungua vituo vya kujifunzia na kufundishia kama hivyo, wangeenda tu kujifunza jinsi ya kuwasiliana katika Kiswahili na hilo lingekuwa jambo zuri. Hapo awali, nilisikia bunge lilikuwa na mpango kama huo ambapo walikuwa wakijifunza Kiswahili, lakini kwa sasa sijui mambo yalikoishia. Mipango kama hiyo tunahitaji kama nchi. (MT2).

Nukuu 35

Kiingereza

If I go to adult literacy, you create some classes outside the school. Then you get some older people either the business community or whichever group, or some are in the offices and you create time for them, you create time and then those ones are taught Kiswahili. That would be the best strategy, because to remove that negative attitude of the language, most of them think that the language is hard. But when you meet them like for a month they change and know that the language can be learnt easily (IP 4).

Kiswahili

...Nikizungumzia kusoma na kuandika kwa watu wazima, unaweza kuandaa darasa katika jamii. Halafu unashirikisha watu wazima, labda jamii ya wafanyabiashara au kikundi cha watu chochote

kingine au hata wengine kama maafisa na unawatengea muda wa kuwafundisha Kiswahili. Huo ungekuwa mkakati bora wa kuondoa mtazamo hasi kuhusu lugha hiyo, wengi wao hufikiria kuwa Kiswahili ni lugha ngumu lakini ukiwafundisha kwa mwezi kama mmoja, watabadilika na kutambua kuwa lugha ya Kiswahili ni rahisi kujifunza ... (MT 4).

Wanajamii na wazazi wenye ari watafundishwa kwa ajili ya kusaidia wanafunzi ambao lugha yao siyo lugha ya wengi katika eneo hilo (Owu-Ewie, 2006). Ssekamwa na Lugumba (2001: 8) wanadai kwamba watetezi wengine wa matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za Uganda ni pamoja na Hussey, Mkurugenzi wa Elimu ambaye aliona Kiswahili kama lugha inayoweza kupunguza changamoto za mawasiliano katika makabila yote na katika jamii mbalimbali katika eneo la Afrika Mashariki.

Mikakati ya ukuzaji wa Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini uganda imedhihirishwa katika kielelezo 6.2 kinachofuata;



Kielelezo 6.2: Suluhu za changamoto zinazokumba ukuaji wa kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini uganda

Kielelezo kilicho hapo juu kinafupisha suluhu au mikakati saba ambayo washiriki katika utafiti huu waliamini itaendeleza ukuaji bora wa lugha ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu.

6.8 Muhtasari wa Sura

Sura hii imewasilisha data juu ya mikakati ya ukuzaji bora wa Kiswahili au suluhu za changamoto zilizokumba ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa

elimu. Katika sura inayofuata, tutaangazia muhtasari wa matokeo, hitimisho, na mapendekezo. Aidha, mawanda ya utafiti zaidi pia yalipendekezwa.

SURA YA SABA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, hitimisho pamoja na kueleza mchango wa utafiti na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

7.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza sera ya lugha katika elimu na kutathmini mchango wake katika ukuzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Data zilikusanywa zikilenga kujibu maswali matatu ya utafiti: Sera ya lugha nchini Uganda ina nafasi gani kuhusu uendelezaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu? Je! Ni changamoto zipi zinazokabili maendeleo ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu nchini Uganda? Je! Ni masuluhisho yapi yanayoweza kutatua changamoto zinazokumba ukuaji wa Kiswahili nchini Uganda kupitia mfumo wa elimu. Data zilizalishwa kutoka kwa sampuli ya makusudi ya washiriki 13 kwa kutumia njia ya mahojiano ya kina, upekuzi wa nyaraka za maktabani na uchambuzi wa yaliyomo ya nyaraka mbalimbali za sera ya lugha. Baadhi ya mahojiano yalikuwa ya ana kwa ana, na wakati mwingine kwa sababu ya janga la ugonjwa wa virusi vya korona (UVIKO-19) lililogubika dunia nzima wakati huo, mahojiano mengine yalifanyika kupitia mikutano ya *zoom* mtandaoni, kupiga simu na kwa kutumia dodoso isiyo funge kupitia baruapepe. Utafiti huu ulifanyika wilayani Kampala, Uganda kwa kutumia watunga sera, waratibu wa lugha na watekelezaji wa sera za lugha kama washiriki wa utafiti huu.

Kwa matumizi ya nadharia ya hatua tano za uchanganuzi wa data kimaudhui ya Braun na Clark (2006), maudhui yaliundwa kulingana na data zilizojibu maswali matatu ya utafiti. Aidha, nyaraka na hati mbalimbali zilipekuliwa pamoja na yaliyomo yake kuchambuliwa.

7.2 Matokeo na Mahitimisho ya Utafiti

Ufuatayo ni muhtasari wa maudhui yote yaliyozalishwa katika uchanganuzi wa data pamoja na mahitimisho kwa mujibu wa kila lengo la utafiti. Muhtasari wa matokeo kutokana na upekuzi na ukaguzi wa hati mbalimbali pia umewasilishwa.

7.2.1 Nafasi ya sera ya lugha katika ukuzaji na ukuaji wa Kiswahili kupitia mfumo wa elimu nchini Uganda

Kupitia uhakiki wa kina wa nyaraka za sera, zenye matamko yaliyojijhusisha na ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda kupitia sekta ya elimu, ilikuwa dhahiri kwamba maendeleo ya lugha ya Kiswahili yanategemea sera nyingi za lugha, matamko na amri za kisiasa.

Aidha, ukaguzi na uchambuzi ulifanyika kwenye mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliosainiwa tarehe 30 Novemba 1999 na kuanza kutumika mnamo tarehe 7 Julai 2000 kufuatia kuridhiwa kwake na nchi tatu wanachama waanzilishi: Kenya, Uganda na Tanzania. Katika mkataba huu, ilikubaliwa kati ya nchi wanachama kwamba Kiswahili kitakuwa lugha ya mawasiliano katika Jumuiya ya Afrika mashariki. Pamoja na hilo, Katiba ya Uganda iliyofanyiwa marekebisho mnamo 2005 kwa mujibu wa kifungu cha 261, kinatamka kwamba: Kiswahili kitakuwa lugha ya pili rasmi nchini Uganda na kitatumika katika hali au miktadha itakayoamuliwa na bunge kisheria.

Hati nyingine iliyopitiwa ni mtaala wa kwanza wa Kiswahili ulioasisiwa na Kituo cha Kitaifa cha Ukuzaji wa Mitaala mnamo 2008 baada ya Kiswahili kufundishwa kwa miaka mingi nchini Uganda bila mtaala wa kufundishia. Katika 2019, wizara ya Elimu na Michezo kupitia Kituo cha Kitaifa cha Ukuzaji Mitaala iliasisi na kutangaza mtaala mpya unaozingatia umilisi wa wanafunzi kwa shule za upili. Mtaala mpya wa

ngazi ya chini ya sekondari yaani kidato cha kwanza hadi cha nne, unaonyesha kuongezeka kwa idadi ya masomo ya lazima ikiwemo lugha ya Kiswahili.

